

**UCHANGANUZI WA USEMI KATIKA SAJILI YA  
DINI:SIFA BAINIFU ZA LUGHA YA MAHUBIRI**

**NA: NDUNG'U VERONICAH**

**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA CHUO KIKUU  
CHA KENYATTA**

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya  
uzamili (Master of Arts) katika Chuo Kikuu cha Kenya.

2001

Ndung'u, Veronicah  
*Uchanganuzi wa usemi  
katika sajili ya*




02/262423

**KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.



---

VERONICAH W. NDUNG'U

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii wa chuo kikuu.



---

DKT. PAUL M. MUSAU



---

DKT. KIMANI NJOGU

**KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY**

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa babangu Dominic Ndung'u na mamangu Jane Muthoni.

Natabaruku kazi hii pia kwa ndugu zangu Wanjiru, Nyambura, Kimani, Wanjiku na

Muiruri kwa kunipa moyo wa kuendeleza masomo yangu.

Mada .....	i
Ungamo .....	ii
Tabaruku .....	iii
Yaliyomo .....	iv
Shukrani .....	vii
Ikisiri .....	viii
Istilahi na vifupisho .....	x
<b>2.0 Malisho wa vifupisho</b>	
SURA YA KWANZA .....	1
UTANGULIZI .....	1
1.0 Utangulizi .....	1
1.1 Misingi ya utafiti .....	1
1.2 Suala La Utafiti .....	2
1.3 Malengo ya Utafiti .....	3
1.4 Sababu za Kuchagua Mada .....	4
1.5 Upeo na Mipaka .....	5
1.6 Misingi ya Kinadharia .....	6
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Hii.....	10
1.8 Mbinu za Utafiti .....	14
1.8.1 Ukusanyaji wa Data .....	15
1.8.2 Mbinu za Uchanganuzi wa Data .....	15
1.9 Kuhusu Data ya Uchanganuzi .....	16
<b>SURA YA PILI</b> .....	
2.0 RUWAZA ZINAZOJITokeza KATIKA LUGHA MAHUBIRI .....	17
2.1 Utangulizi .....	17
2.2 Mwanzo wa Mahubiri .....	18
2.3 Utangulizi wa Somo .....	22
2.4 Matumizi ya Maswali .....	24
2.4.1 Maswali ya Balagha .....	25
2.4.2 Maswali ya Kuwatahadharisha Waumini Wawe Makini .....	28

2.4.3	Maswali ya Kujitathmini .....	30
2.4.4	Maswali Mengine .....	31
2.5	Matumizi ya Mifano Kueleza Ujumbe .....	32
2.6	Takriri .....	34
2.7	Matumizi ya Ishara .....	36
2.8	Matumizi ya Sauti .....	37
2.9	Mwisho wa Mahubiri .....	39
2.9.1	Kuashiria Mwisho wa Mahubiri .....	39
2.9.2	Kutamatisha mahubiri .....	42
2.9.3	Hitimisho .....	43
SURA YA TATU .....		46
3.0	KUCHANGANYA MSIMBO .....	46
3.1	Utangulizi .....	47
3.2	Uambatishaji wa Kiungo .....	47
3.3	Kuchanganya Msimbo Kati ya Sentensi .....	49
3.4	Kuchanganya Msimbo Miongoni mwa Sentensi .....	52
3.5	Ufafanuzi kuhusu Kuchanganya Msimbo Na Maelezo ya Kiisimu .....	54
3.6	Dhima ya Kuchanganya Msimbo .....	57
3.6.1	Ufafanuzi .....	57
3.6.2	Kusisitiza .....	58
3.6.3	Unukuzi .....	60
3.7	Hitimisho .....	61
SURA YA NNE .....		63
4.0	MSHIKAMANO KATIKA LUGHA YA MAHUBIRI .....	63
4.1	Utangulizi .....	63
4.2	Dhana ya Mshikamano .....	63
4.3	Aina za mshikamano .....	65
4.3.1	Urejeshi .....	65

4.3.2 Ubadilishaji na Udondoshi .....	72
4.3.2.1 Ubadilishaji .....	73
4.3.2.2 Udondoshi .....	75
4.3.3 Uunganishi .....	79
4.3.4 Msamiati .....	82
4.3.5 Hitimisho .....	88
SURA YA TANO .....	92
HITIMISHO .....	92
5.1 Malengo na Matokeo ya Utafiti .....	92
5.2 Mapendekezo .....	96
MAREJELEO .....	98
KIAMBATISHO I .....	104
KIAMBATISHO II .....	133
KAMBITISHO III .....	136

## SHUKRANI

Kwanza kabisa ningependa kutoa shukrani zangu kwa daktari P.Musau na daktari K.Njogu kama wasimamizi wangu. Kutokana na mwongozo wao wenye busara pamoja na ushauri wao, niliweza kuimaliza kazi hii. Shukrani zangu zamwendea tena daktari P.Musau kwa ushauri alionipa nilipokuwa nikifunza katika shule ya upili kuhusu kuendeleza masomo yangu. Ni kupitia ushauri huu ambapo niliweza kujisajilisha kwa kozi hii.

Pili, ningependa kuwashukuru wahadhiri wangu wote katika idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika kwa kunifundisha na kunitia moyo masomoni. Baadhi yao ni profesa Kinge'i, Bw. Chacha na Bw. Matti ambao kwa ushauri wao wa hekima nilifaidika mno. Siwezi kuwataja wote hapa lakini nasema asante kwenu nyote.

Nashukuru tume ya kuajiri walimu nchini kwa kunipa likizo ili kuifanya kazi hii. Hali kadhalika, nawashukuru wanafunzi wenzangu Beth, Wambua na Kisia ambao walinasaidia sana hasa wakati mambo yalikuwa magumu.

Aidha, ningependa kuwashukuru dada zangu na ndugu zangu pamoja na marafiki zangu ambao walinipa hima ya kuimaliza kazi hii.

Siwezi kusahau kuwashukuru wazazi wangu, babu yangu Kibugi na Fr. Alfonso kwa kunipa msukumo na hamasa ya kuendelea na masomo yangu.

Mwisho lakini si haba, namshukuru Bi Eunice Wambui kwa kuniruhusu kutumia kompyuta yake na Mrs Gitau kwa usaidizi wake.

## IKISIRI

Katika tasnifu hii, tumechunguza sifa bainifu za lugha ya mahubiri kama zinavyojitokeza katika sajili ya dini katika lugha ya Kiswahili. Tumetumia data kutokana na mahubiri mbalimbali na kuyachanganua ili kudhihirisha sifa zake. Utafiti huu ulikuwa na malengo mawili ambayo ulitekeleza. Kulikuwa na utambuzi wa sifa bainifu za lugha ya mahubiri na utambuzi wa aina za mshikamano na jinsi zinavyounganisha mahubiri. Katika kufanya hivi, mtazamo wa kimtindo na wa mshikamano katika nadharia ya uamilifu wa lugha ilitumika.

Sura ya kwanza ambayo ni utangulizi wa tasnifu imeshughulikia swala la utafiti, sababu za kuchagua swala lenyewe, madhumuni ya utafiti, upeo wa utafiti, misingi ya kinadharia, yaliyoandikwa kuhusu somo lile na mbinu za utafiti. Ni katika sura ya pili ambapo tumejishughulisha na baadhi ya sifa bainifu katika lugha ya mahubiri kama vile jinsi wahubiri wanavyoanza mahubiri yao, njia wanazotumia kuendeleza ujumbe, na namna wanavyohitimisha. Kutokana na uchunguzi wetu tuligundua ya kwamba kuna mianzo maalum ya kuanza mahubiri. Kwa jumla wahubiri huanza kwa maamkuzi na pia kutaja kiini cha ujumbe wao. Wahubiri hutumia njia nyingi kuendeleza ujumbe kama vile matumizi ya mifano takriri, kubadilisha sauti, maswali na kadhalika. Pia, kuna njia maalum za kutamatisha mahubiri. Katika kila ruwaza iliyojadiliwa, maelezo ya kiisimu yametolewa.

Sura ya tatu yaonyesha kuwa mahubiri yana sifa ya kuchanganya msimbo. Kuchanganya msimbo kumeshughulikiwa kama mojawapo ya sifa bainifu katika kuendeleza ujumbe.

Aina muhimu za kuchanganya msimbo na jinsi zinavyojitokeza katika matini za uchanganuzi zimejadiliwa.

Sura ya nne yaonyesha kuwa lugha ya mahubiri ina aina mbalimbali za mshikamano. Kwa mfano, kuna mshikamano wa kimsamiati, urejeshi, uunganishi, ubadilishaji na udondoshi.

Sura ya tano na ya mwisho inajumuisha muhtasari na matokeo ya utafiti kwa jumla. Mapendekezo ya utafiti mwingine unaoweza kufanywa katika uwanja huu pia yamewekwa katika sura hii.

## ISTILAH NA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

- 1) Usemi: mpangilio unaokiuka sentensi ambao ni tendo la mawasiliano, na ambao una muundo na uamilifu.
- 2) Matini: sehemu ya usemi ambayo hupewa umbo na usemi wote kwa jumla.  
Matini ya usemi ni mfumo wa ishara za kiisimu za mawasiliano ambazo zaweza kuwa zimeandikwa au kusemwa. Katika muktadha huu, zile ambazo zimesemwa.
- 3) Sajili: lugha itumikayo katika muktadha fulani.
- 4) Mtindo: utambuzi wa mpangilio wa maumbo ya kiisimu katika matini na athari zinazotolewa katika mahusiano ya utoaji na upokezi wa matini.
- 5) Mshikamano: uhusiano wa karibu ambao hutegemea sarufi au maana katika sehemu fulani za sentensi moja.
- 6) Lugha ya litajia: lugha ya kawaida inayotumika katika ibada na sala za dini.
- 7) Lugha ya thiolojia: lugha inayotumika katika elimu ya dini.
- 8) TY : Tafsiri Yangu
- 9) [...] : Neno ambalo halikueleweka katika matini zilizorekodiwa

# **SURA YA KWANZA**

## **UTANGULIZI**

### **1.0 Utangulizi**

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchanganua lugha ya dini, kama inavyojitokeza katika hotuba za mahubiri. Utafiti huu utachanganua matini za kidini kwa kuzingatia muktadha. Uchanganuzi huu unahusu miundo ya kiisimu pamoja na uamilifu wa lugha ya kidini, kama anavyosema Brown na Yule (1983:1):

Uchanganuzi wa usemi unahusu lugha hasa katika matumizi yake. Kwa hivyo hauwezi kubanwa katika kuelezea maumbo ya kiisimu bila ya kuangalia maumbo hayo yana uamilifu gani katika maisha ya binadamu (Tafsiri Yangu-TY).

Utafiti huu ni uchanganuzi wa data iliyopatikana kutoka kwa wahubiri mbalimbali. Katika kuchanganua data hii, utafiti umechunguza sifa bainifu za lugha ya mahubiri kutokana na ruwaza zilizojitokeza. Yaani, utafiti huu umeangalia ruwaza zinazojitokeza na majukumu ya ruwaza hizi katika usemi.

### **1.1 Misingi Ya Utafiti Huu**

Katika historia ya isimu, kumekuweko na mtazamo kuhusu lugha kama mfumo wa fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki ambao haukuhusisha miktadha ya matumizi. Matawi mengi ya isimu yamechangia katika kubadilisha mitazamo hii ya jadi na kuelekeza kuwa muktadha wa matumizi ya lugha ni muhimu sana na lazima uhusishwe

katika uchanganuzi wa lugha. Haya yanaoana na maoni ya Halliday (1964:76) anayesema kuwa;

Lugha hudhihirika katika tajiriba za kijamii (na wala si katika ombwe). Na papo hapo ndipo inapata misingi, sura na ruwaza zake. Uamilifu mkubwa wa lugha kama tukio la jamii ni matumizi yake kama tukio la mawasiliano baina ya wanajamii. Tamko la lugha haliwezi kueleweka ipasavyo ikiwa litafasiriwa pekee pasipo kuhusishwa na maswala mengi ya mkutadha na hali ya watu waliohusika, ujuzi wao, mahusiano kati yao, mada inayozungumziwa, uwanda wa taaluma, mahala au mazingira waliyomo na masharti mengine mengi. (TY).

Utafiti umefanywa katika matawi mengi ya isimu kama vile Isimu-jamii, Uchanganuzi wa usemi, Uchanganuzi wa matini na pia Ethinografia ya mawasiliano. Tufiti hizi zimechunguza lugha kwa kukiuka mipaka ya sentensi na kuangalia mipaka ya matumizi na kanuni za unakidi. Utafiti uliofanywa katika tasnifu hii umefuata misingi kama hii.

Dini huonyesha lugha changamano ambayo wahubiri hutegemea katika kushawishi na kuwapa waumini wao moyo wa matumaini. Maandishi yalioandikwa kuhusu sajili ya dini yanaonyesha uwanja mkubwa ambamo kuna uwezekano wa utafiti usio kikomo (Crystal 1965; Crystal na Davy 1969; Smith 1993; Watts 1989).

## **1.2 Suala La Utafiti**

Utafiti mwingi umefanywa katika sajili ya dini. (Crystal, 1965; Crystal na Davy, 1969; Smith, 1993 na Watts, 1989). Hata hivyo, hakuna utafiti ambao tunaufahamu katika lugha

ya Kiswahili ulioshughulikia sifa bainifu katika sajili ya mahubiri. Utafiti huu ulidhamiria kujaza pengo hili kwa kuangalia mikakati ya usemi katika lugha ya mahubiri. Umefanya hivi kwa kujaribu kuelezea, kuchanganua na kufasili baadhi ya vipengele vya lugha ya dini. Lugha ya dini kama lugha zingine huwa na mpangilio fulani ambao ni wa kipekee. Uchunguzi wa kutafuta sifa bainifu za lugha hii na jinsi inavyofanya kazi katika mawasiliano ya binadamu ni jambo muhimu na la kiusomi.

Mambo ambayo yanaangaliwa na utafiti huu ni sifa za kimtindo ambazo huitambulisha lugha hii na kuitofautisha na zingine. Bali na vipengele vya kimtindo, kuna maswala yanayohusu uhusishi na uunganishi. Kwa mfano mambo yanayoonyesha mshikamano. Mshikamano ni nyenzo muhimu katika lugha ya mahubiri. Mahubiri yanayotolewa lazima yawe na mshikamano ikiwa yatahitajika kutimiza mawasiliano. Utafiti huu unakusudia kujibu maswali yafuatayo:

- a) Je, lugha ya kidini hasa mahubiri hutambulishwa na sifa zipi bainifu?
- b) Je, katika Kiswahili, ni vipengele vipi vya mshikamano vinavyojitokeza katika lugha ya kidini? Vipengele hivi vinaunganisha vipi vipande vya usemi?

### **1.3 Malengo Ya Utafiti**

Utafiti huu unakusudia kutimiza malengo yafuatayo;

- a) Kutambua sifa bainifu za lugha ya mahubiri katika Kiswahili.
- b) Kutambua aina za mshikamano na jinsi zinavyounganisha lugha ya mahubiri.

#### 1.4 Sababu Za Kuchagua Mada

Lugha ni chombo kinachotumiwa na wahubiri kufikia malengo yao. Matumizi mazuri ya lugha yanaweza kutofautisha mhubiri mmoja na mwingine. Kulingana na Brown na wenzake (1963:158):

Mhubiri mwenye hamasa hutumia lugha ambayo ina uhalisi. Hasemi mambo yasio na msingi, yasio na urazini...ana nguvu za kuamsha urazini wa wanadamu. Yeye huongea kwa ukakamavu! (TY).

Utafiti umefanywa ili kuonyesha mtindo katika lugha ya dini hasa lugha ya litajia (Crystal na Davy 1969). Hata hivyo, utafiti huu haukuangalia mshikamano kama nyenzo kuu katika lugha hii. Na kama Crystal na Davy (1969:41-42) wanavyosema:

Tunahisi kuwa kuna mengi ya kusemwa kuhusu vile sajili tofauti hutumia uhusishi wa sentensi...lakini kwa maoni kuwa hakuna kazi iliyofanyiwa mambo hayo, ... kinachoweza kufanywa ni makisio tu...hivyo, kipengele cha kisarufi katika maelezo yetu kimeachwa (TY).

Hivyo, ingawa dini imekuwa chombo muhimu kinachoongoza maisha ya binadamu na njia kuu ya kuiwasilisha ni lugha, sajili hii haijaangaliwa kiusomi hasa kwa upande wa lugha ya Kiswahili. Kwa sababu hiyo, utafiti huu ni muhimu kwa sababu unaonyesha sifa bainifu katika lugha ya mahubiri ambayo haijashughulikiwa na tafiti zingine. Haya yamefanywa kupitia ruwaza zinazojitokeza na dhana ya mshikamano. Vilevile, utafiti huu unaonyesha jinsi lugha ya Kiswahili inavyojiwakilisha katika sajili hii. Matokeo ya utafiti huu yatakuwa muhimu kwa wanaisimu, wanafunzi wa isimu inayohusiana na

matini na hata wahubiri hasa wanapopanga mahubiri yao. Aidha, utafiti huu ni muhimu pia kwa sababu unaongezea idadi za tafiti za uchanganuzi wa matini katika lugha ya Kiswahili.

### **1.5 Upeo Na Mipaka**

Utafiti huu unahusu sajili ya dini. Hata hivyo, lazima ieleweke kuwa sajili ya dini ni pana sana na inaweza kugubika eneo pana. Kwa mfano maombi, ushiriki katika kusoma Biblia na kadhalika. Utafiti huu unajishughulisha na sehemu ya mahubiri tu, inayohusisha mhubiri na wahubiriwa.

Utafiti huu unajishughulisha na mahubiri ya ana kwa ana. Mahubiri kama haya yanaweza kuwa na muundo wake tofauti yakilinganishwa na yale yanayotolewa kupitia vyombo vya habari. Fauka ya hayo, sajili ya dini inajumuisha aina nyingi za dini. Kwa mfano Kikristu, Kiislamu, Kihindu na kadhalika. Katika utafiti huu, dini ya Kikristu ndiyo iliyoshughulikiwa.

Dini ya Kikristu kwa upande wake huwa na madhehebu mengi ambayo hayawezi kushughulikiwa yote. Madhehebu manne yalichukuliwa ambayo yaliwakilisha makanisa manne. Makanisa haya ni ya Kikatoliki, Kiangilikana, Seventh Day Adventist na Gospel Reedemed Church. Mtafiti alitarajia kwamba makanisa haya yatatoa data ya kutosha kukidhi mahitaji ya utafiti huu kama anavyosema Milroy (1987:21) kuhusu tafiti za lugha:

mpuli kubwa huonekana kama haihitajiki katika tafiti za kiisimu kama katika tafiti zingine. Hii ni kwa sababu tabia za kiisimu zinafanana kuliko aina zingine za tabia zinazochunguzwa na tafiti zingine (TY).

Utafiti huu ulijikita katika sehemu ya Mashariki mwa Nairobi na kushughulikia mitaa ya Kaloleni na Bahati. Sehemu hii ilichaguliwa kwa sababu wakaazi wake ni watu wa asili tofauti wanaotumia Kiswahili. Vilevile, kwa mujibu wa Parkin (1974) kuna ithibati kuwa katika sehemu hii kuna matumizi ya lugha ya Kiswahili. Lugha hii (Kiswahili) hutumika kama njia ya kuwaunganisha watu hawa ambao ni wa asili tofauti. Hii inamaanisha kuwa kupata mahubiri katika lugha ya Kiswahili ni rahisi katika sehemu hii. Hata hivyo, kuna miji mingine ambayo ina sifa hii ya kuwa na watu wa asili tofauti lakini haijafanyiwa utafiti kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili. Hivyo, miji hii haikushughulikiwa. Kila kanisa lilitembelewa mara moja na mahubiri kurekodiwa. Hii ina maana kuwa utafiti ulikuwa na mahubiri manne kama sampuli. (Tazama Kiambatisho I)

## **1.6 Misingi Ya Kinadharia**

Utafiti huu ulitumia nadharia ambayo imejikita katika taaluma ya uamilifu wa lugha. Nadharia hii imefafanuliwa na Halliday (1971). Halliday (1971) anasema kuwa nadharia ya uamilifu wa lugha inajaribu kuelezea muundo wa lugha kama tukio la lugha. Nadharia hii hufanya hivi kwa kurejelea wazo kuwa lugha huwa na jukumu fulani katika maisha yetu. Anaendelea kusema kwamba lugha inahitajika kutimiza aina fulani za mahitaji-bia. Anasema kuwa mkabala huu wa uamilifu wa lugha ni wa manufaa sana kwani hutuungazia mengi kuhusiana na mfumo lugha, na matumizi yake hasa katika muktadha fulani. Kwa hivyo, ikiwa lugha inahitajika kutimiza au kutosheleza mahitaji fulani, basi

haya lazima yadhahirike katika muundo wake. Hii ina maana kuwa uchangamano wa uamilifu wa lugha huenda ukaakisiwa popote katika muundo wa ndani wa lugha yenyewe.

Maoni haya yanaoana na ya Leech na Short (1981) pamoja na Stubbs (1983) ambao wanaitikadi kuwa lugha huwa na uamilifu tofauti hivi kwamba kipande chochote cha lugha huwa ni uteuzi uliofanywa katika daraja mbalimbali za kiuamilifu. Wanasema kuwa maoni kuwa lugha hutumiwa kuwakilisha “fikra” au “mawazo” ni sahili na finyu sana. Wanasema kuwa kuna aina mbalimbali za lugha kutokana na uamilifu wao tofauti. Kwa mfano aina fulani ya lugha huwa na uamilifu wa urejeshi kama vile ripoti za magazeti, aina zingine huwa na uamilifu wa kuelekeza kama maagizo rasmi, kushawishi kama vile lugha ya mahubiri na kadhalika.

Kulingana na Halliday (1971) aina tatu za uamilifu wa lugha hujitokeza. Kwanza, lugha huwa na uamilifu wa uwakilishi ambapo inatumika kuwasilisha “yaliyomo” au mawazo. Pili, lugha ina uamilifu wa kujenga uhusiano kati ya watu. Lugha basi hutumiwa katika kujenga na kudumisha aina zote za uhusiano wa binadamu, huunganisha vikundi vya kijamii na pia hutambulisha mtu binafsi.

Uamilifu wa tatu ni wa matini. Huu ni uamilifu ambao unahusu uundaji wa matini na umo ndani ya lugha. Kupitia kwa uamilifu huu, lugha huunganishwa na muktadha na hivyo huwezesha kupatikana kwa usemi. Kwa mujibu wa Halliday na Hasan (1976:1), matini ni kipashio cha lugha kilichokamilika kisemantiki, kiwe zungumzi au andishi na

chenye urefu wowote. Matini ndio hufanyiwa uchanganuzi wa usemi. Uamilifu wa kimatini wa lugha haujifungi katika kuunda uhusiano baina ya sentensi tu, bali pia huhusika na mpangilio wa ndani wa sentensi, maana yake, pia kuhusiana na muktadha wake.

Utafiti huu ulitumia mihimili yote mitatu ya nadharia ya uamilifu wa lugha. Mhimili wa pili unaonyesha vile mzungumzaji anavyotumia lugha katika kujitambua yeye mwenyewe na kujenga uhusiano na wasikilizaji wake. Hapa ndipo utafiti ulipopata ule mtindo. Kupitia mhimili huu, utafiti ulitumia mtazamo wa kimtindo ambao hulenga kuchanganua lugha ukikusudia kutambua vipashio vya kisiimu ambavyo hutumika katika kila tukio. Crystal na Davy (1969) wamefafanua mtazamo huu na kuelezea kuwa unajaribu kuelezea ni kwa nini vipashio fulani vya kiisimu vinatumika vikipingana na vingine ambavyo vingetumika. Wanaendelea kusema kuwa vipashio hivi vya kiisimu huwekwa katika kategoria kulingana na uamilifu wake katika muktadha wa jamii. Vipashio hivyo ni chochote katika maandishi au mazungumzo ambacho ni cha kipekee katika mfululizo wa lugha. Kwa mfano neno fulani, sehemu ya neno, mfululizo wa maneno, au jinsi ya kutamka neno.

Kupitia mhimili wa kwanza unaonyesha uamilifu wa uwakilishi, na wa tatu ambao unahusu uundaji wa matini ukitilia mkazo kuwa uamilifu huu haujifungi katika kuunda uhusiano baina ya sentensi, mtazamo wa mshikamano ulitumika. Mtazamo huu hudhamiria kutambua ni vipi matini inavyounganishwa na jinsi kipengele kimoja cha usemi kinavyotegemea kingine. Mtazamo huu umeelezwa na wataalamu wengi. Kwa

mfano, Dressler & Beaugrande (1981), Brown & Yule (1983), Werth (1984), Dijk (1977), Njue (1989), Widdowson (1977) na wengine. Hata hivyo, Halliday na Hasan (1976) wamefafanua zaidi. Kulingana na Halliday na Hasan (1976), na Halliday (1985b), mtazamo wa mshikamano huangalia ni nini kinachounganisha matini pamoja. Wanaeleza aina mbalimbali za mshikamano kama vile urejeshi, ubadilishaji, udondoshi, uunganishi na mshikamano wa kimsamiati.

Utafiti huu ulitumia mseto wa mitazamo hii miwili; mtazamo wa kimtindo na mtazamo wa mshikamano katika nadharia ya uamilifu ili kuchanganua namna lugha inavyotumiwa katika sajili ya dini. Nadharia hii iliweza kutosheleza mahitaji ya utafiti huu. Hata hivyo, kuna nadharia zingine ambazo zingetumika katika utafiti wa aina hii, kwa mfano, nadharia ya Ethinografia ya Mawasiliano. Gumperz na Hymes (1972) wamefafanua kuwa huu ni mtazamo wa kiisimu ambao huzingatia muktadha, utamaduni na mazingira tofauti katika jamii ili kuanisha lugha na matumizi yake. Nadharia hii huchunguza vile mawasiliano yanayotumia lugha yanavyoendelezwa. Lengo la kimsingi la nadharia hii ni kuelekeza katika ukusanyaji wa data fafanuzi hasa kwa kuangalia jinsi maana inavyopashwa katika jamii. Nadharia hii hivyo huangalia umilisi wa mawasiliano wa mzungumzaji kwa kulenga jamii- lugha. Kipengele cha upashaji wa maana ni muhimu kwa sababu kinaonyesha lugha hutumika vipi. Hata hivyo, nadharia hii haikutumiwa katika utafiti huu kwa sababu haitilii maanani kwa undani kipengele cha mshikamano ambacho kiliangaliwa na utafiti huu.

Nadharia nyingine ambayo ingeweza kutumika ni ya Grice (1975) ya “makusudio”. Nadharia hii hutumia kanuni ya ushirikisho kama ilivyoelezwa na Pratt (1977). Hii inamaanisha kuwa lazima mtu aseme yanayostahili tu, pia yanayofaa. Grice amependekeza aina nne za mipaka ya mazungumzo.

- i) Lazima yanayosemwa yaelekeze kama inavyostahili.
- ii) Lazima yanayosemwa yawe ya kweli.
- iii) Lazima yanayosemwa yafae.
- iv) Lazima yanayosemwa yasemwe kwa kifupi, yasitanishe na yawe na mipango.

Ikiwa haya hayatafikiwa, anayeongea husemekana kuwa amekiuka kanuni ya ushirikiano. Ingawa nadharia hii ingetumika katika utafiti huu kwa kutoa maelezo ni yapi msemaji angekusudia, angependekeza, au angemaanisha ambayo ni tofauti na yale hasa anayomaanisha haikutumiwa kwa sababu utafiti haukuangalia maana pekee, bali uliangalia sifa za kimtindo na mshikamano kama nyenzo kuu katika lugha ya kidini.

### **1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Hii**

Kuna mengi yaliyoandikwa kuhusu uchanganuzi wa lugha. Kiai (1996) alifanya uchanganuzi wa usemi wa vipindi vya redio kulingana na sajili ya wakulima na hasa lugha ilivyotumika. Mtafiti huyu aliangalia ni vipi lugha ilivyotumika ili ieleweke na wakulima. Vipindi hivi ambavyo vilikuwa katika lugha ya Kiswahili na Gikuyu vilionyesha kuwa maneno mengi ambayo hayakueleweka katika lugha hizi yalitoholewa au yalipatiwa maana ya kitu kilichoeleweka katika jamii ile. Mtafiti huyu alionyesha ni vipi maneno yanavyotumiwa katika sajili hii ili kuwe na uelewano. Tofauti na utafiti wetu, utafiti huu haukuhusisha moja kwa moja msemaji na hadhira.

Michira (1993) alifanya utafiti wa uchanganuzi wa usemi katika lugha ya wachuuzi wa soko la Gikomba na lugha ya matangazo ya biashara redioni nchini Kenya. Kwa kutumia mtazamo wa kimtindo, aligundua kuwa kazi zote mbili zilionyesha kuchanganya msimbo, sintaksia ya lugha zote mbili; ile ya matangazo na ya wachuuzi ni nyepesi na kulikuwa na makosa mengi ya kisarafu. Kazi hii inatofautiana na iliyofofanywa kwa sababu inachanganua lugha ya kibiashara.

Kitsao (1975) alifanya utafiti wa kimtindo katika kazi ya riwaya na tamthilia kadhaa. Akitumia mtazamo wa Crystal & Davy (1969), aliangalia viwango vya semantiki, sarufi na leksia katika kazi alizozichagua. Kazi hii inahusiana na utafiti huu kwa sababu iliangualia mtindo. Hata hivyo, ni tofauti na iliyofofanywa kwa sababu haikugusia lugha ya mazungumzo na haikuangalia dhana ya mshikamano. Hali kadhalika, Kitsao (1982) alitafiti maudhui katika fasihi ya Kiswahili kwa kuangalia tamthilia, riwaya na ushairi. Aliangalia vipengele ambavyo vinaweza kutazamika kama vile urefu wa sentensi, uchanganuano wa sentensi, nambari ya vishazi katika sentensi na kadhalika. Baadaye alitumia data hii kitakwimu. Utafiti huu ulijihusisha na kujaribu kutekeleza mtazamo wa mtindo takwimu. Kazi hii ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu iliangualia mtindo lakini ni tofauti kwa sababu iliangualia kazi za maandishi. Vilevile, utafiti unaofanywa unaangalia mshikamano ambao haukugusiwa katika kazi hii.

Mtafiti mwingine aliyeshughulikia mada hii ni Habwe (1989). Habwe (1989) alitafiti vipengele vya isimu-amilifu katika usemi wa Kiswahili. Utafiti wake ulichunguza baadhi

ya mikakati ya kupitisha maana baina ya wazungumzaji wa Kimvita katika mazungumzo ya kawaida. Maana iliyoangaliwa ni ile iliyokusudiwa na aina ya usemi ilitegemea muktadha wa mahali. Kazi hii pia ilijaribu kuelewa njia za unakidi. Kazi hii ina umuhimu kwa utafiti huu hasa kwa sababu iliangalia vipengele vya isimu-amilifu ambavyo pia vimegusiwa na uchunguzi unaofanywa. Hata hivyo, utafiti uliofanywa na Habwe (1989) ni tofauti kwa sababu uliangalia mazungumzo hasa kwa kuangalia ni vipi wanaozungumza hufasili ujumbe.

Utafiti mwingine ambao unahusiana na uchunguzi huu ni wa Habwe (1999). Katika utafiti huu mtafiti alichanganua usemi katika hotuba za kisiasa. Mtafiti huyu aliangalia hotuba za kisiasa akitumia mkusanyiko wa nadharia au mitazamo mitatu; mtazamo wa mshikamano, mtazamo wa maana iliyokusudiwa na mtazamo wa muundo kimada. Utafiti uliofanywa ulifaidika kutokana na utafiti huu lakini ulikuwa ni tofauti kwa kuwa ulikuwa ukishughulikia sajili tofauti.

Katika uwanja wa dini, kuna yaliyoandikwa kuhusiana na mada hii. Crystal (1965) alieleza katika utafiti wake kuwa lugha ikiwa ndicho chombo cha mawasiliano ambacho kimefungamanishwa na mahitaji mengi ya jamii, huwa na sehemu kubwa katika jukumu la kanisa la kuwasilisha dini na kuonyesha washiriki jinsi ya kuwasiliana na Mungu. Mtafiti huyu alinuia kuonyesha jinsi lugha inavyokuwa sehemu kubwa ya dini tangu mwanzo.

Watafiti wengine walioangalia sajili hii ya dini hasa kuhusiana na lugha ni Crystal na Davy (1969). Watafiti hawa waliangalia mtindo katika lugha ya dini hasa ya litajia. Waliangalia mitindo ya aina mbalimbali ya lugha ya Kiingereza. Katika maandishi yao wanasema kuwa mtu anapochagua lugha ambayo itatumika katika muktadha wa kidini, achague lugha ambayo si ya kiwango cha juu na fiche (lugha ambayo haiieleweki). Lugha isiyofuata kanuni za kisarufi na ambayo haina urasmi pia si nzuri. Wanasema kuwa sajili wanayoiita Kiingereza cha kidini ni tofauti sana na aina zingine za lugha. Wanasema kuwa hii ni sajili ya kipekee hasa kwa sababu ya kutumia lugha chakavu na uwezo wa kutumia miundo ya lugha ambayo ni ya kipekee.

Tafiti hizi mbili vilevile zina umuhimu katika utafiti unaofanywa lakini ni tofauti kwa sababu utafiti huu unaangalia matumizi halisi ya lugha katika sajili hii ya dini hasa kwa kuangalia sifa bainifu na mshikamano kama nyenzo kuu katika lugha hii.

Smith (1993) vilevile alitafiti lugha katika sajili ya dini. Smith (1993) alishughulikia kilichowasilishwa na wahubiri wanawake na wanaume, waliokuwa Seminari. Mtafiti huyu aliangalia ni vipi wanawake na wanaume huwasilisha aina fulani za matini. Utafiti wake uligundua kuwa kipengele cha uana hujitokeza katika mahubiri kama ilivyo katika aina zingine za mahusiano. Utafiti huu una umuhimu katika utafiti unaofanywa kwa sababu unahusu mahubiri na jinsi ya kujieleza. Hata hivyo, tofauti ni kwamba Smith (1993) aliangalia vile aina fulani maalum ya matini ilivyowasilishwa na wahubiri hasa kwa kuzingatia kigezo cha uana. Utafiti unaofanywa unaangalia matumizi ya lugha katika matini mbalimbali za Kiswahili.

Njue (1989) alifanya utafiti uliohusu ruwaza za mshikamano wa watambaji ngano katika lahaja ya Kimvita. Njue (1989) alinuia kutafiti aina za mshikamano ambazo hutawala utanzu huu na vile zinavyosaidia katika kutimiza lengo la utambaji ngano. Alitambua kuwa urejeshi hasa unaokuja baada ya kulitamka neno lenyewe ulikuwa muhimu katika utambaji ngano. Hii ni kwa sababu uliunganisha kisa chenyewe pamoja na kukipatia mwelekeo kisemantiki. Kazi hii ni muhimu kwa utafiti unaofanywa kwa sababu mtazamo wa mshikamano umetumika. Hata hivyo, utafiti huu uliangalia ngano na utafiti ambao umefanywa umeangalia sajili ya dini.

Kutokana na mapitio hayo ya kazi mbalimbali zilizofanywa kuhusu mada iliyofanyiwa utafiti, kuna ushahidi kuwa kuna pengo ambalo linaweza kujazwa na utafiti huu. Hii ni kwa sababu sajili hii ya dini haijashughulikiwa katika lugha ya Kiswahili. Kadhalika, sifa zake bainifu katika Kiswahili hazijatafitiwa na kubainishwa. Vilevile, mshikamano haujashughulikiwa kama nyenzo kuu katika lugha hii.

### **1.8 Mbinu Za Utafiti.**

Utafiti huu ulihusisha njia mbili za utafiti. Utafiti wa maktabani na ule wa nyanjani. Kwanza kabisa, yale yanoyohusu sajili hii yalisomwa kwa mapana kutoka maktabani. Bali na haya, mtafiti alisoma kwa mapana kuhusu uchanganuzi wa usemi. Mambo haya mawili yalimsaidia mtafiti kuelewa mambo ya kinadharia yaliyohitajika katika utafiti huu. Huu ndio uliokuwa utafiti wa kimsingi sana uliotakikana katika uchunguzi huu.

### **1.8.1 Ukusanyaji Wa Data.**

Ingawa kuna mambo mengi yanayofanywa kanisani na yote yanatumia lugha, mtafiti alikusanya data ya mahubiri peke yake. Mahubiri manne yalirekodiwa ambayo ndiyo yalikuwa sampuli ya utafiti. Mahubiri haya yalichukuliwa baada ya kutembelea kila kanisa mara moja. Sampuli hizi zilitumainiwa kuwa wakilishi (angalia sehemu 1.5). Vilevile, ukubwa wa sampuli ulitegemea mtazamo wa kimaelezo ambao ulitekelezwa. Pia, kulikuwa na uchanganuzi wa vipengele vidogo vinavyoleta mshikamano.

Katika kukusanya data hii mtafiti alitumia kinasa sauti kwa ajili ya kurekodi. Mtafiti alitembelea makanisa manne mara moja moja kila kanisa na kurekodi mahubiri. Mahubiri haya yalichunguzwa baadaye ili kupata sifa bainifu na aina za mshikamano. Vilevile, mambo muhimu yaliyofanywa na wahubiri ambayo yangesaidia katika kufasiri data na hayangeweza kurekodiwa yaliandikwa.

### **1.8.2 Mbinu Za Uchanganuzi Wa Data.**

Baada ya kukusanya data na kuihifadhi katika kanda za sauti, mtafiti alizisikiliza kanda hizo na kunakili yaliyomo katika karatasi. Baada ya kufanya hivi, mtafiti alianza kutafsiri data hii ili kutafuta sifa bainifu na aina za mshikamano. Hivyo, kila data katika kila sampuli ilichunguzwa. Katika uchunguzi huu, mtafiti aliangalia sifa za kimtindo zilizojitokeza na zinazoweza kuitambulisha sajili hii. Haya yalitekelezeka kupitia mtazamo wa kimtindo ambao huzingatia matumizi ya msamiati, matumizi ya mifano, msisitizo, kuchanganya msimbo na kadhalika.

Katika uchanganuzi wa data, mtafiti vilevile aliangalia aina za mshikamano ambazo zilijitokeza katika kila aina ya mahubiri. Haya yalifanywa kupitia mtazamo wa mshikamano ambao uliangalia aina za mshikamano kama vile urejeshi, ubadilishaji, udondoshi, uunganishi na mshikamano wa kimsamiati.

Baada ya uchanganuzi huu, katika uandishi wa ripoti au matokeo, mtafiti aliorodhesha sifa bainifu ambazo zilitambulikana kutokana na ruwaza mbalimbali zilizotanda katika kila sampuli ya mahubiri. Katika kila ruwaza ambayo ilijitokeza, maelezo ya kiisimu kuihusu yalitolewa. Aina za mshikamano na jinsi zinavyounganisha vipande kadhaa vya usemi pia zilielezwa katika uandishi wa ripoti.

### **1.9 Kuhusu Data Ya Uchanganuzi**

Sampuli ya tasnifu hii ni matini nne. Katika matini A na B, masomo matatu yalisomwa na mhubiri alisoma lile la mwisho kabla ya kuanza kuhubiri. Katika matini C na D masomo mawili yalisomwa. Mhubiri alisoma somo la pili kabla ya kuanza kuhubiri. (Matini A, B, C na D zinapatikana katika kiambatisho cha I).

Lugha ya mazungumzo huwa haina alama za uakifishi. Sifa kama vile kutua, kuongeza na kupunguza sauti husaidia wasikilizaji kuelewa kuwa sentensi moja imeisha na nyingine kuanzishwa. Kwa vile matini tunazozichambua zimerekodiwa kutokana na masimulizi, ni muhimu kutaja kuwa viakifishi vyote ni vyetu. Isipokuwa viakifishi, mambo yote ni kama yalivyorekodiwa. Hivyo, mifano yote inayotolewa kutokana na data imenukuliwa jinsi wahubiri wenyewe walivyoitamka. Hakuna usahihisaji wowote uliofanyiwa data hiyo.

## SURA YA PILI

### 2.0 RUWAZA ZINAZOJITOKEZA KATIKA LUGHA MAHUBIRI

#### 2.1 Utangulizi

Katika sura hii tutaangalia ruwaza ambazo zinajitokeza katika lugha ya mahubiri kupitia data iliyokusanywa. Ruwaza hizo zinadhihirisha sifa kadhaa bainifu katika lugha ya mahubiri. Katika uchanganuzi wa ruwaza hizo mtazamo wa kimtindo utatumika. Kama ulivyoelezwa na Crystal & Davy (1969) :

Lengo la elimu mtindo ni kuchanganua tabia za lugha, lengo kuu likiwa ni kutambua sifa ambazo zinatokea katika muktadha fulani wa kijamii kutokana na sifa za kijumla za kiisimu. Aidha, kuelezea ikiwezekana kwa nini sifa hizo zimetumika bali na zingine ambazo zingetumika. Vilevile kuziweka sifa hizo katika viterigo mahsusi kupitia misingi ya majukumu katika muktadha wa kijamii.(TY)

Hivyo, sura hii inalenga kuangalia ruwaza ambazo baadaye zitatuonyesha mtindo unaotumika katika lugha ya mahubiri. Ruwaza hizo hudhihirisha mtindo ambao hujengwa na vipashio vya kimsingi vinavyotumiwa na watu wanapowasiliana. Kulingana na Tannen (1984), kila kitu kinaposemwa lazima kisemwe kwa njia fulani na njia hii ndiyo hutokea kama mtindo.

Katika uchanganuzi wa ruwaza hizi, tunachunguza data ya kila matini. Tumechunguza jinsi mahubiri yanavyoanza, ni mambo gani yanayojitokeza katika mwili wa mahubiri na pia mahubiri anahitimisha mahubiri yake vipi. Mwanzo tunatambua ruwaza inayojitokeza,

mifano katika data inatolewa na baada ya mifano kuna maelezo ya kiisimu kuhusu ruwaza ile.

## 2.2 Mwanzo Wa Mahubiri

Data zilizorekodiwa zilionyesha kuwa hata ingawa mhubiri alisoma lile somo la mwisho kabla ya kuanza kuhubiri, hakuingia moja kwa moja katika mahubiri yake. Kila data inaonyesha kuwa alitumia njia fulani ya kuanza mahubiri. Ingawa kila mhubiri alitumia maneno na mtindo wake, ruwaza maalum inajitokeza. Data zote zinaonyesha kuwa wahubiri walianza kwa kuwaamkua waumini. Data ya matini A, ina mwanzo ufuatao:

*Mhubiri: Habari zenu*

*Waumini: Mzuri*

*Mhubiri: Bwana asifiwe*

*Waumini: Amen*

*Mhubiri: Bwana ni mwema asubuhi njema, kwa kunipatia nafasi*

*ili tusemezane pamoja. Ebu mwangalie mwenzako, aliye*

*karibu nawe, mwambie Mungu anakupenda na mimi ndugu*

*yangu.*

*Waumini: Mungu anakupenda na mimi ndugu yangu*

*Mhubiri: Bwana asifiwe sana*

*Waumini: Amen*

*Mhubiri: Kile kinanifanya...*

Tulipochunguza matini B, tunapata ruwaza hii lakini kwa maneno tofauti:

*Mhubiri: Uje roho mtakatifu*

*Waumini: Uje kwa njia ya Maria*

*Mhubiri: Mungu ni mwema*

*Waumini: Kila wakati*

*Mhubiri: Kila wakati*

*Waumini: Mungu ni mwema*

*Mhubiri: Ni siku ya kwanza...*

Data ya matini C pia inathibitisha kuhusu ruwaza hii ya mwanzo wa mahubiri:

*Mhubiri: Mnasemaje watu wa Mungu?*

**Waumini:** Amen

*Mhubiri: Mnasemaje?*

*Waumini: Amen.*

*Mhubiri: Yah-bila neema ya Mungu, hata mimi nisingesimama hapa.*

*Kwa hivyo waimbaji, waimbaji Mungu awabariki, waimbaji*

*Mungu awabariki sana.*

*Waumini: Amen*

*Mhubiri: Oh ahsante sana. Ah... ninapenda niseme...*

Tukiangalia data ya matini D, ruwaza hii ya kuanza mahubiri inajitokeza:

*Mhubiri: Bwana asifiwe*

*Waumini: Amen*

*Mhubiri: Halleluya*

*Waumini: Amen.*

Tukiangalia mianzo hii tunapata kuwa wahubiri hawakuingilia moja kwa moja somo walilotaka kufunza au kuwasilisha. Hata ingawa wahubiri waliwaamkua waumini kwa njia tofauti, tunawaona wakiwaamkua mara ya kwanza na wakisisitiza salamu zile kwa mara ya pili au hata ya tatu kama ilivyo katika matini B. Hii inaonyesha salamu hizi si za kutaka kuwajulia hali waumini. Ruwaza hii inaonyesha kuwa wahubiri walitaka kuleta waumini wao karibu nao ili wawe makini na kupata yatakayosemwa. Mianzo hii inaonyesha kuwa wahubiri wanataka kunasa hisi za waumini ili washiriki katika mahubiri na wajisikie wako pamoja na mhubiri. Walitaka kujenga uhusiano wa ushirika. Haya yanaoana na maoni ya Devito (1987: 133-139) kuwa majukumu makuu ya utangulizi huwa ni:

- i) kuwafanya watu wawe makini;
- ii) kujenga uhusiano kati ya mzungumzaji, hadhira na mada;
- iii) kuelekeza hadhira kuhusu kile kinachofuata.

Maamkuzi au mianzo hii inalenga kutimiza jukumu la kwanza na la pili kuhusu kujenga uhusiano. Aidha, maamkuzi haya ni kauli za heshima ambazo hutumika kiistiara ili kuonyesha kuwa watu wanashiriki jambo moja au huwa na mahitaji yanayolingana. Kwa mfano tukiangalia matini C mhubiri anapouliza, *Mnasemaje watu wa Mungu?*, waumini wote wanajibu *Amen*. Hili ni jambo linaloonyesha kuwa watu hawa wanashiriki jambo moja ndiposa wakajibu kwa namna moja. Kwa upande wa mhubiri hakuwa anatarajia

jawabu lingine na maamkuzi yake yanaonyesha kuwa anataka yeye na waumini wake wawe na mwanzo mmoja. Chambilecho Brown na Levinson (1978:108);

Mikakati ya kuwa na heshima ni mingi. Kuna mikakati inayohusisha mzungumzaji kudai kuwa wana msingi mmoja na hadhira. Haya yanafanyika kupitia kuonyesha kuwa wote wawili huwa katika kundi la watu ambao hushiriki mahitaji maalum pakiwepo malengo na maadili.(TY).

Kwa hivyo maamkuzi haya pamoja na kule kusesitizwa kwake yanaonyesha kuwa wahubiri wanadai msingi mmoja na waumini.

Tunaweza kusema pia kuwa kwa kutumia mianzo hii wahubiri wanataka kupunguza ule urasmi ambao unahitajika katika lugha ya mahubiri. Anapozungumzia diaglosia, Ferguson (1972:236) anaweka lugha ya mahubiri katika msimbo wa hadhi ya juu. Hii ina maana kuwa lugha inayohitajika kutumika katika mahubiri ni lugha rasmi. Kiai (1996) anatuelezea kuwa tunaweza kuchezea aina ya lugha ambayo kwa kiwango kikubwa hutumika katika hali rasmi. Katika kufanya hivyo huwa tunajaribu kupunguza ule urasmi ili kufikia hadhira. Anaendelea kudai kuwa kupunguza urasmi huhitaji mbinu fulani kuingizwa katika kujenga ule ujumbe. Matumizi ya salamu ni mbinu moja iliyotumiwa na wahubiri kupunguza urasmi katika lugha ya mahubiri. Jambo hili linaoana na maoni ya Tannen (1986) kuwa mbinu zote za kushirikisha hadhira ni njia za mzungumzaji za kuunda anachotaka kuongea au kuandika.

Kupitia yale yaliyojadiliwa tumepata kuwa maamkuzi haya yalikuwa na majukumu matatu muhimu. Kwanza, mhubiri alitaka kudai au kuonyesha kuwa yeye na waumini wako na msingi mmoja. Hii ndiyo sababu wahubiri wana majibu wanayoyatarajia kutoka kwa waumini. Waumini nao wanajua wanatarajiwa kujibu vipi. Pili, maamkuzi haya yalikuwa na nia ya kuwafanya waumini wawe makini na vilevile kujenga uhusiano kati ya mhubiri na waumini. Jambo hili lilikuwa na dhamira ya kuwaleta waumini karibu na mhubiri. Tatu, mianzo hii ilidhamiria kupunguza urasmi unaohitajika katika lugha ya mahubiri tukichukulia kuwa lugha hii huwa katika msimbo wa hadhi ya juu katika diaglosia. Hivyo, waumini wanaweza kupokea mahubiri kwa urahisi kwa kuwa hawatahisi kama ni jambo ambalo si la kawaida.

### **2.3 Utangulizi Wa Somo**

Kupitia data iliyokusanywa tunapata kuwa ruwaza nyingine inayojitokeza ni kule kutanguliza somo. Jambo hili linajitokeza katika kila data hata ingawa katika data zingine halijajitokeza moja kwa moja. Mhubiri anapomaliza kuwaamkua na kuwashirikisha waumini katika mahubiri yake anawaambia kiini cha mahubiri yake. Kwa mfano, katika data ya matini A mhubiri anasema:

*Mhubiri: Kile kinanifanya niseme kwamba nakupenda, neno langu asubuhi ya leo lahusu upendo. Na kabla niendeleo na mahubiri ningetaka kusema tuko pamoja na mke wangu...*

*Bwana asifiwe sana Waumini: Amen*

**Mhubiri:** *Basi hii ni...*

Ruwaza hii inajitokeza katika data ya matini B hata ingawa si kwa njia ya moja kwa moja. Katika data hii, mhubiri anatoa kiini cha mahubiri yake katika msitari wa pili anaposema;

**Mhubiri:** *Ni mwaka mpya amezaliwa, amekuwa sasa ni wa kila mtu, huyu mwokozi aliyezaliwa majusi sio wa mayahudi kama vile walivyofikiria, lakini ni wa kila mtu. Somo letu la kwanza...*

Tukiangalia data ya matini C, ruwaza hii imejitokeza kwa mara nyingine tena. Mhubiri anasema;

**Mhubiri:** *ila naomba neema ya Kristo iweze kufanya kazi maishani mwako ili upate kunielewa. "Kisa cha somo letu la leo kinasema, "Aibu ya mdhambi kwa kupenda cheo, kutopenda kuaibika vibaya kulimfanya apoteshe watoto wake wokovu" Ni mimi au ni wewe?*

Katika matini hii, ujumbe huu umerudiwa mara kadha.

Ruwaza hii inajitokeza katika data ya matini D ambapo mhubiri pindi tu anapomaliza kuwaamkua waumini anawaambia kiini cha ujumbe wake:

**Mhubiri:** *Somo letu asubuhi ya leo linahusu baraka.*

Tukiangalia data ya matini A, kiini cha ujumbe wa mhubiri ni “upendo”na mhubiri anaanza kuwajulisha waumini kuhusu dhamira hii. Mhubiri katika matini B anasisitiza kwamba mwokozi ni wa kila mtu na si wa mayahudi pekee. Bali na kutaka kutoa dhamira yake, mhubiri huyu anataja mayahudi kwa sababu kifungu cha Biblia kilichokuwa kimesomwa kilihusu kuja kwa mwokozi ambaye atatoka katika ukoo wa kiyahudi. Hivyo, mhubiri katika kutaja wayahudi alikuwa na nia ya kuwatahadharisha waumini kuwa mwokozi anayeoongea juu yake si wa Mayahudi lakini ni wa kila mtu hata ingawa yeye alikuwa Myahudi. Data ya matini C inaonyesha ujumbe kuhusu kupoteza wokovu kwa kupenda cheo na data ya matini D ina dhamira ya baraka.

Tukiangalia data hii tunapata kuwa wahubiri walitaja dhamira yao pindi tu walipomaliza kuwaamkua waumini kabla ya kufafanua. Kupitia majukumu ya utangulizi kama yalivyoelezwa na Devito (1987), utangulizi huu ulilenga kujenga uhusiano kati ya mzungumzaji, hadhira na mada. Vilevile, ulilenga kuelekeza hadhira kuhusu kile kinachofuata. Hii ina maana wahubiri waliweka mipaka kuhusu jambo ambalo walitaka kuzungumzia. Kwa hivyo waumini wanaweza kuwa wakitafakari kuhusu lile wanaloambiwa mhubiri anapoendelea kuwahubiria.

## **2.4 Matumizi Ya Maswali**

Matumizi ya maswali yamejitokeza katika data ya kila matini Maswali huwa na majukumu muhimu sana katika mawasiliano. Uulizaji maswali huunganisha watu wawili wanaozungumza. Goody (1978) anatueleza kuwa katika kazi ya majaribio iliyofanywa katika saikolojia ya jamii, maswali yalichukuliwa kama mbinu inayoathiri uwezo wa

kupanga na kuwasilisha ujumbe. Kwa hivyo maswali ni matendo ya usemi ambayo huweka watu wawili katika uhusiano wa moja kwa moja. Matumizi ya maswali ni ruwaza nyingine ambayo ilijitokeza katika lugha ya mahubiri. Wahubiri walitumia aina mbalimbali za maswali ambayo yalikuwa na majukumu tofauti. Lugha ya mahubiri ilidhihirisha aina kadha za maswali:

#### 2.4.1 Maswali ya Balagha

Istilahi “maswali ya balagha” imepata fasiri kutoka wataalamu mbalimbali. (Kwa mfano, Leech 1969, Richards na wengine 1985). Hata hivyo, takribani wote wanaafikiana kuwa maswali ya balagha huwa ni kauli ambazo zina nguvu zikiwa katika muundo wa maswali ambazo hazihitaji majibu. Maswali ya balagha yamejitokeza katika kila data iliyokusanywa. Kwa mfano mhubiri katika matini B anasema;

1. *Hata wakati wa nabii Isaiah, walikuwa hivyo tu, sisi tu ni sisi tu, mfalme ni wetu wale wengine si wao. Are we not doing the same thing today? Maybe Wakikuyu wanataka next time, the president lazima awe Mkikuyu...*

Mhubiri aliuliza swali hili “Are we not doing the same thing today?” (sisi hatufanyi hivyo leo?) alipokuwa anaongea kuhusu jinsi mfalme alivyo wa kila mtu na kuwa alipozaliwa Mayahudi walisema ni wao kwa sababu alizaliwa kwao. Walikuwa wanataka huyu mwokozi awe wao na si wa kila mtu. Ni katika muktadha huu anapouliza swali hili. Mhubiri anarejelea muktadha wa kisiasa nchini Kenya ambapo kila kabila linataka rais

atoke kwao. Mhubiri hakuwa anatarajia jawabu kutoka kwa waumini kwa sababu wanaelewa hii ndiyo hali ilivyo nchini Kenya. Katika matini B, mhubiri anauliza swali lingine la balagha anaposema;

2. *Endapo unafanya mazuri... lazima utaumia, lazima utalia siku moja, ulipe. Si hata Yesu alifanya hivyo? Alikuwa...*

Jibu la swali hili ni wazi. Mhubiri na waumini wanajua jibu lake. Awali, mhubiri alikuwa ameelezea jinsi wale watu wanaofanya mambo mazuri wanavyolipa kwa kuteswa. Hivyo katika muktadha ambapo swali hili liliulizwa, jibu lake lilikuwa wazi kwa sababu lilikuwa limeelezwa. Na kama Habwe (1999) anavyosema, swali la balagha linaonekana kwa muundo wa juu kama lina pengo la ujumbe. Hivyo linahitaji jibu. Hata hivyo, ujumbe huo huwa katika muundo wa ndani. Ujumbe huu unaweza kupatikana ikiwa kanuni ya ushirikiano itaeleweka na kanuni za kutafsiri katika muktadha wa hali. Kwa mfano, tukichukua swali la mfano (2) hapo juu, tunapata kuwa kwa muundo wa juu, linaonekana kuwa linahitaji jibu. Hata hiyo, jibu lake lilikuwa limetolewa awali na mhubiri alipokuwa amesema kuwa wanaofanya mazuri watalipa. Hivyo, waumini wanaelewa jibu lake kutokana na muktadha uliotangulia.

Katika matini C, mhubiri anatumia swali la balagha anaposema;

3. *mtu yeyote akitaka kunifuata lazima amchukie baba yake, na mama yake, na mke wake, ... ni wangapi wanawachukia wake zao, yule unalala naye kwa kitanda? Wangapi wanawachukia watoto? Wangapi? Eh... wangapi wanawachukia ndugu zao?*

Mhubiri aliuliza maswali haya yote ya balagha akiyafufuliza baada ya kusoma kifungu kutoka kwa Biblia. Maswali haya yametumiwa na mhubiri akitaka waumini wajue kuwa hakuna mtu ambaye anawachukia wale anaowapenda. Waumini walipoulizwa maswali haya walikaa kimya jambo lililonyesha maana iliyokusudiwa kuwa 'hakuna yeyote aliyemchukia mke wake, watoto,...'. Hivyo, kwa kutumia maswali haya mhubiri alitaka kutawala au kuchezea hisi za waumini na kutaka watafakari zaidi juu ya kifungu ambacho kilikuwa kimesomwa. Haya yanaoana na maoni ya Leech na Short (1981:282) ingawa walikuwa wanarejelea tukio katika riwaya wanaposema kuwa swali ni sihi ya moja kwa moja ya msomaji. Mhubiri anapofanya sihi kama hii kwa waumini anawaleta karibu naye na kuwashirikisha katika kufikiri. Tunaweza kusema kuwa maswali haya ya balagha yametumiwa kama kifaa cha kiisimu cha kupasha maana. Chambilecho Tannen (1984:20);

Iwapo mzungumzaji katika mahusiano anatumia kifaa ambacho anayekisikiliza huelewa kama ilivyodhamiriwa, hali ya kujitambulisha kipragmatiki hujitokeza.(TY)

(kwa maswali mengine ya balagha angalia kiambatisho II 9,10,27.)

Kwa hivyo basi, maswali ya balagha yalitumika mahali ambapo mhubiri alikuwa anajua kuwa hali anayozungumzia ilikuwa inaeleweka vizuri na waumini. (tazama mfano (1) hapo juu.) Maswali haya ya balagha vilevile yalitumiwa kama sihi ya mhubiri kwa waumini kuwa washiriki katika kufikiria.(Tazama mfano (3) hapo juu). Aidha, maswali haya yalitumika pahali ambapo waumini walikuwa wameelezewa jambo hilo na kwa hivyo mhubiri pamoja na waumini walikuwa wanajua jawabu la swali

lililoulizwa.(Tazama mfano (2) hapo juu.) Maswali haya yalikuwa muhimu katika juhudi za kupitisha ujumbe.

#### 2.4.2 Maswali Ya Kuwatahadharisha Waumini Wawe Makini

Kuna maswali yanayotumiwa kama njia ya kuwaamsha waumini au kuwafanya wawe makini zaidi. Maswali haya yanajitokeza katikati ya ufafanuzi wa jambo fulani. Hii ina maana kuwa mhubiri huwa anafafanua jambo fulani na katika maelezo yake anaingiza lile swali na kisha anaendelea tena na ufafanuzi. Aina hii ya maswali ilipatikana katika data ya matini zote nne.

Data ya matini A ilikuwa na maswali sita ambayo yalifuata mtindo huu tulioelezea. Kwa mfano mhubiri anaposema;

1. *Na kabla niendeleo sana ku... kufafanua zaidi ya hayo, ningese... ngetaka kusema (kimya) upendo ndio nguzo ya familia yetu. Kwanzia mtoto kwenda mama, kufika mzee. Na kwa nini ninasema namna hiyo? Nikiangalia upande wangu wa kushoto pale naona watoto pale, nikiangalia...*
2. *Anaanza kuyumba, anaanza kusikia kweli ... he is not stable in his working place. Kwa sababu gani? Hajui litatokea nini aende retirement!*

Katika matini B, mhubiri anauliza swali hili,

3. *Kwa hivyo wakristu wenzangu, somo letu la kwanza linataka kutuambia nini Wayahudi wa kisasa? Ya kwamba ...*

Mhubiri katika matini C ametumia aina hii ya maswali na tunatoa mfano ufuatao;

4. *...kumbe kijana amefanya vituko. Ameiba pesa na akaua mtu. Kwa kukosa nini? Malezi kwa sababu...*

Katika matini D, tuna mfano ufuatao;

5. *Bwana akasema katika kitabu cha mwanzo, ishirini na mbili na kumi na nane, "I will choose [...] all nations on earth shall be blessed because you are obeyed to me" Halleluya!*

*Waumini: Amen.*

*Huyo ni nani? Huyo ni Abrahamu...*

Maswali haya yanaonekana kama ni ya balagha. Hata hivyo, maswali haya yametumiwa kama ya kuwatahadharisha waumini wawe makini katika yale yanayosemwa. Hii ndiyo sababu tunaona kuwa mhubiri anapouliza swali lile, anaendelea kuwapa waumini jibu moja kwa moja. Tunaweza kusema pia kuwa kwa kutumia maswali haya, wahubiri walitaka kuwashirikisha waumini katika ujumbe kama njia mojawapo ya kuondoa uchovu. Ni kama Turk (1985:80) asemavyo;

Katika usemi ambao utachukua muda mrefu, lazima kuwe na njia ya kukatiza ule uzungumzi wa mtu mmoja ili kuongeza uelewano kati yake na hadhira.(TY)

(kwa maswali mengine ya aina hii angalia kiambatisho II 1,2,3,4,5,6.)

Ni dhahiri kwamba wahubiri kwa kutumia maswali haya walikuwa wanataka kuondoa uchovu wa waumini kuwa wamesikiliza kwa muda mrefu. Lengo la wahubiri lilikuwa kuwafanya waumini wamakinike katika kipindi chote cha mahubiri.

### 2.4.3 Maswali Ya Kujitathmini

Maswali mengine ambayo yamejitokeza yana nia ya kuwataka waumini wajitathmini kila mtu nafsi yake. Maswali haya yanapatikana katika matini B na C. Kwa mfano katika matini B mhubiri anasema;

1. *Kuna huyu ambaye amezaliwa, ebu tujiulize wakristu wenzangu, wewe nyota ambayo unaifuata kila wakati ambayo ni Kristu, unaifuataje?*

Katika matini C maswali sita ambayo yana nia ya kujitathmini yalitumika. Kwa mfano mhubiri anauliza;

2. *“Mara ngapi umemweka Yesu, kwenye mlango unakimbia kutenda dhambi na barua ndefu yenye maandiko?*

Data ya matini D inaonyesha aina hii ya maswali mhubiri anaposema;

3. *Unataka kuniambia utakuwa mwaminifu, utakuwa mtiifu katika nyumba ya Bwana. That's what you are saying?*

Maswali haya yametumiwa na wahubiri kwa kutaka waumini wajitathmini. Hii ni sehemu muhimu sana kwani ingawa wahubiri wanatoa somo kwa wote wanalenga mtu binafsi katika kujaribu kuleta yule mtu karibu na Mungu.

(Angalia pia kiambatisho II 11,17,19,20,22.)

#### **2.4.4 Maswali Mengine**

Maswali mengine yametumika katika mifano inayotolewa na mhubiri katika data ya matini C. Katika data hii mhubiri alitoa visa viwili kama kielelezo cha ujumbe wake. Katika kila kisa mhubiri alitumia swali moja akidhamiria kuwafanya waumini wafuate kisa kile. Maswali haya ni:

1. *Kisa cha somo letu la leo kinasema, "Aibu ya mdhambi kwa kupenda cheo, kutopenda kuabika vibaya kulimfanya awakoseshe watoto wake wokovu." Ni mimi au ni wewe?*
2. *"Huyu Shida alipata shida. Shida ni jina lake akapata nini? shida nyingine."*

Swali la kwanza lilitolewa kabla ya mhubiri kuwapa waumini kisa cha Emacullata ambaye hakupenda kuaibika na hivyo akamkosesha mwanawe wokovu. Swali la pili

liliulizwa kabla ya mhubiri kuwapa kisa cha Shida ambaye alipata shida ya kesi. (Taz. kiambatisho I matini C )

Maswali haya mawili yametumiwa ili kuvutia waumini wawe tayari kusikiliza visa ambavyo alikuwa anawatolea. Hali kadhalika, maswali haya mawili yanaonyesha ugumu uliopo katika kuyapa maswali mipaka yake. Hii ni kwa sababu maswali haya yanaingiliana sana na yale ya kutahadharisha waumini wawe makini lakini kama ilivyojadiliwa, yana majukumu tofauti.

## **2.5 Matumizi Ya Mifano Kuelezea Ujumbe**

Ruwaza nyingine ambayo inajitokeza katika lugha ya mahubiri ni matumizi ya mifano. Wahubiri wanatumia mifano dhahiri inayopatikana katika jamii ili kuelezea ujumbe wao. Katika matini A, mhubiri alidhamiria kupitisha ujumbe wa upendo na jinsi Mungu anavyowapenda watu ambao ni viumbe wake. Anatoa mfano wa wanafunzi waliomaliza darasa la nane na wamesikia ya kwamba kuna wengine ambao hawatapata nafasi katika kidato cha kwanza. Mhubiri huyu pia anatoa mfano wa akina mama kutokuwa na chakula na pia kina baba kuachishwa kazi. Hizi zote anazifananisha na shida ambazo Waisraeli walikuwa nazo walipoletewa mkombozi kwa sababu Mungu aliwapenda. Kwa kutoa mifano hii, mhubiri anataka kuonyesha kuwa Mungu kwa upendo wake atawamalizia zile shida.

Mhubiri katika matini B naye anatoa mifano ya kuelezea ujumbe wake kuwa Mungu ni wa kila mtu. Mhubiri huyu ametoa mifano ambayo inajitokeza kinyume na ujumbe huu akitaka kuwaonya watu. Kwa mfano, anatoa mfano wa jinsi mtoto wa Myahudi anavyopewa heshima kubwa na anakua akijua kuwa yeye ni mwenye urithi na Mungu ni

wake tu. Mfano mwingine anaoutoa ni wa jinsi kila kabila Kenya linataka rais atakayekuja atoke katika kabila lao. Mhubiri huyu anataka kuonyesha kuwa Mungu ni wa kila mtu na watu wakichukulia hivyo hawatakuwa na shida ya kupigania uongozi.

Data ya matini C pia inaonyesha matumizi ya mifano kama njia ya kuelezea ujumbe.

Mhubiri katika matini hii anatoa mifano kupitia visa viwili. Kisa kimoja ni cha msichana aliyetitwa Emacullata na jinsi alivyofanya ili kukosesha mwanawe uokovu. Katika kisa hiki, mhubiri alionyesha jinsi Emacullata alivyomwacha mwanawe bila malezi baada ya kujifungua. Baadaye Emacullata alikutana na mwanawe akiwa mtu mzima lakini hakuweza kumwelezea kuwa yeye ndiye mamaye. Mtoto huyu alifanya mambo mabaya na kuhukumiwa kifo. Hivyo, Emacullata alimkosesha wokovu kwa kutompaa malezi bora na baadaye kushindwa kumwelezea mtoto kuwa yeye ndiye mamake. Mhubiri alitoa kisa hiki kuonyesha jinsi watu wanavyofanya dhambi na kushindwa kuungama. Kwa hivyo watakosa wokovu. Kisa cha pili ni cha mtu aliyetitwa Shida ambaye alitaka kutetewa mahakamani. Katika kisa hiki, mhubiri alionyesha jinsi Shida alikuwa na rafiki watatu aliowapenda kwa njia tofauti. Alipopata kesi, marafiki aliowapenda mno hawakuweza kumtetea. Lakini rafiki aliyependwa kidogo ndiye aliyemtetea. Mhubiri alitoa kisa hiki akitaka kufananisha rafiki aliyependwa mno na shughuli na pesa, na pia jamii ya mtu. Alifananisha rafiki aliyependwa kidogo na Yesu Kristo. Katika kutoa kisa hiki, mhubiri alitaka kuonyesha waumini jinsi wanavyoshughulikia mambo mengi ya dunia kuliko Kristu ambaye anaweza kuwasaidia. Alitaka kuonyesha kuwa Kristu tu ndiye anayeweza kuwasaidia. Hivyo, mhubiri alitumia visa hivi viwili kusisitiza ujumbe wake.

Data ya matini D pia inaonyesha mfano wa jinsi mwafrika anapenda kuomba sana na jambo hili linamkosesha baraka. Ujumbe wa mhubiri ulikuwa kuhusu baraka na anasema katika mfano wake lazima waafrika waache tabia ya kuombaomba ili wapate baraka zao. Anatoa mfano wa yeye mwenyewe jinsi alivyokutana na mzungu na akamfanyia kila kitu mpaka aliporudi kwao alikuwa na mshangao mkubwa sana. Hii na kwa sababu mzungu huyu alifikiri waafrika wanajua kuomba tu. Hivyo, kwa mfano huu, mhubiri anasisitiza kuwa ili watu wapate baraka, lazima wajisimamie wao wenyewe.

## 2.6 Takriri

Ruwaza nyingine iliyojitokeza katika lugha ya mahubiri ni takriri. Maneno au sehemu za sentensi zilikaririwa. Kwa mfano katika matini A mhubiri anasema;

1. *Mungu alikuwa na upendo. Ili akatoa mwanao haje hafe msalabani ili tupate wokovu, ili tupate kukombolewa, ili tuweze kuwa katika hali ya uzuri ...*

Mfano mwingine unapatikana katika matini A mhubiri anaposema;

2. *Lakini siku ya leo wewe mtoto unasikitika, wewe mtoto unauliza, unafungua shule kesho, mama atapata fedha ya kuninulia kitabu, atapata fedha ya kuninulia uniform.*

Katika matini B, ruwaza hii ya kukariri inapatikana pia:

3. *Na ni Mungu wa kila mtu. He is not a situational God. Ni Mungu wa kila mtu, ambaye anataka kuona mwanga.*
4. *Lakini hiyo kofia inashikishwa na inataka kuonyesha huyo mtoto si mtoto wa kawaida, ni mtoto wa uyahudi na mtoto ambaye ana urithi.*

Data ya matini C vilevile ina mifano mingi ya takriri. Kwa mfano mhubiri anasema;

5. *Wapenzi ebu tuangalie fungu letu. Nataka tulisome fungu letu. Unajua watu hawajui fungu hili. Sitakwenda kwingine, au nataka kulisoma fungu hili.*
6. *Na kwa sababu hiyo afisa yuko ndani ya moyo wako, imeshindikana hata kumwabudu Mungu vilivyo. Na imeshindikana hata kumtolea Mungu zaka. Na imeshindikana hata kumwambia Mungu kama Mungu anavyotaka.*

Ruwaza hii pia inapatikana katika data ya matini D mhubiri anaposema;

7. *Baraka hizi ambazo tumesoma zimeandikwa, na kama Biblia yako imeandikwa hivyo na kama tumesema hizo baraka ni zako, na ukiangalia sijui ni wangapi wako na hizo baraka, ambazo tumezisoma hapa.*

Tukiangalia takriri ambayo imejitokeza tunaona unafanyika kwa minajili ya kuisisitiza ile hoja. Alter (1981), anapongea kuhusu msisitizo unaopatikana katika Biblia anasema;

Kukariri kwa maneno muhimu huwa na nia ya kuonyesha dhamira kupitia kujitokeza kwake katika sehemu mbalimbali. (TY)

Tukiangalia mfano (1) mhubiri anarudia kwa kutaka kuonyesha dhamira ya “upendo.” Katika matini B mfano (3) unaonyesha kuwa Mungu ni wa kila mtu na kupitia mfano (7), mhubiri katika data ya matini D alikuwa na dhamira ya “baraka” ambayo imejitokeza kupitia kukariri.

## 2.7 Matumizi Ya Ishara

Data iliyorekodiwa ya utafiti huu ilichukuliwa kwa mtafiti kuwa mshiriki. Hii ina maana kuwa mtafiti alitazama yale yaliyokuwa yakiendelea. Utafiti huu uligundua kuwa kulikuwa na matumizi ya ishara za mwili kama vile uso, mikono na hata kichwa. Matumizi haya ya ishara yalikuwa na majukumu ya kuwasiliana. Haya yanaoana na maoni ya Turk (1985:145) kuwa;

Tunapowasilisha jambo kwa kuongea, tunawasiliana sio tu kwa maneno lakini pia kwa matumizi ya ishara, ... na mambo yanayoonyesha hisia. (TY)

Ishara hizi zilikuwa na majukumu tofauti. Wahubiri walitumia ishara za mikono na kuzungusha kichwa mbele na nyuma walipokuwa wasisitiza jambo. Ishara za uso zilionyesha hisi za mhubiri kuhusu jambo alilokuwa anazungumzia. Kauli hii inashadidiwa na Faircough (1989: 27 ) asemapo;

Hata wakati ambapo matini huwa ni za mazungumzo, ... mazungumzo huoanishwa na ishara kama vile za mikono, za uso, kutoka mahali pamoja hadi pengine na jinsi ya kukaa. Kuoana huku huweko kwa kiasi kuwa

mazungumzo wakati mwingine hayaleweki bila kurejelea mambo haya.

(TY).

Kwa mfano katika matini A mhubiri anapoongea kuhusu unabii wa Isaiah kwa kusema; “Tazama mtumishi wangu nimemtengenezea , mteule wangu ambaye nafsi yangu inapendezwa naye.” Bwana asifiwe sana. Katika kutamka kauli hii mhubiri alikuwa anaonyesha furaha usoni huku akikunja na kukunjua uso kama anayeigiza.

## 2.8 Matumizi Ya Sauti

Matumizi ya sauti ni sifa nyingine ambayo inajitokeza kama ruwaza katika lugha ya mahubiri. Wahubiri walitumia sauti zao kwa njia mbalimbali ili ujumbe ueleweke. Kwa mfano kuna wakati wahubiri waliposema jambo na kukaa kimya kwa muda mfupi. Kwa mfano katika matini A mhubiri anasema;

1. *Ili akatoa mwanao haje hafe msalabani ili tupate wokovu, ili tupate kukombolewa, ili tuweze kuwa katika hali ya uzuri. Kwa sababu tuko na njia moja au nyingine katika taabu.(kimya) Vile wana wa Israeli walikuwa ...*

Katika matini B mhubiri anatumia ruwaza hii anaposema;

2. *Katika somo letu la Injili linatuakishia muru, linatuambia, wakristu ambao ukabila it is not in their mind, hata tunapokuja kupokea sio kwa ukabila, tunapokea Kristu tu, nothing else.(kimya) Tunaambiwa ...*

Data ya matini C inadhihirisha matumizi haya ya sauti mhubiri anaposema;

3. *Na kwa sababu huyu afisa yuko ndani mwa moyo wako,imeshindikana hata umwabudu Mungu vilivyo.Na imeshindikana hata kumtolea Mungu zaka ilivyo. Na meshindikana hata kumwimbia Mungu kama Mungu anavyotaka.(kimya)Wapenzi, ebu tuangalie ...*

Mhubiri katika data ya matini D vilevile alitumia ruwaza hii alipokuwa anaongea kuhusu baraka anaposema;

4. *Ukiangalia pengine hauna kitu,(kimya) naweza kuona katika hizo baraka ni zako.*

Wahubiri hawa walikaa kimya ili kuwapa waumini nafasi ya kutafakari ili waelewe maana. Maoni haya yanashahibiana na ya Turk (1985:135) anapodai kuwa:

Kukaa kimya ni njia yenye nguvu sana ya kuwasiliana. Kukaa kimya huku hufanya maana ya kilichosemwa kuzama na pia kutayarisha wasikilizaji kwa kile kinachofuata. (TY)

Bali na kukaa kimya kutumiwa kwa jukumu la kuwezesha maana kuzama , wakati mwingine wahubiri walikaa kimya wakitafuta jambo la kusema. Kwa mfano katika matini mhubiri anaposema;

1. *Na kabla niendelee sana na ku... kufafanua zaidi ya.hayo, ningese... nge-taka kusema (kimya) upendo ndio nguzo ya familia yetu.*

Au katika matini C Mhubiri anaposema;

2. *Nataka tulisome fungu letu. Unajua watu wengi hawajui fungu hili.*

*Sitakwenda kwingine, au nataka kulisoma hili fungu. Luka kumi na nne, tusome kwanza (kimya) Luka kumi na nne, ...*

Wahubiri vilevile walibadilisha sauti yao mara kwa mara. Hii ina maana kuwa walitumia kiimbo tofauti. Vilevile, kuna wakati ambapo wahubiri waliongeza sauti na wakati mwingine kuongea kwa sauti ya chini. Kwa mfano, waliongeza sauti walipokuwa wanasisitiza jambo na kushusha sauti mwishoni mwa sentensi. Haya yote yalifanyika kwa madhumuni ya kuwafanya waumini wawe makini.

## **2.9 Mwisho Wa Mahubiri**

Kabla ya wahubiri kukamilisha mahubiri yao walitumia njia tofauti kuonyesha kuwa wanahitimisha.

### **2.9.1 Kuashiria Mwisho Wa Mahubiri**

Hii ni ruwaza nyingine ambayo inajitokeza katika kila matini. Mhubiri anatumia maneno fulani ambayo yanaonyesha ya kuwa yuko karibu kumaliza kuhubiri. Katika matini A, tunaona mhubiri akisema,

*Kwa hivyo, ndugu umeketi hapa, dada hapo ulipo, kumbuka ya kwamba, huyu Mungu ako pamoja nawe. Na ukienenda siku ya leo, nenda ukisema Bwana asifiwe kwa sababu, leo tumepata upendo kutoka kwa Mungu.*

Hii ilikuwa ni ishara kuwa mhubiri anakamilisha mahubiri yake. Maneno “*kwa hivyo*” hutumiwa kuonyesha kuwa kuna mambo ambayo yamesemwa hapo awali na yanahitimishwa. Matumizi ya maneno haya pamoja na “*ukienenda*” yanaonyesha kuwa mhubiri anahitimisha mahubiri yake. Ruwaza hii pia inajitokeza katika matini B, mhubiri katika matini hii anasema;

*Tuombe mwenyezi Mungu atupe nguvu ya kuendelea tu hii nyota moja. Tunafuata huyu Kristu anayehubiriwa katika Injili. Namalizia kwa kuwaambia wale wano...wanao ambao...wakati huu wana shida ya school fees, hata uniform, hata kiatu ya mtoto. Tuwaombee ili Mwenyezi Mungu awaendelee kuwaonyesha nyota.*

Mhubiri katika matini hii anaonyesha kuashiria kufika mwisho wa mahubiri yake anapowatahadharisha waumini kuwa anamalizia. Vilevile anaposema “*Tunafuata huyu Kristu anayehubiriwa katika Injili*” anaonyesha kuwa amesema mambo kuhusu huyu Kristu na anatamatisha. Hii ni kwa sababu Injili ndilo somo la mwisho lilisomwa katika matini hii na mhubiri alianza kufafanua somo la kwanza na kumalizia na Injili.

Data ya matini C pia ilionyesha kuwa mhubiri aliashiria kuwa anamaliza ujumbe wake.

Mhubiri anasema;

*Labda nimwambie kitu kimoja. Labda nimalizie na huyu mtu. Nataka nifunge  
na huyu mtu. Kuna rafiki yangu...*

Ruwaza hii inajitokeza katika data ya matini D. Mhubiri anaashiria kuwa anamaliza anaposema;

*Nikimaliza ningetaka kuomba kuhusu baraka. Na kabla sijaomba, there is  
someone here ... Nakwambia yale nimeongea hayako njiani mwako.*

Kuashiria huku kuwa mhubiri anahitimisha ujumbe wake kwa kutumia maneno kama “*kwa hivyo*”, “*ukienenda*”, “*namalizia kwa kuwaambia*”, “*labda nimalize na huyu mtu*”, na “*nikimalizia ningetaka kuomba kuhusu baraka*” hakukupatikana kutokana kwa maneno tu. Mhubiri alipokuwa anasema maneno haya alibadilisha sauti yake na kuongea kwa sauti ya chini. Huku kubadilisha sauti pamoja na maneno yale kulidhamiriwa kuwasilisha kuwa anamaliza yale aliyokuwa ameyapanga. Vilevile, kutokana na data iliyorekodiwa, wahubiri walipoashiria kuwa wanamaliza walikariri tena dhamira ya ujumbe wao. Ndio maana katika matini A mhubiri anasema, “*Na ukienenda siku ya leo, nenda ukisema Bwana asifiwe kwa sababu leo tumepata upendo kutoka kwa Mungu*” Dhamira ya matini A ilikuwa upendo. Katika matini B, mhubiri anasema, “*Tuombe ... kuendelea tu na hii nyota moja. ...huyu Kristu aliyehubiriwa ...*” Dhamira ya matini B

ilikuwa Kristu ni wa kila mtu. Mhubiri katika matini D vilevile alikariri dhamira yake alipoashiria kuwa anamaliza kuhubiri kwa kusema, “*Nikimaliza ningetaka kuomba kuhusu baraka*” Dhamira yake ilikuwa baraka. Katika matini C, mhubiri alionyesha kuwa anaashiria kumaliza kwa kutoa kisa: “*Labda nimalizie na huyu mtu. Nataka nifunge na huyu mtu.*” Hii pia ni njia moja ya kuondoa uchovu na kuwafanya waumini wawe makini mpaka mahubiri yaishe.

### **2.9.2 Kutamatisha Mahubiri**

Kupitia data iliyochukuliwa tunaona ya kuwa kulikuwa na ruwaza iliyojitokeza hasa wahubiri walipomaliza mahubiri yao. Katika matini A, mhubiri anasema;

*Na Bwana awabariki. Tuombe.*

Ruwaza hii inajitokeza katika matini B mhubiri anaposema;

*...wasikate matumaini kwa sababu ya waherode wa kisasa. Tusimame.*

Mwisho wa matini C unashahibiana na wa matini A. Mhubiri anasema;

*Mungu na awabariki. Tuombe.*

Matini D vilevile imejitokeza na ruwaza hii ya kuonyesha kuwa mhubiri amefika kikomo cha mahubiri yake. Katika matini hii tunaona mhubiri akisema;

*Funga macho tuombe.*

Hii ina maana kuwa anahitimisha mahubiri yake.

Miisho hii ya mahubiri inaonyesha kuwa mazungumzo yana mipaka na mipaka hii huonyeshwa kwa njia tofauti. Courthard (1985:90) anatumia kuwa;

Miisho ya mazungumzo lazima itimilike- wazungumzaji hawakatizi mazungumzo tu. Ni bayana kuwa mazungumzo huhitimishwa kwa kifungu fulani kama vile “tuonane”, “lala salama” na kadhalika.(TY)

Kauli hii ina maana kuwa kuna mambo yaliyokubalika kutumika kuonyesha kuwa mazungumzo yanahitimishwa au sehemu fulani ya jambo fulani imetimilika. Katika sajili ya dini, na hasa katika mahubiri, mhubiri baada ya kuhubiri anapowaambia waumini “*Bwana awabariki, na tuombe*” waumini wanajua moja kwa moja kuwa sehemu hiyo ya ibada imetimilika. Labda wanaweza kuingia katika sehemu nyingine. Katika muktadha wa utafiti huu tuna miisho ambayo imejadiliwa hapo awali. Miisho hii inaonyesha mipaka ya mahubiri. Jambo hili la kuweka mipaka ni muhimu na lilijitokeza kwingine kama tilivyoona awali. Kwa mfano katika utangulizi wa somo mhubiri alipotaja dhamira yake alimaanisha kuwa hataongea mambo mengine isipokuwa yale aliyoyataja. Hivyo aliweka mipaka ya ujumbe wake.

### 2.9.3 Hitimisho

Sura hii imeangalia ruwaza ambazo zimejitokeza katika lugha ya mahubiri. Kupitia ruwaza hizi, tumeona kuwa ingawa mtindo unaweza kutofautiana kutoka mhubiri mmoja hadi mwingine, kuna mambo kadha ambayo yanashahibiana. Kwa jumla, tumeona kuwa mahubiri huanza kwa njia fulani ambazo zinadhamiria kuwaleta waumini karibu na

mhubiri. Ruwaza hizi ni pamoja na maamkuzi ambayo ingawa yanatumia maneno tofauti, yalikuwa na dhamira moja. Vilevile, katika mianzo wahubiri walitanguliza kwa kutaja dhamira ya mahubiri yao. Walipotaja dhamira zao, wahubiri walikuwa na nia ya kuweka mipaka ya ujumbe waliotarajia kupasha. Loveday (1983:177) anatumia kuwa mianzo ya mazungumzo si mbinu sisizo na maana. Anaendelea kutuelezea kuwa kwa jumla, mianzo huwa na athari katika mazungumzo yanayofuata. Hii ni kwa sababu jukumu lake ni kujenga uhusiano kati ya wanaohusika. Ni katika mfululizo wa mianzo hii ambao wanaoshiriki hutathimiana, na kuweza kujua ama watashirikiana na watafanya hivyo kwa nia zipi.

Kuna ruwaza nyingi zilizotumika kuendeleza ujumbe ili uwafikie waumini na waupate kwa hali ya juu. Hizi ni pamoja na matumizi ya maswali, matumizi ya mifano kuelezea ujumbe, takriri, matumizi ya ishara na matumizi ya sauti. Kati ya ruwaza hizi, kuna zile zilizokuwa na madhumuni ya kuwaondoa waumini uchovu kwa kuwafanya washiriki katika yale yaliyokuwa yakisemwa. Kwa mfano, baadhi ya maswali na matumizi ya sauti. Wahubiri waliashiria kuwa wanamaliza mahubiri yao kwa kutumia njia tofauti. Kila mhubiri aliyasema maneno fulani yaliyoonyesha kuwa anaashiria kumaliza mahubiri yake. Bali na haya, wahubiri walikariri kiini cha ujumbe wao au kutoa kisa fulani kama njia ya kutamatisha. Kulikuwa pia na njia za kutamatisha mahubiri. Tunaweza kulinganisha haya na maoni ya Stubbs (1983:23), anapoongea kuhusu upangaji wa masimulizi anaposema;

Kuna uwezekano wa kuonyesha kuwa mazungumzo ambayo yanachukuwa muda mrefu na ni marefu yana mpango wa kimuundo wa kijumla ... Hadithi huwa na mianzo, mwili na mwisho. ( TY)

Kauli hii ina maana kuwa kuna namna ya kuanza mazungumzo katika sajili ya dini kama tulivyoona katika sehemu ya 2.3 na 2.4. Mazungumzo vilevile huendelezwa kwa kutumia mbinu fulani kama katika sehemu 2.5, 2.6, 2.7 na 2.8. Vilevile, kuna njia za kuhitimisha mazungumzo kama katika sehemu 2.9.

## SURA YA TATU

### 3.0 KUCHANGANYA MSIMBO

#### 3.1 Utangulizi

Uchanganuzi katika sura ya pili ulibainisha baadhi ya ruwaza zilizojitokeza katika lugha ya mahubiri. Ruwaza hizi zilidhihirisha baadhi ya sifa bainifu katika lugha hii. Ruwaza hizi zilikuwa za kuanza, kuendeleza ujumbe na za kuhitimisha mahubiri. Ruwaza nyingine iliyojitokeza ni ya kuchanganya msimbo. Sura hii inachunguza ruwaza hii kama sifa moja bainifu katika lugha ya mahubiri.

Kuchanganya msimbo ni dhana iliyopatiwa fasiri ya kiisimu kuwa na maana ya kuchepeka maneno au sehemu ya neno la lugha moja katika usemi ambao uko katika lugha nyingine. (Richards na wengine 1985, Saville-Troike 1989). Wataalam kama Fasold (1984) na Milroy (1987) wamefanya ufafanuzi wa tofauti ya kuchanganya na kuhamisha msimbo. Hata hivyo, kwa minajili ya kuelezea sehemu hii tutatumia kwa kijumla sana dhana ya kuchanganya msimbo. Kama anavyoeleza Pfaff (1979). Pfaff (1979:293) anaeleza kuchanganya msimbo kuwa dhana inayojumuisha kubadilisha msimbo na ukopaji wa msamiati.

Kuchanganya msimbo ni tukio ambalo ni la kawaida (Habwe, 1999, Romaine, 1989). Misimbo ambayo inachanganywa mara nyingi ni Kiswahili na Kiingereza ingawa wakati mwingine watu huchanganya msimbo wakitumia lugha zao za kiasili.

Kulingana na Romaine (1989), kuna aina tatu za kuchanganya msimbo. Nazo ni:

- i) Uambatishaji wa kiungo. Kwa mfano,  
You! Natumaini hutaki kutupiga picha.
- ii) Uchopekaji wa maneno kati ya sentensi. Kwa mfano,  
Alienda mjini kutafuta kazi. And you know what- hakuwa na mtu wa kumsaidia.
- iii) Uchopekaji wa maneno miongoni mwa sentensi. Kwa mfano,  
Nataka umpigie dadako simu umwambie sitoweza kuenda kwake.  
Will you do that for me?

Kutokana na data iliyorekodiwa, kuchanganya msimbo kulijitokeza kama ruwaza mojawapo ya lugha ya mahubiri. Aina zote tatu za kuchanganya msimbo zilijitokeza katika data iliyochukuliwa ingawa kuna aina zingine zilizojitokeza kwa wingi. Sehemu hii inaonyesha aina hizi za kuchanganya msimbo na kufikia mwisho wa sura hii kuna jedwali ambalo linaonyesha kwa muhtasari matukio ya sentensi ambazo zinajitokeza katika kila aina ya kiisimu ya kuchanganya msimbo. Aidha, kuna maelezo kuhusu maana ya kiisimu ya aina hizi za kuchanganya msimbo.

### **3.2 Uambatishaji Wa Kiungo**

Dhana hii hujumuisha uchopekaji wa kiungo au mshangao wa lugha moja katika usemi mwingine ambao umo katika lugha nyingine. Kuchanganya msimbo huonyesha sifa ya sentensi ambayo ni ya lugha moja kuweza kuwa na ulumbi (Poplack, 1980). Aina hii haikujitokeza kwa wingi katika lugha ya mahubiri.

Katika data ya matini A, mhubiri alitumia aina hii ya kuchanganya msimbo mara moja. Mhubiri alipokuwa anaongea kuhusu vile akina baba walivyo na shida nyingi na wasivyo imara katika mahali pao pa kazi anasema;

1. *Kwa sababu gani? Hajui litatokea nini aende retirement!*

(Kwa sababu gani? Hajui litatokea nini astaafu)

Mhubiri katika sentensi hii alichopeka kiungo cha Kiingereza katika sentensi ya Kiswahili.

Data ya matini B haikuwa na aina hii ya kuchanganya msimbo lakini katika matini C kuna mfano ufuatao;

1. *Oh, Emacullata alipoona vile, akamwambia afisa, “Mimi hapendi mtu isipokuwa wallet!”*

(Oh, Emacullata alipoona vile, akamwambia afisa, “Mimi hapendi mtu isipokuwa pochi!”)

Data ya matini D haikuwa na aina hii ya kuchanganya msimbo (Angalia kiambatisho III nambari 11 na 13.)

Tukiangalia aina hii ya kuchanganya msimbo, tunaweza kudai kuwa wahubiri waliitumia mahala ambapo walikosa kupata moja kwa moja kisawe cha neno husika katika Kiswahili kama katika mfano (1). Pia, aina hii ya kuchanganya msimbo ilitumika ili kuonyesha mshangao hasa katika kusisitiza jambo. Tukiangalia mfano (2) hapo juu, Emacullata (mhusika) anaposema, "Mimi hapendi mtu isipokuwa wallet!" anataka kusisitiza 'wallet' kupitia mshangao.

### 3.3 Kuchanganya Msimbo Kati Ya Sentensi

Aina hii ya kuchanganya msimbo hurejelea aina mbalimbali za kuchanganya msimbo ambazo hutokea katika sentensi. Aina hii pia hujumuisha kuchanganya msimbo katikati mwa neno ikiwa na maana kuwa neno fulani katika lugha fulani huundwa likitumia sheria za kimofolojia za lugha nyingine. Aina hii ya kuchanganya msimbo ndiyo ilijitokeza kwa wingi katika data iliyorekodiwa. Mifano ya kuchanganya msimbo kutokana na data ni kama ifuatayo;

Katika matini A mhubiri anasema;

1. *Yeye anauliza, na inaweza kufika wakati mmoja jina langu liingie kwa computer ya Retrenchment?*

(Yeye anauliza, na inaweza kufika wakati mmoja jina langu liingie katika compyuta ya kupunguzwa kwa wafanyikazi.)

Katika kauli hii, mhubiri anachanganya Kiswahili na Kingereza hasa anapofanya maneno ya Kiingereza kuchukua muundo wa lugha ya Kiswahili katika upatanishi wa kisarufi.

Mhubiri anasema “Computer ya Retrenchment”. Katika Kiswahili, tungetarajia sentensi kama compyuta ya kupunguzwa kwa wafanyikazi. Licha ya kuchanganya msimbo, mhubiri anaonyesha namna ustaafishaji unavyoendelezwa kwa teknolojia ya kisasa inavyowakilishwa hapa na kompyuta.

Katika data ya matini B, mifano mingi imejitokeza ya aina hii ya kuchanganya msimbo. Tuna matukio ishirini na tano ambapo aina hii ya kuchanganya msimbo inajitokeza. Hata hivyo, mfano mmoja ndio utakaokuwa kielelezo:

2. *Wakristu ambao ukabila, it is not in their mind, hata tunapokuja kupokea, sio kwa ukabila, tunapokea Kristu tu, -nothing else.*

(Wakristu ambao ukabila hauko akilini mwao, hata tunapokuja kupokea, sio kwa ukabila tunapokea Kristu tu, -hakuna kitu kingine.)

Mhubiri katika data hii alichanganya Kiswahili na Kiingereza.

Data ya matini C pia inaonyesha aina hii ya kuchanganya msimbo. Katika matini C tulikuwa na matukio tisa ya aina hii ya kuchanganya msimbo. Mfano mmoja ni,

3. *Huyu anakuja direct ah... ikawa kama ni direct. Amefika pale sasa, ikaja case sasa.*

(Huyu anakuja moja kwa moja ah... ikawa kama ni moja kwa moja. Amefika pale sasa, ikaja kesi sasa).

Mhubiri katika sentensi hii alichanganya Kiswahili na Kiingereza. Maneno ya Kiingereza “direct” na “case” yamo ndani mwa sentensi ya Kiswahili.

Aina hii ya kuchanganya msimbo pia inapatikana katika matini D. Data ya matini D ilikuwa na matukio kumi na mawili ya aina hii. Kwa mfano:

4. *Biblia inasema, you will be a blessing. Ibrahimi alikuwa mtu wa kupeana na kwa sababu alikuwa mtu wa kubless watu ...*

(Biblia inasema, wewe utakuwa mtu wa kupeana baraka- Ibrahimi alikuwa mtu wa kupeana na kwa sababu alikuwa mtu wa kubariki watu ...)

Mfano mwingine wa aina hii unajitokeza katika matini B mhubiri anaposema;

5. *Tukifikiria Mungu aliyezaliwa ni wa wakatoliki tu, salvation is only for catholics tutakuwa tumemiss the vote.*

(Tukifikiria ya kwamba Mungu aliyezaliwa ni wa wakatoliki tu, ukombozi ni wa wakatoliki tu, tutakuwa tumepotea njia)

Katika sentensi hizi mbili, wahubiri wanachanganya Kiswahili na Kiingereza. Vilevile wanaunda vitenzi vya Kiingereza kwa kutumia sheria za lugha ya Kiswahili wanaposema “*kubless*” na “*tumemiss*” ambavyo ni “kubariki” na “tumepotea” katika lugha ya Kiswahili. Hii inaonyesha kuwa kuchanganya msimbo huku hakuvunji sheria za kisintaksia za lugha zote mbili. Haya yanaoana na maoni ya Poplack (1980:586) kuwa;

Kuna uwezekano wa kuchanganya msimbo katika usemi hasa mahali ambapo kuingiliana kwa lugha zote mbili hakuvunji sheria za kisintaksia za lugha yoyote.(TY)

(Mifano mingine ya aina hii ya kuchanganya msimbo inapatikana katika kiambatisho III 2,15,19,22,29,38,42,50,55,67,72,86,89)

Kutokana na mifano iliyotolewa, ni dhahiri kuwa aina hii ya kuchanganya msimbo ilitumika kiasi kwamba lugha zote mbili ziliingiliana sana katika sheria zake za kuunda sentensi. Tukiangalia mfano (1) ingawa maneno “computer ya retrenchment” ya Kiingereza yametumika, yamechukuwa muundo wa maneno ya Kiswahili katika upatanisho wa kisarufi. Haya pia yanapatikana katika mfano (4) na (5) ambapo vitenzi vya lugha ya Kiingereza vinaundwa kupitia sheria za Kiswahili. Mifano hii inathibitisha kauli ya Poplack (1980) kuhusu kuchanganya msimbo mahali ambapo kuingiliana kwa lugha zote mbili hakuvunji sheria za kisintaksia za lugha yoyote. Jambo hili pia linaonyesha kuwa wahubiri wana uwezo wa kutumia lugha zote mbili.

### **3.4 Kuchanganya Msimbo Miongoni Mwa Sentensi**

Aina hii hujumuisha kubadilisha sentensi kwa namna ambayo kila kishazi au kila sentensi huwa katika lugha moja. Hii ina maana kuwa sentensi moja hugawanywa mara mbili na lugha zinazohusika. Kila sehemu ya sentensi huundwa kwa kuzingatia sheria za utunzi wa sentensi wa lugha husika. Aina hii ya kuchanganya msimbo ilijitokeza kwa wingi katika data. Tutachukua mfano mmoja mmoja katika kila matini.

Matini A ilikuwa na mfano mmoja tu ambao ni,

1. *Anaanza kuyumba, anaanza kusikikia kweli...*

*He is not stable in his working place.*

(Anaanza kuyumba, anaanza kusikia kweli...sio imara katika mahala pake pa kazi).

Data ya matini B ilikuwa na mifano kumi na moja ingawa tutaonyesha mmoja tu.

2. *Tusiwe kama Mayahudi ambao walisema Mungu ni wetu, we cannot share our God.*

(Tusiwe kama mayahudi ambao walisema Mungu ni wetu hatuwezi kugawana Mungu wetu).

Tukiangalia matini C, tuna mifano miwili ambayo inaonyesha aina hii ya kuchanganya msimbo. Kwa mfano mhubiri anaposema;

3. *Siku moja kijana alimaliza course.*

(Siku moja kijana alimaliza kozi).

Mhubiri katika sentensi hii anatumia kishazi cha Kiswahili na kingine cha Kiingereza ingawa sentensi hii itaeleweka vizuri tukielewa kuwa kuna udondoshi.

Aina hii ya kuchanganya msimbo imetumika kwa wingi katika matini D. Matini D ilikuwa na matukio ishirini na nne ya kuchanganya msimbo kwa aina hii lakini tutatoa mfano mmoja.

4. *Lakini kitu kimoja tuliongea mwakani tulisema, You must be Committed to the house of God. And second, you must be faithful to the house of God.*

(Lakini kitu kimoja tuliongea mwakani tulisema, lazima uwe mtiifu kwa nyumba ya Bwana. Pili, lazima uwe mwaminifu kwa nyumba ya Bwana).

Katika sentensi hii mhubiri anatamka sehemu moja ya sentensi kwa lugha ya Kiswahili na nyingine kwa Kiingereza bila kuchanganya msimbo ndani mwa sentensi.

(Kwa mifano mingine angalia kiambatisho III, 11, 16, 31, 37, 52, 62, 65, 69, 70, 73, 79, 85, 87, 90, 91)

Ni bayana kuwa aina hii ya kuchanganya msimbo ilitumika kwa nia ya kusisitiza. Hata hivyo, matumizi yake yanatuelekeza kwenye uwezo wa lugha zote mbili. Wahubiri walitumia aina hii ya kuchanganya msimbo hasa mahali walipohisi kuwa dhana itaeleweka vizuri katika lugha ya Kiingereza.

### **3.5 .Ufafanuzi Kuhusu Kuchanganya Msimbo Na Maelezo Ya Kiisimu**

Jedwali linalofuata linatuonyesha muhtasari wa matukio ya uchanganyaji msimbo ya sentensi zinazopatikana katika matini zilizotumika.

## MATUKIO YA KUCHANGANYA MSIMBO

MATINI	UAMBATISHAJI WA KIUNGO	KUCHANGANYA MIONGONI MWA SENTENSI	KUCHANGANYA KATI YA SENTENSI	JUMLA
A	1	1	4	6
B	0	11	25	36
C	3	2	9	14
D	0	24	12	36
JUMLA	4	38	50	92

**Jedwali 1 Matukio ya kuchanganya msimbo kama yalivyojitokeza katika matini zote.**

Kutokana na data hii, tunaona kuwa kila aina ya kuchanganya msimbo inapatikana. Jambo hili linaonyesha ya kwamba kuchanganya msimbo ni sehemu moja kuu pahali ambapo kuna ulumbi katika usemi. Wazo hili linaelezwa na Romaine (1989:110) anaposema, kuwa kuchanganya msimbo ni kawaida na ni tabia iliyozoelewa katika jamii zenye ulumbi.

Kulingana na jedwali hili, uambatishaji wa viungo hautumiwi sana kwa sababu jukumu lake ni kuelezea hisia ambazo zinaweza kuelezwa na ishara za mwili kama vile za uso na mikono. Kuchanganya msimbo kati na miongoni mwa sentensi ni aina ambazo zimetumika sana kutokana na jedwali hili na data iliyokusanywa. Aina hizi mbili zinatumiwa sana kwa sababu watu hutumia lugha ambazo zinatumiwa na wao kila siku ili kufanikisha mawasiliano. Poplack (1980) anaeleza kuwa mara nyingi watu huingiza

neni moja kutoka lugha nyingine kwa sababu wamesahahu au hawajalijua lile neno katika lugha ya msingi ambayo inatumika katika sentensi ile.

Tukiangalia jedwali hili tunaona kuwa kuchanganya msimbo kati ya sentensi ndiko kunakojitokeza kwa wingi. Kati ya matukio tisini na mbili ya kuchanganya msimbo, matukio hamsini ni ya aina hii ya kuwa kati ya sentensi. Haya yanaonyesha ya kuwa wahubiri wana uwezo wa kutumia lugha hizi mbili. Maoni haya yanaelezwa na Berk-Seligson (1986:314) anaposema;

Utafiti uliofanywa na Pfaff (1979) kuhusu ulumbi wa watu wazima ulionyesha kuwa kuchanganya msimbo kwingi kati ya sentensi kunahusishwa na uwezo wa juu wa kuwa na ulumbi. Hivyo kuchanganya msimbo kati ya sentensi kunaweza kuchukuliwa kama kipimo cha uwezo wa kuwa na ulumbi. (TY)

Matukio ya kuchanganya msimbo miongoni mwa sentensi pia yalikuwa mengi katika data iliyochukuliwa. Berk-seligson (1986) anaelezea kuwa kuchanganya msimbo huku kunahusishwa na lugha moja kuwa haijazoelwa au kuwa inatawaliwa na nyingine. Tunaweza kusema kuwa hali nchini Kenya ni kuwa lugha ya Kiingereza inaonekana kama imetawala ile ya Kiswahili kwa kuwa ndiyo lugha rasmi. Vilevile ndiyo inayotumika katika shughuli nyingi za serikali. Inatumika katika kufundishia, utoaji wa hotuba na kadhalika. Kwa sababu hiyo, watu wengi wanapenda kujitambulisha nayo.

### 3.6 Dhima Ya Kuchanganya Msimbo

Kuchanganya msimbo huwa kuna majukumu mengi (Gumperz 1982, Gachinu 1996 ). Hata hivyo, kutokana na data hii majukumu matatu ndiyo yanayojitokeza. Kuchanganya msimbo katika data hii kunatekeleza ufafanuzi, kuisisitiza na unukuzi.

#### 3.6.1 Ufafanuzi

Tukiangalia data katika matini hizi tunapata ya kwamba wahubiri wanachanganya msimbo mahali ambapo wameshindwa au wanaonekana kutoelewa maneno katika lugha ambayo inatumika (Kiswahili) au mahali ambapo wanahisi maneno ya lugha nyingine ndiyo yanayoweza kuwasilisha dhana vizuri.

Kwa mfano mhubiri anaposema katika matini A;

1. *Ukiwa mtoto, umefanya mtihani wa kidato cha... (kimya) eh... eh  
standard eight mwaka uliopita ...*

(Ukiwa mtoto, umefanya mtihani wa kidato cha... (kimya) eh...eh darasa la nane mwaka uliopita)

2. *Yeye anauliza na inaweza kufika wakati mmoja jina langu liingie  
kwa computer ya retrenchment!*

(Yeye anauliza na inaweza kufika wakati mmoja jina langu liingie kwa compyuta ya kupunguzwa kwa wafanyikazi.)

Tukiangalia sentensi hizi mbili, tunaona ya kwamba mhubiri alijaribu kutafuta kisawe cha “*standard eight*” kwa Kiswahili akakosa. Hii ndiyo sababu anasitasita, na kwa sababu alikuwa atamke haya na wakati uo huo aendelee na usemi, kuchanganya msimbo

kukatokea. Katika sentensi ya pili, mhubiri hakuwa na kisawe cha jina “*retrenchment*” kwa lugha ya Kiswahili. Hivyo kuchanganya msimbo kukatokea.

Katika matini B, mhubiri anasema;

2. *Wayahudi si kama sisi, hawacha... hawachanganyikani. Myahudi ni Myahudi period Hakuna haja ya kuchanganya .Mungu wake ni Mungu wake period. Hana Mungu mwingine.*

(Wayahudi si kama sisi, hawacha... haachanganyikani. Myahudi ni Myahudi mwisho. Hakuna haja ya kuchanganya. Mungu wake ni Mungu wake mwisho. Hana mungu mwingine.)

Katika sentensi hii mhubiri alitumia neno la Kiingereza “*period*” ili kutoa maana kamilifu. Neno hili linapotumiwa katika lugha ya Kiingereza linaonekana kuwasilisha dhana vizuri kuliko neno “mwisho” la Kiswahili kwa sababu limezoeleka kutumiwa vile katika lugha ya Kiingereza.

(Angalia kiambatisho III 2, 4, 6. )

### 3.6.2 Kusisitiza

Kuchanganya msimbo vilevile kulitumiwa na wahubiri kwa jukumu la kusisitiza. Kwa mfano katika matini A mhubiri anasema;

3. *Anaanza kuyumba, anaanza kusikia kweli... He is not stable in his working place!*

(Anaanza kuyumba, anaanza kusikia kweli... si imara mahali pake pa kazi.)

Matini B vilevile imejaa kuchanganya msimbo ambako kunalenga jukumu hili. Mhubiri anaposisitiza vile wayahudi mpaka leo wanavyojiona kama waliochaguliwa anasema;

4 . *Mtoto akizaliwa baada ya miaka miwili au mitatu tayari amewekwa kakofia hako ... lakini kofia hiyo inashikishwa na inataka kuonyesha huyo mtoto si wa kawaida, ni mtoto myahudi na mtoto ambaye ana urithi. He is of a chosen race.*

(Mtoto akizaliwa baada ya mika miwili au mitatu tayari amewekwa kakofia hako ... lakini kofia hiyo inashikishwa na inataka kuonyesha huyo mtoto si wa kawaida, ni mtoto Myahudi na ni mtoto ambaye ana urithi. Yeye ni wa kabila lililochaguliwa.)

Sentensi hii ya Kiingereza iliyotamkwa na mhubiri ni ya kusisitiza tu kwa sababu tayari maana inaeleweka hata tukiiondoa.

Tukiangalia matini D, jukumu la msisitizo kupitia kuchanganya msimbo vile vile limejitokeza. Kwa mfano mhubiri anasema;

5. *Tuna tabia ya kuombaomba, na ile ni tabia ya umaskini.*

*Once you become a beggar, you are a beggar throughout your life.*

(Tuna tabia ya kuombaomba. Na ile ni tabia ya umaskini. Unapokuwa mtu wa kuomba unakuwa wa kuomba maishani mwako yote)

Katika mfano (5) mhubiri anasisitiza vile watu huwa maskini kwa kutaka kuombaomba kila siku. Wahubiri hawa wanasisitiza jambo kwa kuchanganya msimbo na katika kufanya hivi wanarudia. Kuchanganya msimbo huku kunaona na dai la Rayfields (1970:54) kuwa katika lugha ya kuongea ya kisasa kuchanganya msimbo kumekuwa dhana ya msisitizo kupitia kurudia katika lugha nyingine.

(Angalia kiambatisho III 2,4,6,8,16,29, 35, 54, 59, 87 kwa mifano ya kuchanganya msimbo kwa jukumu la kusisitiza).

Hivyo kuchanganya msimbo kwa jukumu la kusisitiza hutumia lugha kurudia yale maneno ambayo tayari yanaeleweka kutokana na muktadha. Aidha, hutumia lugha ya pili pahali ambapo anayezungumza anahisi kuwa lugha husika ina uwezo zaidi wa kuwasilisha anachotaka jinsi anavyotaka kipokelewe.

### 3.6.3 Unukuzi.

Kuchanganya msimbo katika lugha ya mahubiri kumetumiwa kwa jukumu la unukuzi. Haya yalipatikana katika data ya matini D ambapo mhubiri alinukuu sehemu za Biblia kwa Kiingereza na kurudia lile dondoo kwa lugha ya Kiswahili. Kwa mfano anasema;

6. *Ndiposa Mungu amemnenea mambo saba ... "I will make you into great nation."-That is number one. Abrahamu anaambiwa na Mungu nitakufanya uwe taifa kubwa sana.*

7. *"You will be a blessing." Wewe utakuwa baraka. Bwana akamwambia.*

(Angalia kiambatisho III 62, 63, 65, 66, 67, 68.)

Kunukuu katika lugha ya mahubiri hasa kupitia kuchanganya msimbo kunaelekeza katika msisitizo. Ni kama kwamba mhubiri alitaka kuonyesha kuwa yale si maneno yake lakini ni kama yalivyosemwa katika Biblia. Jambo hili linatuelekeza palepale kwenye uwezo wa lugha hizi mbili zinazochanganywa; Kiswahili na Kiingereza. Katika unukuzi, mhubiri alinukuu dondoo kwa Kiingereza na kulielezea kwa Kiswahili ingawa mahubiri yalikuwa kwa lugha ya Kiswahili. Hili linaonyesha kuwa mhubiri huyu alionelea kuwa lugha ya Kiingereza inaweza kuwasilisha dhana vizuri kuliko lugha ya Kiswahili. Kama tulivyodokeza hapo awali, jambo hili linaonyesha uwezo wa lugha ya Kiingereza dhidi ya lugha ya Kiswahili.

### **3.7 Hitimisho**

Katika sura hii, tumeangalia kuchanganya msimbo kama mojawapo wa sifa bainifu. Sifa bainifu hii imetumika kama mbinu ya kuendeleza ujumbe. Misimbo iliyochanganywa ni Kiswahili na Kiingereza.

Aina tatu za kuchanganya msimbo zilitumika katika lugha ya mahubiri. Tulikuwa na uambatishaji wa kiungo, kuchanganya msimbo kati na miongoni mwa sentensi. Hata hivyo, aina za kuchanganya msimbo kati na miongoni mwa sentensi ndizo zilizotumika zaidi.

Katika uchanganuzi wetu, tulipata sababu kadha za kutokea kwa kuchanganya msimbo. Kwanza, wahubiri walichanganya msimbo wakati walipokosa moja kwa moja kisawe cha

neni husika katika lugha ya Kiswahili. Kulikuwepo pia na kuchanganya msimbo kwa sababu ya kusisitiza. Hivyo, wahubiri walirudia jambo walilosema kwa lugha moja katika lugha nyingine ili kusisitiza. Msisitizo kupitia kuchanganya msimbo pia ulifanyika kupitia unukuzi. Vifungu fulani vya Biblia vilinukuliwa katika lugha ya Kiingereza na dondoo lile kurudiwa katika lugha ya Kiswahili. Jambo lingine lililojitokeza katika sifa bainifu hii, ni kwamba wahubiri walitumia lugha ya Kiingereza pahali walipohisi kuwa itaeleza dhana vizuri.

## **SURA YA NNE**

### **4.0 MSHIKAMANO KATIKA LUGHA YA MAHUBIRI**

#### **4.1 Utangulizi**

Katika sura ya pili na ya tatu tulichunguza ruwaza zilizojitokeza katika lugha ya mahubiri. Ruwaza hizi zilidhihirisha baadhi ya sifa bainifu za lugha ya mahubiri. Hata hivyo kuna ruwaza nyingine kuu ambayo ilijitokeza katika data. Hii ni sifa ya mshikamano.

Katika sura hii tumechanganua dhana ya mshikamano kwa kurejelea data iliyorekodiwa. Tumefanya hivi kwa kuchunguza aina za mshikamano zilizojitokeza. Kabla ya kuchanganua data, tumebainisha aina ya mshikamano inayohusika na kisha kutoa mifano kutoka kila matini kudhibitisha kuwa aina hizi za mshikamano zilijitokeza.

#### **4.2 Dhana Ya Mshikamano**

Dhana ya mshikamano huelezea uhusiano au ufungamano wa vijenzi vya lugha. Kulingana na Halliday na Hasan (1976:4), hii ni dhana ya kisemantiki ambayo hueleza uhusiano wa kimaana unaopatikana katika matini. Uhusiano huu husababisha kujengeka kwa matini. Mshikamano hutokea ikiwa kufasiriwa kwa kipashio fulani katika usemi kutategemea kipashio kingine. Kipashio kinachotegemewa kinaweza kupatikana ama kabla au baada ya kile kinachopaswa kufasiriwa.

Kiswahili ambayo ni lugha ambatishi huwa na sifa ya kuambatisha viambishi katika mzizi wa neno. Jambo hili hufanyika ili kuongeza habari inayopatikana katika neno hilo.

Kulingana na Kapinga (1983:15), kiambishi ni mofimu inayoambatishwa kwenye mzizi au shina la neno ili kulitambulisha neno lenyewe. Lugha ya Kiswahili huwa na viambishi vya aina mbili (Mgullu 1999). Viambishi awali ambavyo hupatikana katika mwanzo wa mzizi wa neno na viambishi tamati vinavyopatikana katika mwisho wa mzizi wa neno. Katika Kiswahili, kila kiambishi huwa ni mofimu lakini sharti kiambatanishwe na mzizi wa neno jingine kwa sababu hakiwezi kujisimamia. Viambishi hivi vinapopatikana katika matumizi halisi ya lugha basi huwa na nguvu za ushikamano. Kwa mfano;

Wana wa Israeli walikuwa na shida nyingi walipokuwa Misri. Walifanyizwa kazi ngumu isiokuwa na malipo. Mungu aliwatoa kutoka utumwa huo.

Tukiangalia sentensi hii viambishi kadhaa vinaleta mshikamano. Kwa mfano kiambishi 'wa' katika "walikuwa, walipokuwa na walifanyizwa" kinarejelea Wanaisraeli. Kiambishi tamati 'o' katika "huo" kinarejelea utumwa. Kwa hivyo viambishi hivi vinaleta mshikamano.

Kaida ya mshikamano ni pale ambapo kufasirika kwa kipashio kimoja kunategemea kipashio kingine. Siyo kuwepo kwa kipashio fulani ambako kunazusha mshikamano bali ni uhusiano uliopo kati ya vipashio hivyo.

Mshikamano unaelezwa kwa upande mmoja kupitia sarufi na vile vile kupitia msamiati. Kulingana na Halliday na Hasan (1976:5) katika mshikamano, maana za kijumla

huelezwwa kupitia sarufi na zile maalum kupitia msamiati. Hivyo kuna mshikamano wa kisarufi na wa kimsamiati. Tuna aina tano za mshikamano. Nazo ni;

- i) Urejeshi
- ii) Ubadilishaji
- iii) Udondoshi
- iv) Uunganishi
- v) Msamiati

Kulingana na data iliyorekodiwa, kila aina ya mshikamano ilijitokeza ingawa kuna aina zilizojitokeza kwa wingi. Lugha ya mahubiri ilidhihirisha kuwa mshikamano mwingi ulijitokeza kupitia msamiati na urejeshi hata ingawa aina zingine zilikuwepo. Tunachunguza kila aina ya mshikamano na kuitolea mifano katika matini zote nne.

## 4.3 Aina Za Mshikamano

### 4.3.1 Urejeshi

Kulingana na Halliday na Hasan (1976) na Halliday (1985b) urejeshi unatokea pale ambapo kufasirika au kueleweka kwa kipashio kimoja kunategemea kingine katika matini. Ikiwa kutakuwa na muumano wa sentensi katika matini, sharti kuwe na vipashio vinavyorejeleana. Hivi ni kumaanisha kuwa badala ya vipashio hivi kufasiriwa kisemantiki kama vinavyojisimamia, vinarejelea kitu kingine katika kufasiriwa kwake.

Kwa mfano, tukiangalia data ya matini A tuna sentensi hii;

1. *Basi, hii ni kalenda, ya Anglikana kweli imetuletea masomo ambayo yako muhimu sana mwaka huu mpya.*

Tukiangalia kipashio 'hii' kinafasirika tukirejelea "kalenda" na vile vile 'ya' na 'i' katika "imetuletea." 'Ambayo' na 'yako' ni vipashio ambavyo vinafasiriwa tukirejelea "masomo." Kwa jumla vipashio hivi vinaonyesha kuwa lazima tupate ujumbe mahali pengine.

Tukichunguza mfano huu tunapata ya kwamba mshikamano hupatikana katika mwendelezo wa urejeaji, ambapo kitu kimoja kinaingia katika usemi kwa mara ya pili. Urejeshi una sifa ya kisemantiki ya kuonyesha udhahiri. Kwa mfano tukiangalia mfano (1) tulioutoa hapo juu, kipashio 'hii' na 'i' katika "imetupatia" vinarejelea ile ile kalenda na si nyingine. Vilevile 'ambayo' na 'yako' vinarejelea yale yale masomo na si mengine. Hivyo tumeona ya kwamba urejeshi unaonyesha uhusiano wa kisemantiki.

Halliday na Hasan (1976) wanapendekeza majina yafuatayo ili kueleza urejeshi:

- i). Endofora
- ii). Ekisofora
- iii). Anafora
- iv). Katafora

Endofora na Ekisofora ni majina yanayosimamia aina mbili muhimu za urejeshi katika taaluma ya isimu. Katika Ekisofora, mzungumzaji/msikilizaji hurejelea mazingira ili kufasiri mazungumzo. Kinachorejelewa hupatikana katika mazingira ya mazungumzo. Urejeshi huu hutumika sana sana kupitia kategoria ya kisarufi ya viashiria. Kwa mfano tukiangalia data ya matini A mhubiri anapozungumzia kuhusu upendo kuwa nguzo anasema;

2. Na kwa nini nasema namna hiyo? Nikiangalia upande wangu wa kushoto pale naona watoto pale, nikiangalia huku kwa viti familia imeyakilishwa vilivyo

Viashiria 'pale' na 'huku' katika mfano (2) hapo juu vinatuelekeza kwenye mahali maalum ambapo tunaweza kuona na kuashiria. Urejeshi wa aina hii unadhihirisha ufungamano uliopo kati ya lugha na mazingira. Urejeshi huu hauonyeshi mshikamano. Urejeshi huonyesha mshikamano ikiwa unarejelea kipashio katika matini.

Endofora ni aina ya urejeshi unaopatikana katika matini. Maana inayokusudiwa inaeleweka bila kurejelea mazingira yaliyo nje ya matini ile. Maana inaeleweka bila kurejelea muktadha usiokuwa wa kiisimu. Hata hivyo, Ekisofora na Endofora huingiliana kiasi kuwa wakati mwingine ni vigumu kujua kama tunashughulikia Endofora au Ekisofora.

Kwa mfano katika data ya matini C mhubiri anaposema;

3. Afisa wa elimu alipofika pale binti aliposimama, akamwangalia, jinsi alivyotabasamu, jinsi anavyoongea, oh afisa akasema...

Tukiangalia 'pale' katika mfano huu, tunaweza kuchukulia kama ni urejeshi wa Ekisofora lakini ni wa Endofora. Hii ni kwa sababu mhubiri alikuwa anatoa kisa fulani na hakutarajia aliokuwa akizungumza nao 'pale' katika mazingira walimokuwa.

Endofora kwa upande wake imegawika mara mbili. Kuna anafora ambao ni urejeshi nyuma na katafora ambao ni urejeshi mbele. Aina zote mbili zilipatikana katika data ya matini zote nne. Urejeshi wa anafora unatokea pale ambapo kiungo kinachofasiriwa hurejelea kiungo ambacho kimetajwa tayari. Kwa mfano katika data ya matini A tuna mfano ufuatao:

4. *Na Biblia inatuambia somo lile tuli... tulilosomelwa –somewa la Isaiah*

*alikuwa anaongea juu ya familia ya Israel. Na tukaona anaongea mambo ya mtumishi ambaye atakuja.*

Kiungo 'anaongea' kinawakilisha Isaiah ambacho ni kiungo kilichotajwa hapo awali. Hivyo mofimu 'a' katika anaongea inarejelea Isaiah. Data ya matini B ilionyesha aina hii ya urejeshi:

5. *Sijui Wakristu tunaweza kuwa na pia wakati mwingine na mafikirio kama hayo.*

Kiungo 'tu' katika tunaweza kinarejelea msemaji ambaye amewakilishwa na 'si' katika sijui na vilevile Wakristu. Kiungo 'hayo' kinarejelea mafikirio ambayo yamezungumziwa awali kuwa Mungu ni wa watu fulani. Ili kufasiri viungo hivi, tunarudi nyuma katika mazungumzo na kupata maana tunayotafuta. Data ya matini C vile vile ilikuwa na urejeshi wa aina hii:

6. *Oh, - Macullata wakaendelea na huyo afisa, ikafika siku moja, Emaculata bahati mbaya akapata mimba. Akaenda kwa afisa akamwambia-afisa, nina mzigo wako...*

Kiungo 'akaenda' na 'akamwambia' vinarejelea Emacullata ambalo ni jina lililotajwa hapo awali.

Matini D vile vile ilikuwa na urejeshi huu wa kianafora. Tutatoa mfano ufuatao;

7. *Wakristu watoto wetu ndio wangukuwa number one in the classes. They should be in the top tens.*

Katika sentensi hii, kiungo 'they' (wao) kinarejelea watoto ambao wametajwa awali. Hivyo, katika urejeshi huu wa anafora, ili kuelewa kiungo fulani katika lugha, tunawajibika kutazama nyuma na wakati mwingine kuruka sentensi kadha wa kadha ili kupata kiungo kinachoweza ufasiri wetu.

Urejeshi wa kikatofora hutokea wakati tunapowajibika kutegemea kiungo kinachopatikana baadaye. Kwa mfano katika matini B, tuna mfano ufuatao;

8. *Ndugu wakristu, sisi kama wakristu wa hii leo, tuangalie ile nyota na hii nyota hakuna kitu kingine, ni Yesu katika maisha yetu*


Katika sentensi hii, viungo 'ile nyota' na, 'hii nyota' vinafasirika katika sentensi ya tatu tunapopata ya kuwa 'nyota' ni Yesu. Data zingine zilidhihirisha urejeshi huu kwa mfano katika matini C mhubiri anaposema;

9. Rafiki wa pili tunayempenda sana ndiye huyu. Huyu ni baba, mama, mjomba, shangazi na jirani.

10. Rafiki wa kwanza alimpenda mno, unajua tukisema sisi Waswahili, eh eh...Tunaofahamu Kiswahili cha huko...

Tukiangalia sentensi hizi, 'huyu' katika mfano (9) ni kiungo kinachotajwa kabla ya kile kiungo kinachorejelea. Baba, mama, mjomba, shangazi, wanatajwa na ndio wanaorejelewa na huyu. Katika mfano wa mfano (10) kiungo 'tukisema' kinarejelea Waswahili ambao wanatajwa baadaye.

Urejeshi huu wa kikatafora ni nadra kutumika katika matini ukilinganishwa na wa anafora. Halliday na Hasan (1976:33) wameweka uhusiano wa aina hizi za urejeshi katika mchoro ufuatao.



Kupitia mifano ya urejeshi iliyotolewa hapo juu ni dhahiri kuwa ngeli ni muhimu sana. Hii ni kwa sababu inategemewa katika upatanishi wa kisarufi. Urejeshi huu unadhihirika kupitia viambishi, viwakilishi nafsi na viashiria.

Ingawa matini zote nne hazikutumia muda sawa, hivyo zingine zilikuwa ndefu, kuna matini zilizotumia urejeshi kwa wingi. Matini A ilionyesha matukio (26) ya urejeshi. Kati ya haya kulikuwa na urejeshi wa Kieksofora na wa Kiendofora. Kutokana na data hii, mhubiri alitumia urejeshi wa kianafora zaidi kuliko wa kikatafora. Data ya matini B ilifuata mtindo uu huu. Katika data hii kulikuwa na matukio (71) ya urejeshi. Kama katika matini A, kulikuwa na urejeshi wa Kieksofora na wa Kiendofora. Vilevile urejeshi wa kianafora ndio ulioshamiri ukilinganishwa na wa kikatafora. Urejeshi katika matini C na D ulifuata misingi hii hii. Matini C ilikuwa na matukio (52) na katika matini D matukio (42)

Kutokana na mifano iliyotolewa, tumeona kuwa wahubiri hutumia urejeshi nyuma (wa kianafora) kwa kutumia mofimu huru au sizizo huru. Vilevile tumepata matumizi ya urejeshi wa kieksofora ambao unategemea muktadha wa hali. Hili linatokana na jambo kuwa mahubiri yalikuwa ya ana kwa ana hivyo mhubiri na hadhira yake wangeweza kufasili kinachozungumziwa. Ni kama Crystal na Davy (1969:102-103 ) wanavyoeleza kuwa hotuba isiyoandikwa inapotolewa hutegemea sana muktadha wa hali.

Mshikamano wa urejeshi huwa na jukumu la kufanya mzungumzaji asitumie maneno mengi. Katika lugha ya mazungumzo, ni rahisi kutumia viambishi badala ya kutumia nomino nzima. Kwa mfano katika matini B mhubiri anaposema;

*Mamajusi walipotaka kuendelea nyota na ikaja ikawaonyesha palepale.*

*Walipoenda palepale, waliona nyota ... Wametoa manemane, wametoa uvumba...*

Tukiangalia sentensi hii, ikiwa urejeshi haukutumiwa, mhubiri angetumia maneno mengi na labda kufanya maana isieleweke. Kwa mfano tungekuwa na aya kama hii;

Mamajusi walipotaka kuendelea nyota na ikaja kuwaonyesha mamajusi palepale. Mamajusi walipoenda palepale. Mamajusi waliona nyota. ...

Mamajusi wametoa manemane, mamajusi wametoa uvumba...

Hivyo, kutumia kiambishi 'wa' badala ya mamajusi ni njia fupi ya kusema jambo. Katika kufanya hivi, waumini wanaelewa zaidi.

#### **4.3.2 Ubadilishaji Na Udondoshi**

Kimsingi, ubadilishaji na udondoshi ni mfanyiko mmoja. Ubadilishaji hutokea ikiwa kipashio kimoja kinabadilishwa na kingine. Udondoshi nao ni utoaji wa kipashio pasipo kuweka kingine pahala pake. Hivyo, udondoshi unaweza kufasiriwa kama aina ya ubadilishaji ambapo kipashio hakibadilishwi na kingine. Aina zote mbili za mshikamano zilidhihirika katika data iliyorekodiwa ingawa si kwa wingi zikilinganishwa na urejeshi na mshikamano wa kimsamiati.

### 4.3.2.1 Ubadilishaji

Ubadilishaji hutokea ili kuepuka uradidi wa maneno au hata mafungu ya maneno.

Uhusiano wa vipashio katika aina hii ya mshikamano huwa ni wa kimsamiati na kisarufi zaidi kuliko kuwa wa kimaana kama ilivyo katika urejeshi. Tukiangalia data ya matini A mifano kadha ya ubadilishi inajitokeza. Tutatoa mifano ifuatayo:

1. *Sijui unga ni pesa ngapi na siku hizi, kila ...mama analia, akifika kule ni kulia, kwa sababu hata uchumi umepita wakina baba wetu. Si hiyo peke yake, nikiangalia mzee wa siku hizi ana shida.*
2. *Yeye anauliza, inaweza kufika wakati mmoja jina langu liingie kwa 'computer ya retrenchment'? Anaanza kujiuliza hayo.*

Tukiangalia sentensi ya (1) tunapata kwamba 'hiyo' ni kabadala cha uchumi. Katika mfano wa (2) 'hayo' ni kabadala cha maneno jina langu liingie kwa 'computer ya retrenchment'.

Data ya matini B vile vile ilikuwa na aina hii ya mshikamano:

3. *Wewe kama baba unapofanya mambo mazuri lazima utalipa...lazima utaumia lazima utalia siku moja, ulipe. Si hata Yesu alifanya hivyo?*
4. *Walipoenda pale pale, waliona nyota... wametoa manemane, wametoa uvu...uvumba na pia wametoa dhahabu. Na katika utamaduni wa wayahudi mtu anapokwambia nimetoa hivyo vitu vitatu kama zawadi...*

Sentensi nambari (3) imetumia kabadala 'hivyo' kusimamia alilipa. Katika mfano (4) 'hivyo vitu vitatu' ni kabadala cha "manemane", "uvumba" na "dhahabu."

Ubadilishaji ulijitokeza katika data ya matini C, kama mfano ufuatao unavyothibitisha.

5. *Eti unanipenda au unanitamani? Unanipenda au unanitamani. Afisa akamwambia ninakupenda. Ebu sema vizuri afisa-akasema yote*

Katika mfano (5) kiungo 'yote' ni kabadala cha "kupenda na kutamani."

Data ya matini D pia ilidhihirisha aina hii ya mshikamano. Kwa mfano;

6. *Sijaona maskini anaomba pale river road na 'kungurukunguru' amenunua nyumba. If you know one, tell me.*

Tukiangalia mfano huu 'one' (mmoja) ni kabadala cha maskini.

Mifano iliyotolewa inathibitisha kuwa ni kama kanuni kuwa ubadilishaji unapofanyika basi kipashio badilishi huwa na kazi moja ya kimuundo na kipashio kinachobadilishana nacho. Aina hii ya mshikamano haikutumiwa sana. Katika matini A kulikuwa na matukio (4), matini B matukio (4), matini C matukio (5) na matini D tukio (1) ambalo halikuwa katika lugha ya Kiswahili. Hii inaonyesha kuwa katika lugha ya Kiswahili, aina hii ya mshikamano haitumiki sana. Kauli hii inaafikiana na Njue (1989:64), anaposema kuwa vabadala ni nadra katika ngano za Kiswahili. Njue anatoa hoja kuwa watambaji ngano hupendelea mshikamano wa kimsamiati. Haya

ndiyo yalijitokeza katika lugha ya mahubiri. Kama ilivyodokezewa hapo awali, ubadilishaji hutokea ili kuepuka kurudiarudia maneno au hata mafungu ya maneno.

#### 4.3.2.2 Udondoshi

Udondoshi ni aina ya ubadilishaji ambapo kinachobadilishwa hakidhihiriki katika mazungumzo au maandishi. Ijapokuwa kinachobadilishwa hakitokei sentensi inaeleweka barabara. Ishara \* itatumiwa kuonyesha pahali neno limedondolewa.

Kwa mfano katika matini A tunaweza kutoa mifano ifuatayo;

1. *Nataka kukuambia wewe ukimaliza form four...umepiga rami mpaka kiatu kikiangaliwa chini unaanza ku...kujiuliza kazi itapatikana wapi. Mpaka saa hizi kila mmoja yule anatafuta\* ataanza wapi, aanzie wapi, amalizie wapi, anashindwa.*

Tukiangalia mfano huu tunapata ya kwamba neno 'kazi' limedondoshwa kati ya neno anatafuta na ataanza. Hata hivyo, sentensi inaeleweka. Data ya matini B pia ilidhihirisha aina hii ya mshikamano:

2. *Tunaambiwa hawa maya...mamajusi, eh watu ambao wamesoma, wanaenda kwa Mfalme wanamwambia ya kwamba, kumeandaliwa mfalme hebu tuonyeshe kwa sababu you are so informed,...halafu\* anaita manabii anawauliza,\* amezaliwa wapi?*

3. *Na mbona hamfanyi kanisani hivyo? Tunapopokea\*, ebu father pokesha wa KANU (Kenya African National Union- Chama cha Kisiasa) kwa sababu uwape ile kubwa kwa sababu ndio wanatawala na ile kidogo kidogo uwape ...*

Mifano hii miwili inaonyesha udondoshi. Katika mfano wa (2) tuna udondoshi mara mbili. Mhubiri anaposema *'halafu anaita...'* amedondoa mfalme (Herode) lakini tunaelewa kuwa ni yeye aliyeita manabii kutokana na muktadha. Aina ya pili ya udondoshi katika sentensi hii unatokea wakati Herode anapowauliza manabii, amezaliwa wapi? Kiungo kilichodondolewa hapa ni mfalme (Kristu) lakini vile vile sentensi inaeleweka. Mfano (3) vile vile una udondoshi lakini wa kipekee. Mhubiri anaposema, *'Tunapopokea, ...'* amedondoa kiungo sakramenti. Hata hivyo udondoshi huu unaweza kueleweka tu na washiriki wa kanisa hili ambao wanajua kuwa kinachopokewa ni sakramenti.

Data ya matini C vile vile ilikuwa na aina hii ya mshikamano.

Tutatoa mifano ifuatayo;

4. *Yule afisa, afisa akasema, mimi ni huyu Emmaculata. Maskini Emmaculata hajui moyoni.\* Akamwambia, Ema, nakupenda*
5. *Mungu si Athmani, kwetu anasema alipokua mtoto yule akasoma na akamaliza form four akachaguliwa kujiunga na chuo kimoja cha Business*

*College Dar-es-salaam. \* Amekwenda kule, Mama yuko Dar, hamjui mtoto, ...*

Tukiangalia mfano (4) tunapata neno afisa limedondoshwa kabla ya neno 'akamwambia Ema'. Hata hivyo tunaelewa kuwa afisa ndiye aliyekuwa anamwambia Emacullata jinsi anavyompenda. Katika mfano (5) tuna udondoshi mara mbili. Baada ya Dar-es-salaam, neno mtoto limedondolewa kabla ya neno amekwenda. Hata hivyo, tunaelewa kuwa mtoto ndiye aliyeeenda Dar-es-Salaam. Mhubiri anaendelea kusema, 'alikwenda kule' na katika kusema hivi, neno Dar-es-salaam limedondolewa.

Katika matini D, mifano ya aina hii ya mshikamano ilijitokeza. Kwa mfano;

6. *Basi huyu Abrahamu ambaye ndiye baba wa kizazi hiki, akaambiwa wewe nitakufanya taifa kubwa...watu wote wa dunia watabarikiwa kwa ajili yako. Ndiposa\* akasema, kutoka uzazi wako, nitaweza kubariki watu wengi wa dunia.*

7. *Biblia tumesoma katika maisha yako, ungetaka kubarikiwa na hiyo ndiyo kusudi ya Mungu,...maana hafahamu Unafikiria haya maandiko iliandikiwa Mayahudi. Wewe ndiye myahudi wa leo. Sasa- haya maandiko ni yako,... na ndipo tukasoma,\* ikatwambia, you will be blessed as you come out, as you come in.*

Tukiangalia sentensi (6) tunapata ya kwamba kuna udondoshi mhubiri anaposema, 'ndiposa akasema'. Neno Mungu limedondolewa katika sentensi hii. Lakini kulingana na

yale ambayo yalikuwa yamezungumziwa hapo awali, tunaelewa Mungu ndiye aliyekuwa akimwambia Abrahamu maneno haya. Katika mfano (7) mhubiri anaposema 'Na ndipo tukasoma, ikatwambia...' amedondoa neno Biblia ambalo lilikuwa limetajwa awali.

Aina hii ya mshikamano ilikuwa na matukio mengi kuliko ubadilishaji. Matini A ilikuwa na matukio (8), matini B matukio (17), matini C matukio (9) na matini D matukio(8)

Kama katika ubadilishi, udondoshi hutumika kwa jukumu la kutorudia maneno. Hii ni kwa sababu hata ingawa kurudia kunaweka jambo kuwa dhahiri, kunaweza vilevile kuchosha. Udondoshi pia unaweza kutumika kuleta waumini karibu na mhubiri. Hii ni kwa sababu ikiwa waumini wanaweza kufuata pahali ambapo hapana maneno kadhaa, basi ina maana kuwa walikuwa wakifuata yaliyokuwa yanaendelea awali katika mahubiri.

Tunapoangalia aina hizi mbili za mshikamano, ubadilishaji na udondoshi, tunaona kuwa katika lugha ya Kiswahili ni dhana zinazokaribiana sana. Aina hizi zinakaribiana kiasi kwamba tunaweza kutodhibitisha kama ni udondoshi ama ubadilishaji. Tukirejelea mfano (5) hapo juu, mhubiri anaposema 'amekwenda kule', 'kule' ni kiungo ambacho kinaweza kuwa kibadala cha Dar-es-salaam, lakini kwa sababu katika sentensi hiyo kuna kiungo kingine 'Dar' kiungo 'kule' chaweza kuchukuliwa kama ni mahala pengine. Hivyo ni katika kuelewa kuwa kuna udondoshi ambapo tutaelewa. sentensi hii. Tunaweza kutamatisha kwa kusema kuwa kutotokea kwa kipashio kinachodondoshwa katika muundo wa sentensi hakusababishi kutoeleweka.

### 4.3.3 Uunganishi

Kapinga (1983:185) amepatia viunganishi anavyoita vihusishi fasili kuwa ni;

Aina mojawapo ya maneno yanayounganisha. Maneno hayo huonyesha uhusiano baina ya neno na neno au baina ya fungu moja la maneno na fungu lingine.

Kutokana na maelezo haya, kiunganishi kina kazi ya kuleta vipashio pamoja (Mgullu,1999). Uunganishi ni tofauti kiasili ukilinganishwa na aina zingine za mshikamano. Uunganishi hauonyeshi uhusiano wa kinafora tu.

Viungo vya uunganishi huwa havina ushikamano vyenyewe lakini kwa njia isiyo ya moja kwa moja huwa na ushikamano kwa sababu ya maana yake inayodhihirika. Hivyo, uunganishi huwa si wa kisarufi moja kwa moja. Katika uunganishi, kuna maneno yanayotumiwa ambayo yana nguvu za mshikamano. Nguvu hizi ni kama zile zinazoletwa na aina zingine za mshikamano. Hata hivyo, katika uunganishi neno linalotumiwa huonyesha tu kuwa sentensi fulani zinaumana. Neno hili linakuwa daraja hivi kwamba likokikosekana, basi mshikamano unakisiwa tu bali haujitokezi wazi wazi. Haya ni yakilinganishwa na urejeshi ambapo uhusiano wa vitajwa kwa kawaida huwa ni wa kimaana. Hii ina maana kuwa tunawajibika kurejelea kwingine ili kufasiri kiungo fulani. Au tukiangalia udondoshi na ubadilishaji ambapo kuwepo au kutokuwepo kwa kabadala humaanisha kuwa nafasi ya kiungo fulani imesimamiwa na kingine ambacho hakijidhihirishi. Uunganishi kama aina ya mshikamano ulijitokeza kwa wingi katika lugha ya mahubiri.

Tunapochunguza data ya matini A, tulipata baadhi ya mifano kama;

1. *Kile kinanifanya niseme kwamba nakupenda, neno langu asubuhi ya leo lahusu upendo. Na kabla niendelee na mahubiri ningependa kusema...*
2. *Basi, ikawa ni unabii, utatoka kwa Mungu, na huo unabii utatoka kwa Mungu huwa ni unabii unaweza kuwa na mara mbili. Mara ya kwanza, kuna unabii unatendeka...*

Tukiangalia mfano (1) kiunganishi 'na' kina nguvu za ushikamano kwa sababu mhubiri katika sentensi ya kwanza ameelezea anataka kuhubiri juu ya nini. Katika sentensi ya pili ambayo inaunganishwa na 'na' mhubiri anaelezea atakayofanya kabla ya kuendelea na aliyotaja. Katika mfano (2) tunapata kiunganishi 'mara ya kwanza' kikiwa na nguvu za ushikamano kwa sababu kinaonyesha sentensi hizi mbili zinaumana na zina uhusiano.

Katika matini B, kuna mifano chungu nzima ya mshikamano kupitia uunganishi. Tutatoa mifano ifuatayo;

3. *...Mbona hamuulizi padre wetu ni Mkikuyu, next time lazima awe Mjalu, ah –not in the catholic church. Au tuseme askofu mkuu katika nchi hii ni...*
4. *Endapo unafanya mambo mazuri lazima utalipa....si hata Yesu alifanya hivyo? Alikuwa...Kwa hivyo kila mkristu ambaye anafuata ukristu wake lazima atalipa.*

Mifano hii miwili inaonyesha mshikamano kupitia uunganishi. Katika sentensi ya tatu, kiungo 'au' kinaonyesha nguvu za mshikamano kwa sababu kinawezesha sentensi hizi mbili kuumana. Katika mfano (4) kiungo 'kwa hivyo', kinaonyesha kuwa sentensi hizi mbili zina uhusiano.

Data ya matini C pia inaonyesha uunganishi kama aina ya mshikamano. Tutatoa mifano ifuatayo:

5. *Siku moja, kijana akamaliza course. Sasa rafiki yake anaendelea kumtafutia kaa ... nyumbani.*
6. *Anasema, Emacullata ndiye aliyekuwa mama, alikuwa mama mtoto, lakini alishindwa kumweleza kwamba mimi ndio mama yako. Ndivyo hivyo leo, tumemwacha Yesu...*

Sentensi nambari (5) ina kiunganishi 'sasa' ambacho kinaonyesha kuwa sentensi mbili zinazozungumziwa zina uhusiano. Vile vile mfano (6) sentensi ya pili inaonyesha uhusiano na ya pili kupitia kiunganishi 'ndivyo hivyo'.

Katika matini D, ushikamano kupitia uunganishi pia ulijitokeza mifano ifuatayo:

7. *Abrahamu wakati Mungu aliona watu wamekuwa waovu, alimchukua Abrahamu, ili dunia ikaweze kukombolewa,... Basi Ibrahimu aliamurishwa, akaambiwa toka chini ya watu, ...*

8. ... japo ningetaka ujue ni kitu kimoja ya kwamba kwa muda mrefu sana kila kukiacha umetosheka na kuishi umasikini ulio nao. Lakini Mungu, hakukumba uishi katika hali ya umasikini.

Tukiangalia mfano (7) kiunganishi 'basi' kina nguvu za ushikamano. Kiunganishi hiki kimeunganisha sentensi ya kwanza na ya pili kwa sababu sentensi ya pili inaendeleza mawazo ambayo yamejitokeza katika sentensi ya kwanza. Vilevile, tukiangalia mfano (8) tuna kiunganishi 'lakini' ambacho kimeunganisha sentensi hizo mbili. Sentensi ya kwanza inaelezea kuhusu kuishi katika hali ya umasikini na dhana hii inaendelezwa katika sentensi ya pili.

Bali na mshikamano wa kimsamiati na wa urejeshi, uunganishi ndio uliotumika sana katika mahubiri. Matini A ilikuwa na matukio (17), matini B matukio (28), matini C matukio (17) na matini D matukio (21). Uunganishi ni aina muhimu sana ya mshikamano kwa sababu ndio hufanya matini nzima kuwa kitu kimoja.

#### 4.3.4 Msamiati

Mshikamano wa kimsamiati hudhihirika kupitia uteuzi wa msamiati. Kwa jumla, aina hii huwa ni ama marudio ya msamiati, matumizi ya visawe au matumizi ya maneno yanayokaribiana kimaana.

Nomino za kawaida vilevile huwa na nguvu za kimshikamano ikiwa zinatokea katika muktadha wa urejeshi. Hii ina maana kuwa zina kitajwa kimoja na kipashio kilichotangulia. Kwa mfano;

Unaweza kunielezea unapitia wapi ukienda Kawangware?

Sijawahi kuenda mahali hapo.

Neno 'mahali' ni nomino ya kawaida lakini ina nguvu za mshikamano wa kimsamiati kwa kuwa inarejelea Kawangware. Hata hivyo, nomino hii haiwezi kuwa na jukumu la mshikamano ikiwa haiambatani na kirejeshi kingine. Kirejeshi katika sentensi hii ni 'hapo' ambacho kinaonyesha kuwa panaporejelewa ni Kawangware na si mahali pengine. Jambo hili linaoana na maoni ya Halliday na Hasan (1976:275) kuwa nomino ya kawaida ikiwa na jukumu la mshikamano inaambatanishwa takribani kila wakati na kirejeshi cha kudhihirisha.

Kuna aina mbili muhimu za mshikamano wa kimsamiati .Kwanza, tunaweza kuwa na msamiati ule ule ukirudiwa katika kuleta mshikamano. Tunaweza pia kuwa na msamiati ambao unashahibiana kimaana ukileta mshikamano katika matini.

Kwa mfano;

Nchi ya Kenya ni yenye amani. Hii ndiyo

maana nchini Kenya vita havitokei ovyo ovyo.

Neno “Kenya’ lina nguvu za mshikamano wa kimsamiati linaporudiwa mara ya pili. Kama tulivyoelezea awali tunaweza kuwa na msamiati unaoshabihiana kimaana ukileta mshikamano. Kwa mfano:

Ali alipata shida nyingi alipoenda nga’ mbo .

Kwa sababu ya taabu akaanza kutumia madawa ya kulevya.

Katika sentensi hii ‘taabu’ na ‘shida’ ni maneno ambayo ya na maana sawa. Hivyo taabu katika sentensi ya pili inaleta ushikamano katika matini hii.

Aina hii ya mshikamano wa kimsamiati ndiyo iliyojitokeza kwa wingi katika data iliyochukuliwa. Aina ya pili ya mshikamano wa kimsamiati hutokea ikiwa msamiati unaoandamana kwa kawaida na ambao ni vinyume unaweza kutumiwa. Kwa mfano ;

Wanaume wa kijiji cha Sheba ni

wakamavu? Wanawake ni wakamavu.

Tukiangalia mfano huu wanawake na wanaume si visawe na maneno haya hayarejelei kitu kimoja . Hata hivyo, kawaida maneno haya yanaandamana na kutokea kwake katika usemi husaidia katika uundaji kimuundo. Hivyo ni maneno yanayoleta mshikamano. Madai haya yanapata uzito yakichunguzwa pamoja na kauli ya Halliday na Hasan (1976:285) wanaposema;

Tunaweza kupanua msingi wa uhusiano kileksia ambao huonyesha nguvu za mshikamano. Tunaweza kufanya hivi kwa kusema kuwa kuna

mshikamano kati ya jozi lolote la vipashio vya kileksia ambayo huwa na maana kileksia. (TY)

Tukirejelea data iliyorekodiwa tunapata ya kwamba mshikamano wa kimsamiati ulijitokeza kwa wingi katika lugha ya mahubiri. Kutokana na data ya matini A, kuna mifano ifuatao:

1. *Na masomo yake tumesomewa; yako na uhusiano sana na (kimya) mtumishi ambao Isaiah alisema atakuja...Na Biblia inatuambia somo lile tulilosomelwasomewa la Isaiah, alikuwa anaongea juu ya familia ya Israel. Na tukaona anaongea mambo ya mtumishi ambaye atakuja.*
2. *Mungu atakuonyesha mahali utapita. Kwa hivyo, kila ukifikiria wewe ukiangalia mzigo wako haujiwezi. Kumbuka ya kwamba Mungu atabariki wale ambao wako karibu na wao.*

Tukiangalia sentensi hizi mbili tunaona kuwa kuna mshikamano wa kimsamiati. Katika mfano (1) maneno *Mtumishi* na *Isaiah* yamerudiwa na sentensi zile zinaumana. Katika mfano (2) neno *Mungu* ndilo linaloleta mshikamano wa kimsamiati. Neno hili linaonyesha ni yule yule Mungu aliyetajwa katika sentensi ya kwanza. Data ya matini B vile vile inadhahirisha mshikamano wa kimsamiati:

3. *Katika somo letu la kwanza, tunasikia vile nabii Isaiah alipotabiri akiambia Yerusalem Amka uandae nuru kwa sababu nuru ilikuwa ianze Yerusalem. Na Yerusalem ni mji ambao ni mtakatifu mpaka sasa, wa Wayahudi.*

4. *Nabii Isaiah anafafanua katika mwokozi, masiha ni wa kila mtu.*

*Mtakatifu Paul kwa Waefeso anawaambia vivyo hivyo. Ninyi wa...Waefeso mna...ati kwa sababu mimi mtakatifu Paul niliwahubiria mwokozi amezaliwa kwenu, mkombozi huyu Yesu Kristu si wenu tu, ni wa kila mtu, ni mkombozi, pia wa...*

Mifano ambayo tumeitoa hapa inaonyesha mshikamano wa kimsamiati. Katika mfano (3) kurudiwa kwa jina *Yerusalemu* ndiko kunakoleta mshikamano katika sehemu hii ya matini. Hivyo Yerusalem inapotajwa mara ya pili na ya tatu, msikilizaji anaelewa kuwa ni ile ile Yerusalem iliyotajwa mara ya kwanza. Katika mfano (4), sehemu hii ya matini inaonyesha mshikamano wa hali ya juu katika ya kurudiakurudia maneno na vilevile matumizi ya visawe. Maneno kama *mtakatifu paulo* na *Waefeso* yamerudiwa. Visawe vilivyotumiwa ni *Masiha* na *Yesu Kristu*, na *Mkombozi* na *Mwokozi*. Vile vile licha ya *Mkombozi* na *Mwokozi* kutumiwa kama visawe, maneno haya yote yanaonyesha mshikamano.

Mshikamano wa kimsamiati ulijitokeza pia katika data ya matini C, kwa mfano:

5. *Afisa wa elimu alipofika pale, binti aliposimama, akamwangalia, Jinsi alivyotabasamu, jinsi anavyoongea Oh afisa akasema eh- ndio maana...*
6. *Mungu si Athuman, kwetu anasema alipokua mtoto yule akasoma na akamaliza, form four akachaguliwa kujiunga na chuo kimoja cha Business college Dar-*

*es salaam. Amekwenda kule, mama yuko Dar, hamjui mtoto, ali.. alimwona siku nyingi.*

Katika mifano hii ,mfano (5) unatuonyesha mshikamano wa kimsamiati kupitia kurudiwa kwa *afisa* Sehemu hii ya matini haingekuwa na mshikamano ikiwa neno hili (afisa) halikurudiwa kwa sababu ingefasirika kama ni binti aliyeyasema maneno haya. Katika mfano (6) neno *Dar* ingawa ni ufupisho wa Dar es-salam ndilo linaloleta mshikamano. Hivyo, katika kurudiwa kwake msikilizaji anaelewa kuwa anayezungumza anaongea juu ya mahali pamoja.

Data ya matini D kadhalika ilionyesha mshikamano wa kimsamiati,kwa mfano;

7. *Baraka hizi ambazo tumesoma zimeandikwa, kama Biblia yako imeandikwa hivyo kama tumesoma hizo baraka ni zako, na ukiangaliasijui ni wangapi wako na hizo baraka, ambazo tumesoma hapa.*
8. *Na Mungu atakubariki- kwa hivyo leo ni siku ambayo Bwana anatakakubariki. Siku ya leo Bwana angetakaka abariki kanisa, tuweze kuhubiria watu.*

Katika mfano (7) neno 'baraka' limerudiwa mara mbili katika sehemu hii ya matini. Kurudiwa kwa neno hili kunaleta mshikamano. Katika mfano (8) neno Bwana limetumiwa kama kisawe cha jina Mungu. Neno hili vile vile linaleta mshikamano katika sehemu hii ya matini

Kulingana na mifano (1-8) iliyotolewa, tumeona kuwa mshikamano wa kimsamiati haujitokezi kwa sababu kuna kipashio cha kileksia ambacho kimejitokeza. Halliday na Hasan (1976:288) wanatwambia kuwa, kila kipashio cha kileksia kinaweza kuwa na uhusiano wa kimshikamano. Hata hivyo, kipashio hiki kikiwa pekee hakionyeshi kama kina jukumu la mshikamano au la.

Mshikamano wa kimsamiati ndio uliojitokeza kwa wingi kuliko aina nyingine yoyote katika lugha hii ya mahubiri. Katika matini A, tulikuwa na matukio (47) , matini B matukio (135), matini C matukio (80) na matini D matukio (90). Mshikamano wa kimsamiati ulidhihirika katika matumizi ya urudiaji. Matumizi ya visawe pia yalidhihirika.

Mshikamano wa kimsamiati ni muhimu katika kuunganisha vipande kadhaa vya usemi. Vilevile, mshikamano wa kimsamiati huweza kuonyesha mada inayozungumziwa.

#### **4.4 Hitimisho**

Tumechunguza mshikamano katika lugha ya mahubiri katika sura hii. Tumeona kuwa kwa kiwango kikubwa lugha hii ina mshikamano. Tumeangalia aina za mshikamano kama vile urejeshi, ubadilishaji, udondoshi, uunganishi na msamiati. Mshikamano wa kimsamiati na urejeshi ndio uliotumika sana ukilinganishwa na aina zingine za mshikamano. Tunapoangalia mshikamano wa kimsamiati tunapata kuwa kuna maneno mengi yanayorudiwarudiwa na mengine yanatumiwa kama visawe. Haya yote ni muhimu

katika usemi. Hivyo maneno kama ‘Mungu’, ‘Yesu Kristo’, ‘Biblia’, ‘Bwana’, ‘Watakatifu’, ‘Manabii’ yametumika kuleta ushikamano wa kimsamiati. Tunaweza kusema kuwa kutajwa kwa maneno haya na hasa kurudiwa kwake hutambulisha sajili ya dini mbali na mshikamano.

Ingawa mahubiri yaliyotolewa na wahubiri hayakuwa na urefu sawa, kwa kiasi kikubwa yote yalikuwa marefu. Urefu huu wa mahubiri uliwezesha urejeshi kama aina ya mshikamano kutumika sana. Hii ni kwa sababu mhubiri anaposema jambo, anapolirejelea baadaye hawezi kutumia jina lile lile la kwanza kila wakati. Na ikiwa angefanya hivyo, basi usemi wake ungekuwa na matatizo ya kufasiriwa.

Kuhusu ubadilishaji na udondoshi, tunapata kuwa huu ni mfanyiko mmoja katika lugha ukijitokeza kwa njia tofauti. Aina hizi za mshikamano zinatumiwa ili kupunguza utumizi wa maneno mengi.

Uunganishi ni aina ya mshikamano iliyotumika kwa kiasi kikubwa katika lugha ya mahubiri. Katika aina hii ya mshikamano, sio lazima neno liwe kiunganishi (kama tunavyoelewa viunganishi). Matumizi ya maneno kama ‘kwanza’, ‘sasa’, ‘mara ya kwanza’ yalitumika kama viunganishi ili kuleta mshikamano.

Kwa jumla tunaweza kusema kuwa hakuna mipaka dhahiri kati ya aina hizi za mshikamano. Kwa mfano tukirejelea matini B katika mfano (4) (sehemu 4.3.4), tunapata msamiati kama ‘Masiha’, ‘Mwokozi’ na ‘Mkombozi’ ukitumika kama visawe. Tunaweza

pia kusema 'Mwokozi' na 'Mkombozi' ni vibadala vya Masiha. Haya yanaoana na madai ya Halliday na Hasan (1976:279) wanaposema;

Hivyo, mipaka kati ya mshikamano wa kimsamiati hasa ule wa kurudia na wa kisarufi wa urejeshi si dhahiri.(TY)

Vilevile, mipaka kati ya udondoshi na ubadilishaji haiwezi kutanganishwa kujulikana kwa udhahiri. Tunapochunguza matini hizi za mahubiri tunapata kuwa mifano yake ni michache sana. Tunaweza kusema basi kuwa katika lugha ya Kiswahili aina hizi hazijitokezi waziwazi.

Tunapochunguza mshikamano katika matini hizi, tunagundua kuwa hata ingawa vipashio vya mshikamano vinajitokeza, kuna matatizo ya matumizi ya lugha. Hivyo kuna matini zingine ambazo zina mshikamano kuliko zingine. Kwa mfano matini B ina mshikamano zaidi kuliko zingine. Matini A inafuata matini B, halafu matini C. Matini D ndio ya mwisho katika ulinganisho huu. Tulipochunguza sababu za jambo hili, tulipata kuwa lilitokana na na asili za matini. Katika uchunguzi wetu tuligundua kuwa waliotoa mahubiri ya matini B, A na C ni wahubiri waliopata mafunzo ya hali ya juu kuhusu kuhubiri. Mhubiri aliyetoa mahubiri ya matini D hakuwa amepata mafunzo ya kuhubiri na kiwango chake cha elimu hakikuwa cha juu.

Kutokana na utafiti huu ni dhahiri kwamba matumizi ya lugha ambayo yana mshikamano hutegemea mtoaji. Haya ni pamoja na mafunzo aliyopata kuhusu kuhubiri na pia kiwango



## SURA YA TANO

### 5.0 HITIMISHO

#### 5.1 Malengo Na Matokeo Ya Utafiti

Lengo kuu katika utafiti huu ilikuwa ni kutafuta sifa bainifu katika lugha ya mahubiri hasa inapowasilishwa katika lugha ya Kiswahili. Utafiti ulichanganua data kutoka mashariki mwa Nairobi katika mtaa wa Kaloleni na Bahati. Malengo makuu ya utafiti huu yalikuwa kukusanya data, kutambua sifa zake bainifu na kuzichanganua kiisimu. Sifa bainifu zilizopatikana zilitambuliwa kutokana na ruwaza ambazo zilikuwa katika matini zote. Utafiti huu ulitumia nadharia ya uamilifu wa lugha hasa mtazamo wa kimtindo na wa mshikamano.

Data ya uchanganuzi ilipatikana kutoka makanisa manne ambayo ni; Katoliki, Anglikana, Seventh Day Adventist na Gospel Reedemed Church. Hivyo, mahubiri manne yalichanganuliwa, moja kutoka kila kanisa kwa kutumia mitazamo miwili katika nadharia ya uamilifu wa lugha. Mtazamo wa kimtindo (Crystal na Davy 1969) na mtazamo wa mshikamano (Halliday na Hasan 1976) ndiyo iliyotumika.

Data ilionyesha kuwa kuna ruwaza zilizotanda katika kila matini ambazo zilifanana. Ruwaza hizi ndizo zilibainisha sifa bainifu za lugha hii. Mahubiri yote yalikuwa na mianzo ambayo ilikuwa aina ya maamkuzi. Ruwaza hii ilikuwa na majukumu matatu: kuonyesha wahubiri kuwa wako na msingi mmoja, kuwaleta waumini karibu na mhubiri, na kupunguza urasmi katika lugha ya mahubiri. Vilevile katika mianzo hii, wahubiri

walitaja dhamira ya mahubiri yao. Kwa kufanya hivi, wahubiri walidhamiria kuweka mipaka ya ujumbe waliotarajia kuupasha.

Kulikuwepo pia na ruwaza za kuendeleza ujumbe wa mahubiri. Hizi ni pamoja na matumizi ya maswali, kuchanganya msimbo, matumizi ya mifano kuelezea na kufafanulia ujumbe, takriri, matumizi ya ishara na matumizi ya sauti. Kila mojawapo ya ruwaza hizi ilikuwa na jukumu fulani. Utafiti ulibainisha aina mbalimbali za matumizi ya maswali. Kuna maswali ya balagha ambayo yalitumiwa kama sihi kwa waumini kuwa washiriki katika kufikiria. Kulikuwepo na maswali ya kuwatahadhrisha waumini kuwa makini; Wahubiri walitumia aina hii ya maswali ili kuwavutia waumini kusikiliza kwa muda mrefu. Wahubiri pia walitumia maswali ya kutaka waumini wajitathmini, hii ikiwa ni sehemu muhimu sana katika mahubiri.

Katika kuendeleza ujumbe, data ilionyesha matumizi ya kuchanganya msimbo. Katika ruwaza hii, aina tatu za kuchanganya msimbo zilijitokeza. Kuchanganya msimbo kati na miongoni mwa sentensi ndiko kulikojitokeza kwa wingi kuliko uambatishaji wa kiungo. Lugha zilizochanganywa ni Kiswahili na Kiingereza. Uambatishaji wa kiungo kama aina ya kuchanganya msimbo ulipatikana mahala ambapo wahubiri walikosa kupata moja kwa moja kisawe cha neno katika lugha ya Kiswahili. Kuchanganya msimbo kati ya sentensi kwa kiwango kikubwa kulitumika wakati lugha mbili zilizochanganywa zilingiliana sana katika sheria zake za uundaji wa sentensi. Hili ni jambo lililodhihirisha kuwa wahubiri wana uwezo wa kutumia lugha zote mbili kikamilifu. Wahubiri walitumia lugha ya Kiingereza mahali walipohisi kuwa dhana itaeleweka vizuri katika lugha ya Kiingereza.

Wahubiri pia walitumia mifano iwe ya visa au matukio yaliyotokea kuelezea ujumbe wao. Hili lilifanywa kwa nia ya kurahisisha kueleweka kwa ujumbe.

Matumizi ya sauti na takriri pia yalitumika. Katika matumizi ya sauti, wahubiri kwa mfano, walikaa kimya ili kufanya maana ya walichowakilisha izame, na pia wakati wa kutafuta jambo la kusema. Takriri ilitumiwa kwa nia ya kusisitiza.

Mahubiri pia yalikuwa na miisho yake. Kabla ya wahubiri kukamilisha mahubiri yao, walionyesha au waliashiria kuwa wanahitimisha. Walifanya hivi kwa kutumia maneno fulani pamoja na kuongea kwa sauti ya chini. Hii ilikuwa pia njia moja ya kuondoa uchovu na kuwafanya waumini wawe makini mpaka mwisho wa mahubiri. Mwisho kabisa, wahubiri walitamatisha mahubiri yao kwa maneno fulani. Kwa mfano,- “Na Bwana awabariki. Tuombe.”, “Tusimame”, “Mungu na awabariki. Tuombe” na “Funga macho tuombe”. Miisho ya mahubiri ilionyesha kuwa mazungumzo yana mipaka na mipaka hii huonyeshwa kwa njia tofauti.

Sifa nyingine bainifu iliyojitokeza ni mshikamano. Mshikamano katika lugha ya dini ya Kiswahili ulijitokeza kwa njia mbalimbali. Kati ya njia mbalimbali zilizodhihirisha mshikamano katika lugha hiyo ni msamiati. Utafiti huu ulidhihirisha njia mbalimbali zinazotumika ambapo ama msamiati ule ule unarudiwa au mwingine badalia unatumiwa.

Njia ya pili iliyotumika sana katika kuleta mshikamano ni urejeshi. Urejeshi ulikuwa wa aina mbili; wa kieksofora na wa kiendofora. Katika urejeshi wa kiendofora, aina ya

kianafora ilitumika zaidi ikilinganishwa na ya kikatafora. Katika aina hii ya mshikamano, kulikuwa na matumizi ya viambishi.

Uunganishi ni aina nyingine ya mshikamano iliyotumika kwa wingi. Utafiti ulionyesha kuwa hata maneno ambayo kawaida hayatumiki kama viunganishi kwa mfano “kwanza”, “sasa”... yalitumika. Kama Faircough (1989:131) anavyosema, mifano ya uunganishi huonyesha kuwa uhusiano wa vihusishi ambao unachukuliwa kuwa wa kawaida unaweza kuwa dhana iliyofichika. Hata hivyo, uhusiano kama huu sio lazima uwe na viunganishi; unaweza kuwa umekusudiwa tu katika muoano wa sentensi.

Ubadilishaji na udondoshi ni aina za mshikamano ambazo hazikutokea sana katika utafiti huu. Kutokana na uchache wa mifano, yake tulipata kuwa aina hizi hazijitokezi waziwazi katika lugha ya dini ya Kiswahili.

Aina hizi za mshikamano, zinazotumika kwa pamoja katika matini zinategemeana na kuiunganisha matini. Mawazo haya yanaendelezwa na Loveday (1983:182) anaposema kuwa lugha huwa imefumana. Ili kuhakikisha kuwa kuna mshikamano, lugha hufuiliza kwa kurudiarudia, kutumia vibadala na kudondoa.

Katika uchunguzi huu ilidhihirika pia kuwa kuna ubinafsi unaodhihirika katika lugha ya mahubiri. Ubinafsi huu, huathiri kutegemeana kwa aina hizi za mshikamano. Kwa hivyo, ili matini ya mahubiri iumane kabisa, sharti itumie aina hizi za mshikamano vilivyo.

Ingawa mshikamano ulionyeshwa katika kila mahubiri, kuoana vizuri kwa mahubiri hayo kulitegemea ufundi wa mhubiri mwenyewe. Haya yanatuelekeza kwenye kauli kuwa ingawa lugha ya mahubiri ina njia zake za kuleta mshikamano, kuna pia hoja ya upekee au ubinafsi wa mhubiri, katika matumizi ya lugha. Kwa mfano, matumizi ya neno “na” katika matini A na “B” yanaonyesha ubinafsi na si uunganishi. Katika matini C, mhubiri alitumia maneno kama “yah”, “oh”, “eh” na “ah” kuonyesha upekee wake. Neno “basi” katika matini D lililotumiwa mara nyingi lilionyesha upekee wake. Hivyo, maneno kama haya hayakutumiwa kufuatia nguvu za mshikamano bali yanatumiwa kufuatia mazoea ya mhubiri.

## **5.2 Mapendekezo**

Utafiti huu umeangalia sifa bainifu za lugha ya mahubiri kwa kijumla. Baadhi ya sifa hizi bainifu kama matumizi ya sauti ni eneo ambalo lingefanyiwa utafiti kwa undani. Vipengele vya kiarudhi kama kiimbo (lafudhi), mkazo na tempo vinaweza kufanyiwa utafiti. Pia, kuna uwezekano kuwa kiimbo kinapotumiwa kama kipengele cha matumizi ya lugha kinaweza kusababisha mshikamano hasa wa kimaana. Utafiti pia unaweza kufanywa ili kuchunguza matumizi ya ishara katika katika usemi. Utafiti huu pia haukugusia kipengele cha muwala ambacho kinaenda sambamba na mshikamano. Hivyo, ni vizuri ikiwa utafiti wa kuchunguza muwala (mshikamano ukiwa sehemu mojawapo) utafanywa.

Utafiti uliofanywa ulishirikisha eneo la mji. Utafiti mwingine unaoshirikisha maeneo yasio ya mji unaweza kufanywa kwa nia ya kufanya ulinganisho wa matokeo. Hali

kadhalika, utafiti huu ulishughulikia makanisa makuu na kuna mahubiri ambayo yanaendelezwa kwa mitaa. Utafiti wa mahubiri kama haya ambapo hadhira ni ya kuingia na kutoka unaweza kufanywa ili kuchunguza lugha inatumiwa vipi.

Altes, H (1981). *The Art of Biblical Narrative*. New York: Basic Books Publishers.

Utafiti mwingine unaoweza kufanywa ni wa ulinganisho wa matumizi ya lugha kati ya wahubiri wanaume na wanawake. Aidha, utafiti huu unaweza kufanywa kwa kutumia nadharia zingine.

Swickhard, J. "Studies of the African Mother." *African Studies Language & Society* 15 (pp. 331-342)

Brown, H.C et al (1963). *Steps to Sermon: A Plan for sermon preparation*, Nashville: TN Broadman Press.

Brown, G and Yule, G. (1983) *Discourse analysis*. Cambridge: Cambridge University Press.

Brown, P&Levinson, S (1978). "Universals of Language Usage: Politeness Phenomenon" In Gooly, E.N. *Questions and Politeness Strategies in Social Interactions* (pp. 116-134) Cambridge: Cambridge University Press.

Coakley, M (1981). *An Introduction to Discourse Analysis*. London: Longman.

Goodman, (1969). *A Liturgical Language to a Christian Perspective*. London: New Black Press.

Gylden, D (1985). *Linguistics, Language and Religion*. London: Burns & Oates.

Graddol, P and Leech, G. (1999). *Reconfiguring English Style*. New York: Longman.

## MAREJELEO

- Alter, R (1981). **The Art of Biblical Narrative**. New York: Basic Books Publishers.
- Berk-Seligson, S. (1986). "Linguistic Constraints on intersentential code Switching: A study of Spanish/Hebrew Bilingualism" In **Language & Society** 15 (pp. 331-348)
- Brown, H.C et al (1963 ). **Steps to Sermon : A Plan for sermon preparation**. Nashville: TN Broadman Press.
- Brown, G and Yule G, (1983). **Discourse analysis** .Cambridge: Cambridge University Press.
- Brown, P & Levinson, S (1978). "Universals of Language Usage: Politeness Phenomenon" In Goody, E.N **Question and Politeness: Strategies in Social Interactions**. (pp. 106-134) Cambridge: Cambridge University Press.
- Courthard, M (1981). **An introduction to Discourse Analysis**. London: Longman.
- \_\_\_\_\_ (1964) **A Liturgical Language in a Christian Perspective**. London: New Black Friars.
- Crystal, D (1965). **Linguistics, Language and Religion**. London: Burns & Oates.
- Crystal, D and Davy, D (1969). **Investigating English Style**. New York: Longman.

- Darbyshire, A. (1971). **A Grammar of Style**. London: Tonbridge Printers.
- Devito, A. (1987). **The Elements of Public Speaking**. Cambridge: Harper & Row Publishers.
- Dijk, T. (1977). **Text and Context**. New York : Longman.
- Dressler, W and Beaugrande (1981). **Introduction To Text Linguistics**. New York: Longman.
- Faircough, N (1989). **Language and Power**. London: Longman.
- Fasold, R (1984). **The Sociolinguistics of Society**. Oxford: Basil Blackwell.
- Ferguson, C. (1972). "Diaglossia" Giglioli, P. **Language and Context**. (pp.232- 251) Harmondsworth: Cox & Wyman Ltd.
- Gachinu, J (1996). "Linguistic Aspects of Code-switching in Gikuyu, Kiswahili and English." M.A Thesis Kenyatta University. (Unpublished)
- Gregory, M & Carroll, S (1978). **Language and Situation: Language Varieties and their Social Context**. London: Routledge and Kegan Paul.
- Goody, E.N (1978). "Towards a Theory of Questions." Goody, E. N **Questions and Politeness: Strategies in Social interactions**. (pp. 17-43). Cambridge: Cambridge University Press.
- Grice, P (1975). "Logic and Conversation". P.Cole & J.Morgan (eds.) **Syntax and Semantics**. New York: Academic Press.
- Gurmpertz, J (1982). **Discourse Strategies**. Cambridge: Cambridge University Press.

Gumperz, J & Hymes, D (1972). **Directions in Sociolinguistics: The Ethnography of Communication**. Oxford: Basil Blackwell.

Habwe, J. H (1989). "Elements of Pragmatic Discourse among the Mvita people." M.A Thesis University of Nairobi (Unpublished)

\_\_\_\_\_ (1999). "Discourse Analysis in Swahili Political Speeches" .Phd Thesis University of Nairobi (Unpublished)

Halliday, M.A.K et al (1964). **The Linguistic Science and Language Teaching**. London: Longman.

Halliday, M and Hasan, R (1976). **Cohesion in English**. London : Edward Arnold

Halliday, M.A.K (1971). "Linguistic Function and Literary Style: An Inquiry of William Goldings "The Inheritors". Chartman, S(ed.) **Literary Style: A Symposium**. (pp.330-360). London: Oxford University Press.

\_\_\_\_\_ (1973). **Explorations in the Functions of Language**. London: Edward Arnold.

\_\_\_\_\_ (1985a ). "Dimensions of Discourse Analysis Grammar". Dijk, T.V(ed.) **A Handbook of Discourse Analysis**. (pp.29-56). London: Academic Press volume 2 .

\_\_\_\_\_ (1985b ). **An Introduction to Functional Grammar**. New York: Edward Arnold.

Kapinga, M.C (1983). **Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu**. Dar es Salam: TUKI.

- Kiai, A.W (1996). "A Discourse Analysis of Education Radio Programs to Farmers Adaptation Register". M.A Thesis. University of Nairobi (Unpublished)
- Kitsao, J (1975). "A Stylistic Approach Adopted for the study of written Swahili Prose Texts" M.A Thesis University. of Nairobi (Unpublished).
- \_\_\_\_\_ (1982). "An investigation of Themes in Swahili Literature. An Application of Stylostatistics to chosen texts". Phd. Thesis University of Nairobi. (Unpublished).
- Leech, G (1969). **A Linguistic Guide to Poetry**. London: Longman.
- Leech, G, N and Short M (1981). **Style in fiction**. Burnt Mill: Longman.
- Loveday, L (1983). "Rhetoric Patterns in Conflict: The Social Cultural Relativity of Discourse Organising Processes." **Journal of Pragmatics** vol. 7. (pp. 169-190).
- Lyons, J (1977). **Semantics, vol 1&2** London: Cambridge University Press.
- Mgullu, R (1999). **Mtalaa wa Isimu:Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili**. Nairobi: Longhorn.
- Michira, J. N (1993). "Uchanganuzi wa Kimtindo wa Lugha ya Wachuuzi na Lugha ya Matangazo ya Biashara redioni." Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi(Haijachapishwa).
- Milroy, L (1987). **Observing and Analysing Natural Language**. New York: Basil Blackwell.

Njue , J.G (1989). "Muala Katika Kiswahili:Umuhimu wake Katika Uchambuzi wa Ngano za Waswahili" Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachpishwa).

Parkin, D.J (1974) "Status Factors in Language Adding: Bahati Housing Estate in Nairobi." Whiteley, W.H **Language in Kenya**. (pp.147-165). Nairobi: Oxford University Press.

---

Language Shift and Ethnicity in Nairobi: The Speech Community of Kaloleni." Whiteley, W.H **Language in Kenya**. (pp.167-187). Nairobi: Oxford University Press.

Pfaff, C.W (1979). "Constraints in Language Mixing." **Language** 55. (pp. 291-318)

Pratt, M (1977). **Towards A speech Theory of Literary Discourse**. Bloomington: Indiana University Press.

Poplack, S (1980). "Sometimes I will start a Sentence in Spanish y termino en Espanol": Toward a typology of code switching. **Linguistics** 18. (pp. 581-618).

Rayfields, L. (1970). **The Language of a Bilingual Community**. Mouton: The Hague.

Richards, J et al (1985). **A Longman Dictionary of Applied Linguistics**. London: Longman.

Romaine, S (1989). **Bilingualism**. Oxford: Basil Blackwell.

Saville-Troike, M (1989). **The Ethnography of Communication: An Introduction**. Oxford: Basil Blackwell.

- Smith, F (1993). "The Pulpit and Womans Place: Gender and The Framing of The Exegetical Self in Sermon Performances". Tannen D (ed.) **Framing Discourse**.(pp.146-173). Oxford: Oxford University Press.
- Stubbs, M (1983). **Discourse Analysis**. Oxford: Basil Blackwell.
- Tannen, D (1984) **Conversational Style**. New Jersey: Ablex Publishing Cooperation.
- \_\_\_\_\_ (1986). **Talking Voices: Repetition, Dialogue, and Imagery in Conversational Discourse**. Cambridge: Cambridge University Press.
- Turk, C (1985). **Effective Speaking**. London: Chapman & Hall.
- Watts, N (1989). **Language and Communication**. Oxford: Oxford University Press.
- Werth, P (1984). **Focus, Coherence and Emphasis**. Sydney: Croom Helm.
- Widdowson, H.G (1977). **Teaching Language as Communication**. London : Oxford University Press.
- Williams, J.M (1979). **Style: Towards Clarity and Grace**. Chicago and London: The University of Chicago Press.

## KIAMBATISHO I

### MATINI A

#### MAHUBIRI : KANISA LA KIANGLIKANA -KALOLENI

Mhubiri: Habari zenu?

Waumini: Mzuri

Mhubiri: Bwana asifiwe?

Waumini: Amen.

Mhubiri: 1. Bwana ni mwema asubuhi njema, kwa kunipatia nafasi ili tuseemezane pamoja. 2. Ebu mwangalie mwenzako aliye karibu nawe, mwambie Mungu anakupenda na mimi ndugu yangu.

Waumini: 3. (Mungu anakupenda na mimi ndugu yangu).

Mhubiri: 4. Bwana asifiwe sana

Waumini: Amen

Mhubiri: 5. Kile kinanifanya niseme kwamba nakupenda, neno langu asubuhi ya leo lahusu upendo. 6. Na kabla niendeleo na mahubiri, ningependa kusema tuko pamoja na mke wangu na watoto wangu na dadangu, na ningependa waamke tu, wamsalimie kwa kumpigia mkono juu. (makofi kutoka kwa waumini)

Mhubiri: 7. Bwana asifiwe sana

Waumini: Amen

Mhubiri: 8. Basi, hii ni kalenda, ya Anglikana, kweli imetuletea masomo ambayo yako muhimu sana hasa katika mwaka huu mpya. 9. Na masomo yake tumesomewa, yako na uhusiano sana na (kimya) mtumishi ambao Isaiah alisema atakuja. 10. Na tukigundua vilivyo, hii ni Jumapili ya kwanza tangu udhihirisho wa Kristo Yesu. 11. Na kabla niendeleo sana ku... kufafanua zaidi ya hayo, ningese..nge-taka kusema (kimya) upendo ndio nguzo ya familia yetu. 12. Kwanzia mtoto, kwenda mama, kufika mzee. 13. Na kwa nini nasema namna hiyo? 14. Nikiangalia upande wangu wa kushoto pale naona watoto wako pale, nikiangalia huku kwa viti, ninaona familia imeyakilishwa vilivyo. 15. Na Bibilia inatwambia somo lile tuli... tulilosomelwa-somewa la Isaiah, alikuwa anaongea juu ya familia ya Israeli. 16. Na tukaona anaongea mambo ya mtumishi ambao atakuja. 17. Lakini kabla mtumishi aje, tutaanza kuangalia, kwa nini mtumishi anaingia? 18. Tunaona Mungu, akawapenda wana Israeli tangu jadi, tangu pale Ibrahimu, Yakobo na Isaka. 19. Tukaona akifuatana nao kule Misri, akafuatana nao kule jangwani, akawafundisha mpaka ah... nchi ya ahadi. 20. Na wakati walipofika nchi ya ahadi, kule mambo yakawa mengi, ambayo iliwatoa katika mapenzi na maagizo ya Mungu. 21. Na ikawa watapata shida sana. 22. Na tukasikia mara ya kwanza hawa watu wakabebwa na Assyria, wakachukuliwa wakapelekwa mateka. 23. Na wakati huu, nabii Isaiah anaongea ni kuwaambia hawa watu, tunasikia msitari wa saba, ukisikia hawa watu walikuwa wako na shida kubwa, na kwa sababu tayari walikuwa wameshikwa mateka na wababiloni. 24. Nataka kumaanisha nini? 25. Nataka kumaanisha ya kwamba, wana Israeli walikuwa katika hali ambayo walikuwa wanataka mtumishi ambaye tunaambiwa atakuja awafungue macho, atakuja awatoe gerezani, ambao wamefungiwa . 26. Basi, ikawa ni unabii, utatoka kwa Mungu, na huo unabii utatoka kwa mungu huwa ni unabii unaweza

kuwa na mara mbili. **27.** Mara ya kwanza kuna unabii unatendeka wakati ule ule, na wa pili, ni yule, ni ungetendeka siku baadaye. **28.** Nataka, huu unabii unaendelea hapa ni unabii wa wana Israeli ambao wa.. wa, unabii wa... wa ar.. arobaini na mbili wa Isaiah unaanza na kusema. Tazama mtumishi wangu nimeemtengenezea, mteule wangu ambaye nafsi yangu imependezwa naye. **29.** Bwana asifiwe sana

Waumini: Amen.

**Mhubiri: 30.** Basi ni kuonyesha ya kwamba, Mungu alikuwa na upendo. **31.** Ili akatoa mwanao haje hafe msalabani ili tupate wokovu, ili tupate kukombolewa, ili tuweze kuwa katika hali ya uzuri, kwa sababu tuko na njia moja ama nyingine katika taabu. **32.** Vile wana wa Israeli walikuwa na taabu nyingi kwa sababu tunajua mtu ambaye ameshikwa mateka, hajiwezi kamwe. **33.** Mtu ametekwa mateka, hajui njia aendako, hafanyi kile atakacho, lakini anaendelea kudhulumiwa. Na anaendelea kuwa katika hali mbaya. **34.** Lakini Yesu, akatumwa na Mungu akiwa pale juu mbinguni, aendeleze ule unabii, Isaiah tayari alisema utakuja kutendeka. **35.** Na siku ya leo wadugu na wadada, na watoto wenzetu, leo ninaweza kuangalia nikaona kweli, tunaenda kuwa na njia moja au nyingine, tuko katika hali ile wana wa Israeli walikuwa. **36.** Ukiwa mtoto, umefanya mtihani wa kidato cha... (kimya) eh...eh standard eight mwaka uliopita, tumesikia mtihani umetoka, lakini kwa kuchangisha, au kutufanya sisi tuanze kuuliza, shida hii ni nini? **37.** Tunasika elfu eh.. eh watu mia mbili sitini elfu hawatapa kidato cha kwanza. **38.**Sasa watoto wanaanza kuyumba, wanaanza kujiulisha, kujiuliza, hii shida imeanza kutokea, niko mmoja wao au niko wapi? **39.** Ebu aangalia mama pale ameketi siku ya leo. **40.** Amesikia lazima aje aambie Mungu, niko na shida ama moja ama nyingine, ile ambayo mimi mwenyewe nimeanza kuyafikilia, kuwaza na kuwazua, na sijiwezi. **41.**

Ndio umekuja umeketi hapo, umekuja. Mwingine amekuja kusema ahsante kwa upendo wako. **42.** Mwingine amekuja kwa sababu anaona nyumba yake uchumi kweli umezorota. **43.** Mtakubaliana nami wakina mama. Kila wakati ni kufikiri kuhusu kununua unga. **44.** Ilikuwa shilingi ngapi? Sijui unga ni pesa ngapi na siku hizi, kila... kila mama analia, akifika kule ni kulia, kwa sababu hata uchumi umepita wakina, wakina baba wetu. **45.** Si hiyo peke yake, nikiangalia mzee wa siku hizi, ako na shida kubwa. **46.** Yeye mwenyewe akiangalia anashindwa ataanza njia wapi, atapita wapi kwa familia hii. **47.** Yeye anauliza, na inaweza kufika wakati mmoja jina langu lingie kwa computer ya Retrenchment? **48.** Anaanza kujiuliza hayo. Anaanza kuyumba, anaanza kusikia kweli... He is not stable in his working place. **49.** Kwa sababu gani? Hajui litatokea nini aende retirement! Na ni ya lazima. **50.** Mtakubaliana na mimi ule unabii wa Isaiah umeanza kufika. Ya kwamba, walikuwa na shinda. **51.** Nitasoma msitari wa saba, msitari wa sita inasema, "mimi Bwana nimekuita katika haki, nami nitakushika mkono, na kukulinda na kukutwaa uwe agano la watu na nuru ya mataifa". **52.** Msitari wa saba ambao unasema msikie, "huyafungua macho ya vipo... vipofu, kuwatoa gerezani waliofungwa, kuwatoa wale walioketi vitani katika nyumba ya kufungwa." **53.** Nataka kukwambia wewe ukimaliza form four, wewe umemaliza masomo yako, ya kwamba, umepiga rami mpaka kiatu kikiangaliwa chini unaanza ku... kujiuliza kazi itapatikana wapi. **54.** Mpaka saa hizi kila mmoja yule anatafuta ataanza wapi, anzie wapi amalizie wapi, anashindwa. **55.** Lakini ndugu na dada siku ya leo, wewe mtoto unasikitika, wewe mtoto unauliza, unafungua shule kesho, mama ataweza kupata fedha ya kuninulia kitabu, ataweza kupata fedha ya kuninulia uniform. **56.** Niko na unabii siku ya leo, na ni unabii wa Mungu ambaye anasema, upendo uwe kwako. Bwana asifiwe sana.

Waumini: Amen.

Mhubiri: **57.** Amekuonyesha njia maana umepita. Unabii ni kwamba – aambia mwenzako kwamba... niko na njia, wewe uko na njia?

Waumini: (Niko na njia, wewe una njia?)

Mhubiri: **58.** Kwa sababu gani? Kwa sababu Mungu yuko pamoja nawe. Mungu atakuonyesha mahali utapitia. **59.** Kwa hivyo, kila ukifikiria wewe, ukiangalia mzigo wako haujiwezi. **60.** Kumbuka ya kwamba Mungu hayuko mbali na wewe. **61.** Mungu anabariki wale ambao wako karibu nawe, wako karibu na wao. **62.** Niko na unabii ya kwamba mtumishi Yesu, atakuja akutoe machozi, yaani wewe unalia atakuja akupatie wokovu wa bure, anakuja, kujeni tusemezane. **63.** Hata kama dhambi zako ziko nyekundu namna gani, nitakusafisha. **64.** Kwa hivyo, ndugu umeketi hapa, dada hapo ulipo, kumbuka ya kwamba, huu Mungu ako pamoja nawe. **65.** Na ukienda siku ya leo, nenda ukisema, Bwana asifiwe kwa sababu, leo tumepata upendo kutoka kwa Mungu. **66.** Na Bwana awabariki. **67.** Na tuombe.

## **MATINI B**

### **MAHUBIRI: KANISA LA KIKATOLIKI – KALOLENI**

**Mhubiri:Uje roho mtakatifu.**

Waumini: Uje kwa njia ya Maria.

**Mhubiri: Mungu ni mwema.**

Waumini:Kila wakati.

Mhubiri : Kila wakati

Waumini: Mungu ni mwema.

1. Ni siku ya kwanza ya mwaka, ambapo sisi wakristu ni vizuri tuendeleo kushukuru Mungu kwa siku hizo saba- 01, mwaka mpya, na mambo mapya yatategemea individual, yatategemea wewe haitegemei sisi katika ule upya. 2. Na kwa sababu hata kama ni mwaka mpya amezaliwa, amekuwa sasa ni wa kila mtu, huyu mwokozi aliye-a zaliwa majusi sio wa mayahudi kama vile walivyofikiria, lakini ni wa kila mtu.3. Katika somo letu la kwanza, tunasikia vile nabii Isaiah alivyotabiri akiambia Yerusaremu, amka uandae nuru kwa sababu nuru ilikuwa ianze Yerusalemu.4. Na Yerusalemu ni mji ambao ni mtakatifu mpaka sasa , wa Wayahudi.5. Ni mji ambao walipewa na mwenyezi Mungu walipotoka katika nchi ya Misri. 6.Na wakapewa mji katika Yerusaremu, na wakapewa Waisraeli.7. Na mtu akichezea Israeli, basi anakuwa akichezea utu wa wana wa Israeli. Na ndipo ninapongea bado kuna vita kati ya waisraeli na Palestine, ambapo Wayahudi wanajua tulipewa na mwenyezi Mungu, nani mwingine ambaye anaweza kuja kuwa anatusumbua katika nchi hii? 8. Nabii Isaiah anawaambia hawa wayahudi basi nuru inakuja pale. 9. Na inapofika pale, sio nuru yenu ni ya walimwengu. 10.Na watu watakuwa wakihihi kutoka mbali wanakuja hapo ili wapate ule utakatifu.11.That holiness

katika Yerusaremu. Na ali... alituandikia hapa akisema wataleta dha... dhahabu pamoja na uvumba. **12.** Na sio tu wa kutoka Yerusaremu, ni wa kutoka nchi ambayo ni mbali.**13** Wameona wale wa kutoka Sheba ya kwamba tutaenda Yerusaremu, kama ilivyo...tabiriwa na nabii Isaiah na tutatoa uvumba, tutatoa dhahabu, kama ishara ya kuonyesha ya kwamba kuna wakati ambako atakuja mfalme mtawala. **14.** Na huyu mtawala, hatatoka katika kabila eh kabila ambayo ni kuu, anatoka kabila lile ndogo, lile la Yuda, ambapo mtawala atatoka hapo. **15.** Katika utabiri wa huyu nabii, Isaiah na pia naye anasema, katika muda wa kuonekana nyota basi itaonekana palepale. **16.** Kwa mtakatifu Mathayo ambaye anatuambia sio kama story. **17.** It is a historical fact ambapo hawa manabii na mamajusi walikuwepo.**18.** Kwa hivyo wakristo somo letu la kwanza linataka kutwambia nini wayahudi wa sasa, wakristu wa kisasa? Ya kwamba huyu ambaye amezaliwa anatoka katika “mbari” ya Yuda, na ni mtawala. **19.** Na sio tu wa Wayahudi, hata sisi ni Mungu wetu. **20.** Na ni Mungu wa kila mtu. He is not a situational God. **21.**Ni Mungu wa kila mtu, ambaye anapenda kuona mwanga. **22.** Na kuona mwanga inategemea wewe uko macho namna gani-you cannot be forced.**23.**Huwezi kuambiwa alafu... ni wewe mwenyewe katika roho yako ufungue uone mwanga. **24.** Tusiwe kama Mayahudi ambao walisema Mungu ni wetu, we cannot share our God. **25.** Nabii Isaiah anafafanua katika mwokozi, Masiha ni wa kila mtu. **26.** Mtakatifu Paul, kwa waefeso anawaambia vivyo hivyo. **27.** Ninyi wa... waefeso mna ...ati kwa sababu mimi mtakatifu Paulo niliwahubiria kwamba mwokozi amezaliwa kwenu, mkombozi huyu Yesu Kristu si wenu tu, ni wa kila mtu, ni mkombozi pia wa Galatia, ni mkombozi wa Wakorintho, ni mkombo—zi wa kila mtu, sio ninyi. **28.** Kwa hivyo msijigambe. **29.** Ni lazima mtambue mjifungue muwe na mafikirio ya kuwa Kristu ambaye anahubiriwa na

mimi kama mtakatifu Paulo ni Kristu wa kila mtu. 30. Sijui wakristu tunaweza kuwa na pia wakati mwingine na mafikirio kama hayo. 31. Tukifikiria ya kwamba Mungu aliyezaliwa ni wa wakatoliki tu, salvation is only for catholics, tutakuwa tume -miss the vote. 32. Tutakuwa tuna mafikirio mengine kwa sababu, ukombozi sio tu wa wakatoliki, ukombozi ni wa kila mtu, kwa sababu nuru, ukombozi umefunguliwa kwa wale ambao wana nia njema. For those of good will. 33. Kwa hivyo unaweza kuwa mtakatifu na huna nia nzuri, unaweza kuwa hautaki mwanga, unajitajia tu kwa jina, nitakuwa mimi ni mkatoliki Mungu ni wangu lakini akikwambia ufanye hivi, you share, unashy kutokana na mambo hayo na watu wengine. 34. Wayahudi pia, huu mtakatifu anawaonya ya kwamba ebu tujiangalie kwa sababu huyu Kristu huwa amezaliwa kwa wale ambao wanapenda mema. 35. Na katika desturi ya wayahudi pia, utapata tunapongea huwa wana mambo haya ya kuweka kofia kama ile maaskofu wanaweka kwa kichwa. 36. Kama mtoto akizaliwa baada ya miaka miwili au mitatu already amewekwa kakofia hako kwa kichwa kama myahudi. 37. Hata wakati mwingine hana nywele, lakini hiyo kofia inashikishwa na inataka kuonyesha huyo mtoto, si mtoto wa kawaida, huyo ni mtoto wa uyahudi na ni mtoto ambaye ana urithi .He is of a chosen race.38. Na anapoendelea, hiyo kofia inaendelea akijua ya kwamba, mimi ni myahudi na mimi ni myahudi damu. 39. Tunasikia ya kwamba wayahudi si kama sisi, hawacha... hawachanganyikani-myahudi ni myahudi-period. Hakuna haja ya kuchanganya. Mungu wake ni Mungu wake-period-hana Mungu mwingine ni huyo tu. 40. Kwa hivyo yeye anajua ni mimi tu hakuna mwingine 41 .Kwa sababu Kristu ni wa kila mtu either uweke kofia or you are chosen or you are not chosen, Mungu, ni Mungu wetu, wa kila mtu.42.Either tunapenda au hatupendi Mungu, Mungu anatupenda.The love of God is dynamic, it is not static.Upendo

wa mwenyezi Mungu si wa kusimama, ni upendo ambao unaendelea. 43. Upendo wa Mungu ni wa alfa na omega, haupinduki kabisa, sisi upendo wetu huwa unapinduka lakini wa mwenyezi Mungu haupinduki. 44. Kwa hivyo, hii leo sisi kama wakristu, tunaambiwa Mungu wetu, ambao tunafikiria ni wetu ni Mungu wa kila mtu, na ndipo ni epiphania. 45. Amefungua malimwengu kwa wale ambao wanamtamani, kwa wale ambao wako wanajua ni nani. 46. Ndipo tunaambiwa hata zama za mtakatifu Paulo kulikuwa na hizo siasa ya kwamba ni sisi tu, ni sisi tu. 47. Hata wakati wa nabii Isaiah, walikuwa hivyo tu, sisi tu ni sisi tu, mfalme ni wetu, wale wengine si wao. Are we not doing the same thing today? 48. Maybe Wakikuyu wanataka next time, the president lazima awe Mkikuyu, ati kwa sababu sisi ndio wengi. Next time, lazima Mjaluo awe president, next time, Mkamba awe president, next time, lazima mm Mmeru awe president au lazima awe Mkalenjini. 49. Hakuna wimbo mwingine ambao tunaimba! Five years zimeisha, ni hiyo tu. President, president, president, president! nini? Sisi tu, sisi tu –ndio awajengee barabara?. 50. Wakikuyu wamepata, Wakalenjini wamepata lazima achaguliwe, we need to ask ourselves, katika maisha yetu, tuwe very serious ya kwamba sisi ni taifa moja, it does not matter yule ambaye atakuwa raisi ni nani au MP(Member of parliament) ni nani, kwa sababu sisi ni wa Mungu mmoja. 51. Angalia vile mmekaa, mbona huhisi wewe ni Mkikuyu ama ni Mjaluo au ni Mmeru? Mbona hamhisi hivyo? Kwa sababu mna Mungu mmoja. Mbona hamuulizi padre wetu ni Mkikuyu, next time lazima awe Mjaluo, ah- not in the catholic church. 52. Au tuseme askofu mkuu katika nchi hii ni Mkamba, next time tuchague Mkikuyu,- that is not a catholic church! Yule ambaye anakuja, awe Mjaluo, awe nini ni askofu. 53. Na ndipo kila wakati we make a bladder katika maisha yetu. Wakristu wanataka kusema ni sisi tu, tuchague fulani,

tuchague fulani, hatutaki mtu mwingine.54.And we waste a lot of money tuk.. tukio... tukiongea mambo hayo. 55. Five years gone na ni hiyo tu! 56. KANU(Kenya African National Union-Chama cha Kisiasa) inataka kuungana na NDP(National development Party-Chama cha Kisiasa) – hakuna wimbo mwingine! DP (Democratic Party-Chama cha Kisiasa) naye ni hivyo hivyo tu. 57. Na mbona hamfanyi kanisani hivyo? 58. Tunapokea, ebu father pokesha wa KANU kwa sababu uwape ile kubwa kwa sababu ndio wanatawala na ile kidogo kidogo uwape hawa ambao ni wa DP au...hatusemi hivyo,because we share one God. Lakini sijui ni shetani upi ambao mambo mengine yakija hutukosesha. 59. Tunasahau mambo mengine ambao, ni mambo ambao ni wazi. 60.Tunakumbuka mimi tu kama vile Myahudi alisema ni mimi tu and we cannot share. 61. Ebu tukumbukange hivyo. Either you are out or you are in the church, sisi ni wakristu. Ukabila hauingii kamwe katika swal hilo la mukristu. 62. Kwani unafikiri ati kwa sababu Wakikuyu ni wengi in this government mbinguni watakuwa watakuwa wengi?- that is not the way- au watakatifu weengi watakuwa Wakikuyu ati kwa sababu walikuwa wengi. 63. Au kwa sababu haya, hawa makabila kidogo ni waduni, mbinguni watakuwa wadogo kwa sababu ni waduni-no!It is not the situation. 64. Tuone hiyo nyota na kuifuata .65. Na ndipo mtakatifu huyu Paulo kwa ... kwa Wakolosai anawaambia, tutubu kwa sababu Mungu wetu ni Mungu wa kila mtu. 66. Katika somo letu la Injili linatuakishia nuru, linatuambia, wakristu ambao ukabila, it is not in their mind, hata tunapokuja kupokea sio kwa ukabila,tunapokea Kristu tu, nothing else. 67. Tunaambiwa hawa maya...mamajusi, eh watu ambao wamesoma, wanaenda, kwa mfalme wanamwambia ya kwamba, kumeandaliwa mfalme ebu tuonyeshe kwa sababu you are so informed, wewe ndiwe mfalme, ebu tuonyeshe. 68. Lakini wanafikiri hata yeye kwa

sababu hii ni nchi yake, anajua zaidi. 69. Halafu anaita manabii anawauliza, amezaliwa wapi? Hawakumficha, walimwambia vile iliamuliwa, na vile Isaiah alisema huyo mtoto katika majumba ya Yuda kutatoka mtawala.70.Na hapo ndipo huyo anawambia haya mamajusi, kwanza because I am not sure, hata siwezi kuamini,ebu kwanza muende mukamwone halafu mpitie hapa,hata mimi ninaenda kumsujudia- nitaenda kumpigia magoti nimwombe. Which, which president angefanya hivyo? 71. Hata wale ambao wanatawala asikie kuna president kule Kaloleni aseme nenda mumuone, hata mimi nitakuja ku... kuona -ni nani? 72.Na ndipo Mungu anawaambia hawa mamajusi wapitie kwa njia nyingine, kwa sababu huyu ambaye ana... ana... anafikiriwa anajua mengi anataka kuua huu mtoto.73.Kuna huyu ambaye ni Herode,badala ya kuonyesha wale wengine pahala nyota ipo anawadivert.74.Na tunaambiwa nyota ilipotea, kwa muda huo walikuwa katika Herode. 75. Na walipotaka kuendelea nyota na ikaja ikawaonyesha palepale. 76. Walipoenda palepale, waliona nyota kama ilivyotabiriwa ya Bethlehemu kutazaliwa mtoto. Wametoa manemane, wametoa uvu... uvumba na pia wametoa dhahabu.77. Na katika utamaduni wa wayahudi mtu anapokwambia nimetoa hivyo vitu vitatu kama zawadi,lazima awe mfalme. 78. Anapokwambia nimetoa dhahabu, uvumba na manemane automatically unajua yule ni mfalme na ana heshima. 79. Dhahabu haitolewi watu wa kawaida,uvumba hautolewi watu wa kawaida, hata tunapofanya katika misa kama nitafanya katika hii hekaru,uvumba kama unanukia vizuri sifanyi hivyo nyumbani kwangu, au mahali pengine, there is a special place where tunatumia uvumba. 80.Kuna huyu ambaye amezaliwa,ebu tujiulize leo wakristu wenzangu,wewe nyota ambayo unaifuata kila wakati, ambayo ni Kristu,unaifuataje? 81. Na unapofuata hiyo nyota mahali ambapo unataka katika maisha yako, ukumbuke ya kwamba kuna maherode

ambao watakutoa katika neema ya Mwenyezi Mungu, alafu Yesu Kristu -hujui nyota, hujui kielelezo na mahali Kristu ako. **82.**Na kwa sababu kuna marafiki wako unawaona ambao wanataka kukutoa katika huo uzuri,ili usione mambo yale. **83.**In simple way, in brief, sisi kama wakristu unapofanya mambo mazuri, you have to pay for it. Lazima utalipa. **84.**Wewe kama baba unapofanya mambo mazuri lazima utalipa. **85.** Na utalipa kwa uchungu. Endapo unafanya mambo mazuri ya kutafuta hiyo nyota,katika maisha yako,hakuna shortcut-Lazima utaumia,lazima utalia siku moja, ulipe. **86.** Si hata Yesu alifanya hivyo? Alikuwa kutukomboa na alilipa in hard wa... way. **87.** Kwa hivyo kila mukristu ambaye anafuata ukristu wake, lazima atalipa. **88.** Na wale ambao wanapenda maovu, they don't pay. **89.** Yule ambaye anaiba maybe shilingi kumi au mayai that is the person who suffers-lakini wale wanaiba mabilioni katika nchi yetu, oh they go, they are doing very well. **90.**They are doing very well,lakini yule ambaye ni maskini,hajui hata namna gani, he is the one who suffers. **91.** Lakini kumbuka Mwenyezi Mungu lazima atampa tuzo lake siku ya mwisho, wakiwa na Abrahamu. **92.**Tuchukue nafasi hii, sisi kama wakristu, tujue tunapofuata nyota, katika maisha yetu,lazima utalipa. There is no choice. Lazima utalipa kwa uchungu. **93.** Ndugu wakristu,sisi kama wakristu wa hii leo, tuangalie ile nyota na hii nyota hakuna kitu kingine, ni Yesu katika maisha yetu.**94.** Na haitegemei wewe ni baba au ni mama, kumbuka ukiifuata hii nyota haifuatwi haraka. **95.** Tunaambiwa katika somo la kwanza, walitoka Sheba na ubani na zawadi wanakuja kumwona, kumpa zawadi. **96.** Nyinyi sijui mahali mumetoka, mimi sijui. **97.**Na umetoka mbali, umekuja hapa, sio kwa sababu ya ardhi, sio kwa sababu...kwa sababu unataka kusikia neno la Mwenyezi Mungu, la huyo ambaye ni nyota. **98.**He is the shinin... shining star, ambaye sio mtu mwingine, umpe shida zako, umpe raha zako, ili uwe

pamoja na hiyo nyota. **99.** Mama... mamajusi of course tunajua there were so many stars, sio hiyo peke yake, lakini walichagua that particular nyota. **100.**Sisi nasi kama wakristu tuna maisha mengine mengi, yenye furaha, maisha mengine mazuri na ma malimwenguni lakini tunafuata hiyo nyota, tunahitaji that particular nyota. That particular nyota inaitwa Kristu, tuichukue. **101.** Nyota ndio hiyo Kristu. Kufuata Kristu sio rahisi. Kuna marafiki wangu, marafiki wako na wa yule mwingineambao unafikiri ni wazuri, lakini ni Herode. **102.** Wanataka kukutoa katika ile neema ya kwenda kufuata ile nyota. **103.**Kuna wengi ambao wanahubiri nyota na kuiona nyota kama injili. **104.** Lakini kuna kuna wengi kwa sababu ya Herode wa wakati huu, wanadanganywa na hawana neema ya Mwenyezi Mungu. **105.** Tuombe mwenyezi Mungu atupe nguvu ya kuendelea tu hii nyota moja. **107.** Tunafuata huyo Kristu anahubiriwa katika injili. **108.**Namalizia kwa kuwambia wale wano...wanao ambao wakati huu wana shida ya school fees,hata uniform,hata kiatu ya mtoto tuwaombe ili Mwenyezi Mungu awaendeleo kuwaonyesha nyota. **109.**They should not give up! Waendeleo kukazana na kuomba Mwenyezi Mungu ili wapate karo ya watoto wao, wapate uniform na wa ...wasikate matumaini kwa sababu ya waherode wa kisasa. Tusimame.

## MATINI C

### MAHUBIRI: SEVENTH DAY ADVENTIST – BAHATI

1. Mhubiri:Mnasemaje watu wa Mungu?

Waumini:Amen

Mhubiri:Mnasemaje?

Waumini:Amen

2 yah – bila neema ya Mungu, hata mimi nisingesimama hapa. 3. Kwa hivyo waimbaji, waimbaji Mungu awabariki, waimbaji Mungu awabariki sana. Amen

4. Oh – Ahsante sana.

Ah ... ninapenda niseme kitu kimoja leo, ninahitaji kuwapatia somo muhimu sana. 5. Ila naomba neema ya Kristo iweze kufanya kazi maishani mwako ili upate kunielewa. 6. Kisa cha somo letu la leo kinasema, “Aibu ya mdhambi kwa kupenda cheo, kutopenda kuaibika vibaya kulimfanya apoteshe watoto wake wokovu” 7. Ni wewe au ni mimi? Aibu ya mdhambi, ilimfanya awakoseshe watoto wake wokovu. Ah wapenzi siku ya leo, ah nihitaji kuwaambia kitu kimoja. 9. Nataka kuwaambia habari za watu wawili. 10. Habari za watu wawili na ninafunga somo langu asubuhi ya leo. 11. Ah ...utangulizi wa somo unasema, siku moja watu wawili walikuwa wakibishana juu ya ukweli wa maisha. 12. Wa kwanza alisema, msichana yule ataolewa na nani? Mbona sura yake nzuri hivyo? Lakini mbichi hivi? 13. Mwingine akamkatiza akasema, huyu msichana alizaa mtoto akamwacha! 14 Mtu wa pili anasema na yule kijana aliyekuwa anatafuta mtetezi mahakamani, ilikuwaje? 15. Kesi yake ilikuwa ngumu. 16. Lakini alipata watetezi wawili. Wawili wakamdanganya wa tatu, aliyekuwa maskini, akamtetea. 17. Karibuni

katika soma la leo. **18.** Wapenzi siku ya leo, nataka kuwaambia vitu vya kuchekesha. Kuna binti ambaye kwa jina alikuwa anaitwa Emacullata, samahani Emacullata kama uko hapa sio wewe! **20.** Huyu binti, alikuwa na akili kuliko wasichana wote secondary moja kwetu huko inaitwa Mwanza Girls. **21.** Huyu binti, Mungu alimjalia kumuumba akiwa sura nzuri. **22.** Inawezekana ah... hata sijawahi kumwona katika wengine maana yule binti alikuwa akiongea, utapenda kumwona aendelee kuongea, aki... akitabasamu utapenda kuona tabasamu yake. **23.** Huyu binti alikuwa anaitwa Emmacullata. Binti wa pekee, ambaye Mungu kwa ufundi alimuumba, akaumba utalam wake pale. **24.** Kama alivyoumba mke wako, kama alivyoumba mke wangu, na wengine ambao hamjapata, iko siku ambayo Mungu atakupatia msichana wa pekee **25.** Emacullata alipokuwa anasoma pale, siku moja shetani akamtembelea. **26.** Aliingia ndani ya vioo. **27.** Afisa wa elimu alipofika pale, binti aliposimama, akamwangalia, jinsi alioyatabasamu, jinsi anavyoongea, oh afisa akasema eh-ndio maana hata wimbo mmoja nime...tunga nikisema – Enyi wanaume msiwachokoze nini? Wanawake. **29.** Yule afisa, afisa akasema, mimi ni huyu. Emacullata. Maskini Emacullata hajui moyoni. **30.** Akamwambia Ema, nakupenda. **31.** Eti unanipenda au unanitamani? Unanipenda au unanitamani **32.** Afisa akamwambia ninakupenda. Ebu sema vizuri afisa – akasema yote. **33.** Aliposema yote, Emacullata akajua tayari eh...eh Emacullata ameisha mzidi mke wake aliyemwacha nyumbani. **34.** Wangapi wanaona wasichana kule town, wanazidi hata wake zao walioacha nyumbani? **35.** Oh – Emacullata alipoona vile, akamwambia afisa, “mimi hapendi mtu, isipokuwa wallet!” Yaani hata uwe na sura mbaya, ukiwa na pesa, twende... si mnajua! **36.** Oh – Macullata, wakaendelea na huyo afisa, ikafika siku moja, Emacullata bahati mbaya akapata mimba. **37.** Akaenda kwa afisa akamwambia – afisa, nina mzigo wako – Afisa

akaangalia – mzigo gani? Akasema, mbona siuoni? Unaona vile ninavyopendeza – akasema, ndio maana nilikuchagua – Apana afisa – nina mzigo wako – nina mimba. Uko na nini? Mimba. Ya nani? Yako. Akasema, mimi ni afisa wa kuajiri watu, waalimu, si afisa wa kuajiri mimba? Akasema, ondoka na nisisikie huu upumbavu tena. **38.** Emacullata akaenda shule, alipofika, ah anafika, ah Emacullata sasa mimba imeanza kuonekana maskini wa Mungu! **39.** Akufukuzwa shule. Alipofukuzwa shule, binti anahangaika, sura nzuri lakini mimba iko. **40.** Alipokuwa amehangaika, akazaa mtoto. Mtoto yule alipomzaa, akakaa naye miezi mitatu. **41.** Akasema sasa mimi naondoka, akaondoka kwanda kwa mama yake, sehemu moja inaitwa ukerewe. **42.** Alipofika, akaandika barua ndefu anamwambia mama, nilipata mimba nikiwa form two, sasa mtoto mjukuu wako huyo – lea mama. **43.** Mimi naenda zangu Dar-es-salaam kuangalia maisha yanavyokwenda, barua ndefu. **44.** Alipofika kwenye mlango, kama hapa, akakalaza katoto pale. Amemaliza kumlaza akamfinya mtoto akalia pale. **45.** Mama akaamka, akatoka ndani, mbona leo nasikia mtoto analia? Analia nje, mtoto analia. Kuja kuangalia, anakuta katoto, barua ndefu. **46.** Kusoma, Emacullata. Mama akashangaa mtoto huyu, si amezaa angekuja tungekaa? **47.** Emacullata akaenda. **48.** Mungu si athumani, kwetu anasema alipokua mtoto yule akasoma na akamaliza form four akachaguliwa kujiunga na chuo kimoja cha Business College Dar-es-salam. **50.** Amekwenda kule, mama yuko Dar, hamjui mtoto, ali... alimwona siku nyingi. **51.** Siku moja, kijana akamaliza course. **52.** Sasa rafiki yake anaenda kumtafutia kaa... nyumba akaenda kwa mama yule yule mama yake mzazi, akasema mama, natafuta nyumba, unaweza kupata chumba kimoja kwa ajiri ya kijana huyu? Kijana mwaminifu. **53.** Mama alipomwona huyu kijana, akampenda. **54.** Alipompenda akamwambia mwanangu utakaa kwangu bure. **55.** Alipokuwa anaendelea

kukaa, mtoto akawa anafanya kazi, akamwambia, usi... usipike chakula nitakupikia, utakula. **56.** Mtoto hajui kinachoendelea ni nini? Mtoto hajui mama yake ni nani? **57.** Siku moja, mama akamwambia ah ... ebu njoo mwanangu. Keti. Akakaa. **55.** Akamuuliza, baba yako na mama yako anaitwa nani? **59.** Alipomuuliza, mtoto akalia. Akamwambia mama, baba na mama siwajui. Kwa nini? Nasikia tu mama, baba alim... alimpatia mimba mama, akiwa mwanza. **60.** Akiwa Mwanza? Sekondari moja inaitwa Mwanza Girls. Na huyo mama alikuwa anaitwa Emacullata. **61.** Alipotamka, mama akaanza kulia, lakini aibu iko ndani yake. **62.** Hapendi kumwambia mimi ndio mama yako. **63.** Wakati analia, boyfriend wake akaingia. Unafanya nini hapa? Na huyu ni nani? Akapigwa makofi. Kijana yule akaondoka. **63.** Siku ya kwanza, sasa anapanga leo nitamwambia, mimo ndio mama yako Emacullata. Wakaanza kuongea, walipoanza kuongea, kumbe kijana amefanya vituko. Ameiba pesa na akaua mtu. **65.** Kwa kukosa nini? Malezi kwa sababu hakuwa na baba wale hakuwa na mama katika malezi. **66.** Askari wanafika wanamwambia, kijana uko chini ya ulinzi. Twende. Anaondoka. **67.** Mama anabaki ameduwaa, anaangalia jinsi mambo yalivyokwenda. **68.** Kuona vile, kijana alipokwenda kule, mama akachelewa kufika akakuta ame... ame... ameandikiwa kwamba kwa sababu ameua, itabidi na yeye afe. **69.** Aibu ya mdhambi, ilimfanya mama amkoseshe mtoto wake wokovu. **70.** Wapenzi, nataka kuwaambia leo, nataka niwaambie leo wapenzi, anasema ndugu zangu na mama mnaokaa na watoto wetu, mama alikaa na mtoto siku tatu, hivi mnajua mtoto ni nini-eh. **71.** Mara ngapi umekaa na mtoto, ndani ya maisha yako, ndani ya moyo wako, ukishindiwa kumweleza mtoto yule hata kile kilichomo ndani ya maisha yako? **72.** Anasema, Emacullata ndiye alikuwa mama, alikuwa mama wa mtoto, lakini alishindwa kumweleza kwamba mimi ndio mama yako.

73. Ndivyo hivyo leo, ni mara ngapi tumemwacha yesu mlangoni tukaangalia wakati tukienda kutenda dhambi? 74. Mara ngapi umemweka Yesu, kwenye mlango unakimbia kutenda dhambi na barua ndefu yenye maandiko? Na mtoto analia pale? Mara ngapi unaondoka kwenda kutenda dhambi na watu wanaumia? 75. Anasema, mara watu wanapoumia na kuona aibu, na kushindwa kuungama, Kristu mbinguni anaungama, anahuzunika. 76. Emacullata alishindwa kumweleza mtoto wake kwamba yeye ndiye mama. Kwa sababu dhambi ilikuwa maishani mwake. 77. Leo ni watu wengi wameshindwa kuungama dhambi zao, na wanatembea na dhambi. 78. Biblia yangu nikisoma katika kitabu cha Timotheo ah tano – ya kwanza tano msitari wa ishirini na nne anasema, dhambi za watu wengine ziko dhahiri zatangulia kwenda eh... hukumuni. Wengine dhambi zawafuata. 79. Hizi ndizo zilimfanya Emacullata ashindwe kumwambia mtoto wake kwamba wewe, wewe, mimi ndimi mama yako. 80. Anasema hivi, wengi, wengi wetu tumezaa watoto na kuwaacha mlangoni. 81. Wengine, maafisa wanapoingia moyoni, yawezekana afisa huyu amekaa moyoni mwako ni afisa wa wizi wa zaka. 82. Yawezekana kabisa unaye afisa ambaye ni uvivu, kama ilivyokuwa Emacullata, labda yawezekana ni uchoyo au ni masengenyo yamo ndani ya moyo wa... wako. 83. Au ni kuvunja sabatu, au ni kufanya kazi siku ya sabatu, au una maboyfriend hata ishirini 84 Yawezekana ni afisa yuko ndani ya moyo wako. 85. Na kwa sababu huyu afisa yuko ndani ya moyo wako, imeshindikana hata kumwabudu Mungu vilivyo. 86. Na imeshindikana hata kumtolea Mungu zaka ilivyo. 87. Na imeshindikana hata kumwambia Mungu kama Mungu alivyotaka. 88. Wapenzi ebu tuangalie fungu letu. Nataka tulisome fungu letu. Unajua watu wengi hawajui fungu hili. 89. Sitakwenda kwingine, au nataka kulisoma hili fungu. Luka 14: tusome kwanza (kimya) Luka 14: msitari wa kumi, wa

ishirini na tano, anasema hivi “Makutano wengi walipokuwa wakifuatana naye yeye aligeuka akawaambia, mtu akija kwangu na yeye hamchukii baba yake, na mama yake, na mke wake, naam, hata nafsi yake mwenyewe, hawezi kuwa mwanafunzi wangu” 90. Unajua wapenzi hili fungu ukirifikiria kwa haraka eh... huwezi kuelewa. 91. Ebu fikiri ni wakati huo Yesu amelisha watu kwa... kwa mikate na samaki, na wakati ule watu walikuwa wanapona, lakini sasa amekutana – watu wanamtaka wengi kabisa. Lakini kwanza yesu anageuka anawaambia, mtu yeyote, akitaka kunifuata, lazima amchukie baba, na mama yake, na mke wake, na watoto, na ndugu zake, hata nafsi yake. Hivyo akifa sasa atakuwa mwanafunzi wangu. 92. Ni wangapi hapa wanawachukia baba zao? Nione kwa mkono. Ni wangapi wanawachukia wake zao, yule unalala naye kwa kitanda? Wangapi wanawachukia watoto? Wangapi? Eh wangapi wanawachukia ndugu zao? 93. Nawauliza tena swali lingine – ninyi ni wanafunzi wa nani? 94. Ndio maana nawaambia wapenzi, lipo somo gumu sana leo, aduhuri ya leo! Kwamba ni vigumu kum... kuchukia mke wako. 95. Labda nimwambie kitu kimoja. Labda nimalize na huyu mtu. Nataka nifunge na huyu mtu 96. Kuna rafiki yangu mmoja namwita rafiki. Alikuwa anaitwa Shida. 97. Nimewaambia habari za Emacullata, sasa niwaambie huyu wa pili – Shida. 98. Huyu Shida, alipata shida. Shida ni jina lake akapata nini? Shida nyingine. 99. Alishitakiwa mahakamani na aliposhitakiwa mahakamani, Shida alitaka mtetezi wa kumtetea, lakini alikuwa na rafiki watatu. 100. Rafiki wa kwanza alimpenda mno, unajua tukisema sis waswahili, eh eh.. tunaofahamu Kiswahili cha huko – ninakupenda mno, yaani anakupenda upeo, anakupenda kuliko vingine. 101. Alafu rafiki wa pili, alimpenda sana. Nakupenda sana. 102. Rafiki wa tatu alimpenda kidogo. 103. Sasa akaenda kwa ndugu rafiki – unajua bwana rafiki nilikupenda mno-nimepata case na ukitoa utetezi

wako hakuna shida. Tunaweza kwenda? **104.** Akasema ndio, wakaenda. Akamtoa kwenye mlango wake. Pale nje. Alipofika hapo akamwambia, rafiki yangu, utetezi wangu mwisho ni hapo. Kwa hivyo, nenda mahakamani salama. **105.** Ah, na nilikupenda mno hivi? Umenifikisha kwenye mlangoni, urafiki gani huu. Akasema nenda. **106** Akarudi kwenye nyumba. Akamwambia rafiki yake, akamwambia unajua nilikupenda sana, sasa naomba ukanitete mahakamani – oh akaamka- Twende Shida. Bwana Shida usiwe na Shida – twende. **107** Akaenda mpaka mahakamani akakaa. **108.** Hakimu akasema, mtetezi wako yuko wapi? Akasema ah... ah akasema yule pale; come! njoo, njoo. **109.** Akasema, bwana hakimu, mimi namtetea kwa kumleta mpaka mahakamani. Lakini sitasimama kwenye kizimba ili kusema yale ambayo ni – alifanya. **110.** Akasema, nilivyokupenda hivyo? Hakimu anatoa wito – kuna mwingine ambaye anaweza kukutetea? **111.** Akasema yupo! Kimbia – akakimbia alipofika, akamwambia, unajua wewe nilikupenda kidogo – si unaelewa? Akasema ndio. Sasa twende ukanitete. **112.** Akasema usiwe na wasiwasi. Akaenda mpaka mahakamani. Alipofika mahakamani, moja kwa moja mpaka kizimbani. **113.** Akasema hakimu mimi ndiye rafiki ambaye ninajua huyu aliyetenda na nitakachokisema, hakimu utakubali. **114.** Hakimu akashangaa, hawa wengine wamefika wamekaa. Huyu anakuja direct ah ikawa kama ni direct – amefika pale sasa ikaja case sasa. **115.** Nataka niwambie, alipokuwa anaeleza yule rafiki wa tatu, huyo ambaye nataka kumweleza, na unielewe wewe, hakimu akamwambia – uko huru, nenda nyumbani. **116.** Sasa ndugu zangu wapenzi, rafiki yetu wa kwanza tunayempenda mno jina lake anaitwa shuguli na pesa. **117.** Ndio maana kazi ya bwana haiendi mbele. Ndio maana nimeona mzee wa kanisa anauliza – wangapi wako tayari kuchangia kanisa letu? Wengine wame... wameweka tu mikono kwa sababu

tunampenda mno! **118.** Rafiki wa pili tunayempenda sana ndiye huyu. **119.** Huyu ni baba, mama, mjomba, shangazi na jirani. **120** Wapenzi yupo rafiki wa mwisho, ambaye tunampenda kidogo na jina lake ni Yesu Kristo mwana wa Mungu. **121.** Huyu ndiye tunampenda kidogo. Ndio maana hata ninapokuwa ninahubiri, au ninapokuwa kanisani, ninapoambiwa niende kanisa – kwa sababu sijauona uzuri wa kule – siwezi kufanya. **122.** Ndio maana mwimbaji anaamua kuja kuimba anamwambia Mungu wakati ana “boyfriend” kwa nini? Yaani unamwambia Baba wa Mbinguni wakati una boyfriend! **123.** Unaamua kwamba upewe kazi kanisani wakati unaiba zaka? Lini mwizi akaenda mbinguni? Tunampenda kidogo. **124.** Na kwa sababu hiyo, nakwambia, ndani ya kanisa leo kuna watu wawili, wengine wataandikwa P.O. Box Uzima wa milele na wengine wataandikwa P.O. Box Mauti ya Milele. **125.** Na tunahitaji toba ya pekee, kabla Yesu rafiki yetu hajatoka sehemu ya kututetea. Mungu na awabariki. Tuombe.

## **MATINI D**

### **MAHUBIRI: GOSPEL REDEEMED CHURCH - BAHATI**

Mhubiri: Bwana asifiwe?

Waumini: Amen

Mhubiri: Halleluya!

Waumini: Amen

Somo letu asubuhi ya leo linahusu baraka

1.Basi ningetaka kuchukua nafasi hii,- mwambiye aliye karibu nawe, usikose baraka hizi.

waumini:(usikose baraka hizi)

2.Baraka hizi ambazo tumesoma zimeandikwa, kama Biblia yako imeandikwa hivyo na

kama tumesema hizo baraka ni zako, na ukiangalia sijui ni wangapi wako na hizo

baraka,ambazo tumesoma hapa.3.Ukiangalia pengine hauna kitu, (kimya) naweza kuona

katika hizo baraka ni zako. –kwa sababu hautafahamu na kuelewa ya kwamba baraka hizi

ni zako.4.Na umekosa baraka sasa.5.Kwanza siku hii ya leo, tungetaka tuelewe namna ya

kuchukua baraka zetu.6.Tuweze kuelewa jinsi Bwana alivyosema katika baraka,

tunaweza kumwambia hizi baraka ziliangukia wana wa Israeli, na mimi sio mwana wa

Israeli, itakuwaje mchungaji nami nihusike katika hizi baraka?7.Unajua katika ukoo wetu

tunaishi katika laana.8.Wacha nikwambie siku ya leo, na usikie sawasawa wewe siku,

ambayo Mungu, alikuteua wale ambao watakuwa katika hii jamii ya laana, utolewe

katika jamii ya laana, ukaingizwa katika jamii ya kubarikiwa.Amen

Waumini: Amen.

9.Utatolewa katika jamii ya laana- ni kweli baba alikuwa mchawi, watu wenu walikuwa wachawi, na watu wa jamii kama hizo huishi katika mambo ya laana.10.Lakini wewe, ukitolewa pale, nakutoa pale, uingie katika nchi ambayo sasa nakuzungumzia,ambayo ni nchi ya haki, watu wanatolewa katika laana za uchawi,za majini, wewe unakuwa kiumbe kipya. Sema Amen.

Waumini : Amen.

11.Kwa hivyo hizo laana hazifuatani na wewe lakini jinsi unapoingia katika nchi ya baraka, ambazo tunaitiwa na Biblia, sasa nitakwambia.

12.Bwana akasema katika kitabu cha mwanzo, ishirini na mbili na kumi na nane, "I will choose you [...] all nations on earth will be blessed because of you are obeyed to me." Halleluya!

Waumini:amen.

13.Huyo ni nani? huyo ni Abrahamu, we are living and we are saved because of Abraham. Kuokoka kwetu na kuishi kwetu ni kwa sababu Abrahamu alikuwa mtu wa kutii.14.Abrahamu wakati Mungu aliona watu wamekuwa waovu, alimchukua Abrahamu,ili dunia ikaweze kukombolewa, kukutia katika hali sawa na Abrahamu. Say Amen!

Waumini :Amen

15.Basi iburahimu aliamrisha, akaambiwa toka nchi ya watu wenu, na a... Aburahamu hakuwa mtu wa maneno.16.Aliposikia sauti ya Mungu, yeye alitoka mara moja, na akaanza safari yake ya kwenda, maana Mungu hangeweza kumbarikia katika nchi hiyo ilikuwa na uovu mwingi.17.Sasa Abraham akatoka , na akaenda zake,na huko njiani akienda ndiposa Bwana alimnenea mambo saba –so I will go through this very quickly –

vile alimwambia.**18.** I will make you into great nation-That's number one.Abraham anaambiwa na Mungu, nitakufanya uwe taifa kubwa sana.**19.**I will bless you na Bwana atakubariki.**20.**I will make you, your name great- na jina lako litakuwa kubwa.**21**You will be a blessing –wewe utakuwa baraka, Bwana akamwambia.**22.** Five, I will bless those who bless you- wale ambao watakuriki nami nitawabariki .Amen !

Waumini: Amen

**23.** Number sita, whoever curses you, I will curse.Brother you are a serious man, hakuna mtu akuchezea atapita, if you are living like Abraham. Ukiwa mwaminifu na mtiifu.**24.**Mungu atasimama nawe, hakuna laana, hakuna uchawi utakuwa njia lako and stall your progress. Amen.

Waumini :Amen

**25.**Ya mwisho, all people on earth will be blessed through you- watu wote watabarikiwa kupitia kwako.Halleluya.

**26.**Basi, huyo ni Abrahamu ambaye ndiye baba wa kizazi hiki,akaambiwa wewe nitakufanya kuwa taifa kubwa.**27.**Na pia ya mwisho, ya saba inasema, dunia yote, watu wote wa dunia watabarikiwa kwa ajili yako.**28.** Ndiposa akasema, kutoka katika uzazi wako, nitaweza kubariki watu wengi wa dunia.**29.** Sasa nataka kila mtu asikie sawasawa, kwa sababu Yesu Kristo,alizaliwa kutoka ukoo wa Abrahamu.Halleluya!

Waumini:Amen.

**30.** Kwa hivyo kupitia katika Yesu, Kristo kanisa inaweza kubarikiwa.**31.** Maana alisema ukitaka katika usawa wako,watu wote wa dunia watabarikiwa.Amen

Waumini:Amen.

32.Kwa hivyo yeyote yule amwaminiye Yesu, kama mwokozi wake, baraka hizi ni zake.33.Ni wangapi hapa ambao wanaamini Yesu ni mwokozi wao? 34.Unasema Yesu ni mwokozi wa maisha yangu.(kimya) God bless you.35. Hizo baraka ni zako mpendwa siku ya leo.36.Lakini kitu ungetaka kujua ni namna ya kwenda kuchukua hizo baraka na kukaa nazo.37. Maana inakubidi ujue, Ibrahimu aliambiwa na Mungu kama wewe hautageukia mimi, kama wewe hautageukia mambo ya nchi wewe ulienda, tunaona Ibrahimu alipokuwa akitoka katika nchi kule, alichukua mtu mwingine wakaenda na yeye.38. Na wakati huo walikuwa na huyo mtu mwingine, baraka zikakosa kuonekana.39.Hautakuwa na uhusiano na Mungu, kwa sababu kulikuwa na kutoamini, na hayo yalikuwa katika matamshi yake.40.Kuna kutoamini kwingi na ndiposa baraka zinakosa zaidi, miujiza inakosa zaidi,maana kuna watu wanasema, toka-come, go out-come in,go out-come in-and such prayers will almost make you to be in one place.41.Maanake sasa unamwambia toka –anatoka, come-anacome.42. Kwa hivyo Ibrahimu alipoachana na huyo ndugu, wakati huo alianza kuona heshima lake,zikamshukia.43.Tunasikia ibrahamu alikuwa amebarikwa, alikuwa na pesa nyingi,alikuwa na punda wengi, alikuwa na ngamia wengi, alikuwa na kila kitu na alikuwa mtu wa kupeana.44.Biblia inasema, you will be a blessing. Ibrahimu alikuwa mtu wa kupeana na kwa sababu alikuwa mtu wa kubless watu, basi baraka zikamshukia.45.Kwa hivyo siku ya leo wapendwa, jambo ningetaka ujue ni kitu kimoja, ya kwamba kwa muda mrefu sana kila kukicha umetosheka na kuishi na umasikini ulio nao.46.Lakini Mungu, hakukuumba uishi katika hali ya umasikini.47.Sio furaha ya Mungu kuona watoto waliookoka wakae katika hali ya kushindwa na dunia.48.Tungekuwa tumeshinda dunia, maana Mungu ana mpango mzuri,

kwetu.**49.**Biblia tumesoma, katika maisha yako, ungetaka kubarikiwa na hiyo ndiyo kusudi ya Mungu, ili akuokoe na alikuambia utoke katika ukoo wenu.**50.**Maana ukoo wenu wa laana ,akakwambia utoke atakubariki.**51.**Lakini kuna kitu kimoja kinazuia baraka zako siku ya leo,. maana hufahamu, unafikiria haya maandiko iliandikiwa mayahudi.**52.**Wewe ndiye Myahudi wa leo sasa-haya maandiko ni yako, baraka ni zako.**53.**Na ndipo tukasoma, ikatwambia, you will be blessed as you come out, as you come in .**54.**Kwa hivyo mpendwa, ingetakikana uonekane ukibarikiwa ukitoka nyumbani, kwenda kazini zile ni baraka,kurudi, zile ni baraka.**55.** Na Bwana anasema, ataweza kubariki wewe na mali nyingi, na watoto wako na wewe hamtakuwa na shida, hamtakuwa wakishindwa shuleni.**56.**Wakirsto watoto wetu ndio wangukuwa number one in the classes. They should be in the top tens.Amen

Waumini: Amen.

**57** They should be in the top tens. If they are not there, brothers its high time you go to your knees, maana Bwana ameahidi ya kuwa watakuwa top tens, so we should be top tens in Kenya.Maana tunaamini baraka ni zetu. Halleluya.

Waumini: Amen

**58** Kwa hivyo, siku ya leo Bwana anatunenea juu ya baraka.**59** Na bwana angetaka kuwabariki kwa njia ya juu sana.**60.**Maana anasema mwakani huu, ataenda kubariki watu.**61** Lakini kitu kimoja ningetaka tuwe ikiwa baraka zako unapokea siku ya leo, utanza kuzi... endelea kuzipokea lazima uwe mtu wa kutii, lazima uwe mtiifu.**62** Lakini kitu kimoja tuliongea mwakani tulisema, you must be committed to the house of God. And second, you must be faithful, to the house of God.**63** .Ni wangapi wanasema i must get my blessings this year? ni wangapi? Inua mkono sasa.**64** Unataka kuniambia utakuwa

mwaminifu, utakuwa mtiifu katika nyumba ya Bwana-that's you are saying?Basi baraka ni zako.**65** Na mungu atakubariki –kwa hivyo leo ni siku ambayo bwana anataka kukubariki..Siku ya leo Bwana angetaka abariki kanisa,tuweze kubarikia watu.**66** Maana Afrika tuna tabia mbaya kwa sababu tunataka kushinda katika hali ya laana.**67** Tuna tabia ya kuombaomba, na ile ni tabia ya umaskini. Once you become a beggar, you are a beggar throughout your life.**68** Sijaona maskini anaomba pale river road miaka yote na “kungurukunguru” amenunua nyumba. If you know one, tell me. A beggar is always a beggar throughout.**69.**Kama tumejidunisha na kuwa waaminifu, na kutoa katika nyumba ya bwana, wapendwa tungeona baraka zetu.**70.**Bwana angeamuru kutoka mbinguni baraka zako.**71** Lakini, hii tabia ya kulialia, saa zote ni kulia, ni kulia, wacha nikwambie, God has lost your plans so that you are cursing yourself.**72** .Brother ametuambia asubuhi, the Lord has gone before you, so why should you cry? **73.**Hakuna haja ya ku... kulia mbele ya Mungu! .Ni heri umwambie Bwana, nashukuru kwa sababu Bwana uliniokoa, ukanifanya kuwa tajiri, mimi niko tajiri, mimi ni tajiri. Kuanzia leo, pronounce wealth in your life! **74** .Sio kuanza kulia saa yote.Haki mimi mguu wangu,mimi mguu, mguu nini? Ambia Yesu I love you because I am ill.nimepona.**75** Huu ni wakati wa baraka wapendwa.**76** Unajua, marekani, brother you will just bare with me, they just don't respect Africans.Americans, I will come there- but I am sure they don't respect us.**77** Kwa sababu tuna hiyo tabia mbaya ya kuomba.**78** Hiyo tabia ya kuomba now and then, hiyo ndiyo imekusumbua katika njia zako.**79** Hiyo ndiyo imekuletea shida katika nyumba yako.**80** Kila wakati “kasuku”! Usiombe! Mwambie Bwana anayekuangalia na utaona mkono wa Bwana. Amen.

Waumini: Amen.

**81.**Lakini lazima uwe faithful na mwaminifu. You must be committed to the house of God and you must be faithful, and then God will release the blessings to you!

Alleluya!

Waumini:Amen.

**82.**Siku moja nilikuwa mahali, na Mungu akanigusa sikuomba siku hiyo .**83**

Tulikutana na brother mzungu town, nikamwambia twende kwa chai tukangia kwa

chai akitaka kulipa kwa sababu anajua mwafrika kila siku ni kulipiwa, nikamwambia

nimelipa, akashangaa.**84** Nilikuwa nimebeba yeye na gari yangu, sikumwambaia

aweke petroli,akashangaa.**85** Tukaenda tena mahali pengine, nikamwambia tukule

chips –akaniuliza, “we have eaten, are we going to eat again?” Nikasema we are

going to eat again, tukakula, nikalipa.**86** .Huyo mzungu alienda akasema, kwani

Kenya kumekuwaje? Mimi ninajua mwafrika kazi ni kungonjea mzungu alipe.Amen.

Waumini:Amen.

**87** Hiyo ndiyo tabia ya mwafrika.Toa hiyo ndani yako na usikubali mtu akulipie

chakula mzungu au mwingine, kama una pesa lipa kwanza. And that’s the way we

will be blessing our people. And when you become a blessing to other people God

will command a blessing. Alleluya. Sema Amen.

Waumini: Amen.

**88** Jameni ujumbe wa leo ni mtamu sana maana ni njia ya kubarikiwa.**89** Hicho uko

nacho kintosha kutumikia Bwana.**90** .Hiyo shilingi yako mia moja inatosha kutoa

fungu la shilingi kumi na kutoa sadaka shilingi ishirini. Amen.

Waumini: Amen.

91 Usingojee milioni ndio umtumikie Bwana, kuwa mwaminifu katika nyumba la Bwana and be committed and then you shall see God. 92. Nikimaliza ningetaka kuomba kuhusu baraka. Na kabla sijaomba, there is someone here, God cannot command a blessing upon you even if you are faithful, you are committed, God cannot command a blessing upon your life. 93 Please you are here and you know within yourself, you have not led to confession upon Jesus Christ as your personal saviour, nakwambia yale nimeongea hayako njiani mwako. 94 Lakini unaweza kuwa mmoja wetu. 95. Kama uko hapa na hujaamini Yesu, singetaka upitiwe na baraka ambayo Bwana ataenda kutoa siku ya leo. 96 .Ningetaka uungane na wapendwa wengine, ambao wameapa kuwa waaminifu, unaweza kuwa mwaminifu, utoe pesa, lakini bado hujasema Yesu ni mwokozi. Kuenda kanisani kutoka sio neno, unahitaji huyo Yesu ili akulishe maishani mwako- kuna yeyote kabla sijaomba? Kunaye? Funga macho tuombe.

## KIAMBATISHO II

### MASWALI YA BALAGHA

#### MATINI A

1. Na kabla niendeleo sana ku ... kufafanua zaidi ya hayo, ningese... nge-taka kusema (kimya) upendo ndio nguzo ya familia yetu. Kwanzia mtoto, kwenda mama, kufika mzee.

Na kwa nini nasema namna hiyo? Nikiangalia...

2. Lakini kabla mtumishi aje, tutaanza kuangalia, kwa nini mtumishi anaingia? Tunaona Mungu, akawapenda wana wa Israeli tangu jadi...

3. na kwa sababu wana wa Israeli walikuwa wameshikwa mateka na wababiloni. Nataka kumaanisha nini? Nataka kumaanisha...

4. Lakini kwa kuchangisha, au kutafanya sisi tuanze kuuliza, shida hii ni nini? Tunasikia elfu...

5. Anaanza kuyumba, ananza kusikia kweli ... he is not stable in his working place. Kwa sababu gani? Hajui litatokea nini aende retirement!

6. Amekuonyesha njia na umepita ... Kwa sababu gani? Kwa sababu Mungu yuko pamoja nawe.

#### MATINI B

7. Kwa hivyo wakristu somo letu la kwanza linataka kutwambia nini wayahudi wa kisasa? Ya kwamba...

8. Hata wakati wa nabii Isaiah walikuwa hivyo tu, sisi tu ni sisi tu, ... Are we not doing the same thing today? Maybe Wakikuyu wanataka...

9.Ukabila hauingii katika swali hilo la mukristu. Kwani unafikiria ati kwa sababu Wakikuyu ni wengi in this government mbinguni watakuwa wengi? That is not the way.

10.ebu kwanza muende mukamwone halafu mpitie hapa, hata mimi nitaenda kumsujudia...Which, which president angefanya hivyo? Hata wale...

11.Kuna huyu ambaye amezaliwa, ebu tujiuliuze leo wakristu wenzangu, wewe nyota ambayo unaifuata kila wakati, ambayo ni Kristu unaifuataje?

12.Endapo unafanya mambo mazuri...lazima utaumia, lazima utalia siku moja, ulipe. Si hata Yesu alifanya hivyo? Alikuwa kutukomboa...

### **MATINI C**

13.Kisa cha somo letu la leo kinasema, "Aibu ya mdhambi kwa kupenda cheo, kutopenda kuabika vibaya kulimfanya apoteshe watoto wake wokovu" Ni mimi au ni wewe? Aibu...

14.Wangapi wanawaona wasichana kule town wanazidi hata wake zao walioacha nyumbani?

15.Mama akamka akatoka ndani, mbona leo nasikia mtoto analia? Analia ...

16.kumbe kijana amefanya vituko.Ameiba pesa na akaua mtu. Kwa kukosa nini? Malezi kwa sababu...

17.Mara ngapi umekaa na mtoto ndani ya maisha yako, ndani ya moyo wako, ukishindwa kumweleza mtoto yule kilicomo ndani ya maisha yako?

18.Ndivyo hivyo leo, ni mara ngapi tumemwacha Yesu tukaangalia wakati tunaenda kutenda dhambi?

19.Mara ngapi umemweka Yesu, kwenye mlango unakimbia kutenda dhambi na barua ndefu yenye maandiko?

20. Mara ngapi unaenda kutenda dhambi na watu wanaumia?

21. mtu yeyote akitaka kunifuata, lazima amchukie baba, na mama yake, na mke wake,...

ni wangapi wanawachukia wake zao, yule unalala naye kwa kitanda? Wangapi wanawachukia watoto? Eh...wangapi wanawachukia ndugu zao?

22. Nawauliza tena swali liingine-ninyi ni wanafunzi wa nani?

23. Huyu Shida, alipata shida. Shida ni jina lake akapata nini? Shida nyingine.

## **MATINI D**

24. "I will choose you posterior all nations on earth will be blessed because you are obeyed to me" Huyo ni nani ? Huyo ni Abrahamu...

25. Yeyote yule amwaminiye Yesu, kama mwokozi wake, baraka hizi ni zake. Ni wangapi ambao wanaamini Yesu ni mwokozi wao? Unasema Yesu ni mwokozi wa maisha yangu.

26. Unataka kuniambia utakuwa mwaminifu, utakuwa mtiifu katika nyumba ya Bwana. That's what you are saying? Basi baraka ni zako.

27. Brother ametwambia asubuhi, the Lord has gone before you, so why should you cry? Hakuna haja ya ku...kulia

### KIAMBATISHO III

#### KUCHANGANYA MSIMBO

- 1.Ukiwa mtoto umefanya mtihani wa kidato cha ...(kimya) eh...eh standard eight mwaka uliopita,...
- 2.Yeye anauliza,na inaweza kufika wakati mmoja jina langu liingie kwa computer ya retrenchment?
- 3.Ananza kuyumba, ananza kusikia kweli ... he is not stable in his working place.
- 4.Kwa sababu gani? Hajui litatokea lini aende retirement!
- 5.Nataka kukwambia wewe ukimaliza form four, wewe umemaliza masomo yako...
- 6.... Mama ataweza kupata fedha ya kuninulia kitabu, ataweza kupata fedha ya kuninulia uniform.
- 7...na mambo haya yatategemea individual yatategemea wewe·haitegemei sisi katika ule upya.
- 8.kwa mtakatifu Mathayo ambaye anatwambia si kama story. It is a historical fact ambapo hawa manabii na mamajusi wakuwapo.
- 9.Ya kwamba huyu ambaye amezaliwa anatoka katika “mbari” ya Yuda ni mtawala.
- 10.Na ni Mungu wa kila mtu . He is not a situational God.
- 11.Na kuona mwanga inategemea wewe uko macho namna gani-you cannot be forced.
- 12.Tusiwe kama mayahudi ambao walisema Mungu ni wetu, we cannot share our God.
- 13.Tukifikiria ya kwamba Mungu aliyezaliwa ni wa wakatoliki tu, salvation is only for catholics, tutakuwa tumemiss the vote.
- 14.Ukombozi umefunguliwa kwa wale ambao wana nia njema. For those of good will.
- 15.... nitakuwa mimi ni mukatoliki, Mungu ni wangu lakini akikwambia ufanye hivi, you share, unashy kutokana na mambo hayo...

16.Lakini kofia hiyo inashikishwa na inataka kuonyesha huyo mtoto si wa kawaida, ni mtoto wa myahudi na ni mtoto ambaye ana urithi. He is of a chosen race.

17.Wayahudi si kama sisi,hawacha...hawachanganyikani. Myahudi ni Myahudi period. Hakuna haja ya kuchanganya. Mungu wake ni Mungu wake period hana Mungu mwingine ni huyo tu.

18.Kwa sababu Kristu ni wa kila mtu, either uweke kofia or you are chosen or you are not chosen, Mungu, ni Mungu wetu, wa kila mtu.

19.Either tunampenda au hatupendi Mungu, Mungu anatupenda.the love of God is dynamic, it is not static. Upendo wa mwenyezi Mungu si wa kusimama, ni upendo unaendelea.

20.Are we not doing the same thing today? Maybe Wakikuyu wanataka next time, the president lazima awe Mkikuyu, ati kwa sababu ndio wengi. Next time, lazima Mjaluo awe president, next time Mkamba awe president, next time, lazima awe mm...Mmeru au lazima awe Mkalenjini. Hakuna wimbo mwingine tunaimba! Five years zimeisha, ni hiyo tu , president, president, president president!

21.Wakikuyu wamepata, Wakalenjini wamepata, lazima achaguliwe, we need to ask ourselves, katika maisha yetu,tuwe very serious ya kwamba sisi ni taifa moja, it does not matter yule atakuwa rais ni nani, au MP ni nani, kwa sababu sisi ni wa Mungu mmoja.

22.Mbona hamuulizi padre wetu ni Mkikuyu, next time lazima awe Mjaluo, ah- not in the catholic church. Au tuseme askofu mkuu katika nchi hii ni Mkamba, next time tuchague Mkikuyu- that is not a catholic church.

23.Na ndipo wakati mwingine we make a bladder katika maisha yetu.

24. And we waste a lot of money tuki... tukio... tukiongea mambo hayo. Five years gone na ni hiyo tu!
- 25.... hatusemi hivyo, because we share one God.
26. Tunakumbuka mimi tu kama vile Myahudi alisema ni mimi tu and we cannot share.
27. Ebu tukumbukange hivyo. Either you are out or you in the church, sisi ni wakristu.
28. Kwani unafikiri ati kwa sababu Wakikuyu ni wengi in this government mbinguni watakuwa wengi? That is not the way!
29. Wakristu ambao ukabila, it is not in their mind, hata tunapokuja kupokea, sio kwa ukabila, tunapokea Kristu tu -nothing else.
30. Na hapo ndipo huyo anawambia hawa mamajusi kwanza because I am not sure, hata siwezi kuamini, ebu...
31. Which, which president angefanya hivyo?
32. Kuna huyu ambaye ni Herode, badala ya kuonyesha wale wengine njia anawadivert.
33. Anapokwambia nimetoa dhahabu, uvumba na manemane, automatically unajua yule ni mfalme na ana heshima.
34. Uvumba kama unanukia vizuri sifanyi hivyo nyumbani kwangu, au mahali pengine, there is a special place where tunatumia uvumba.
35. In simple way, in brief, sisi kama wakristu unapofanya mambo mazuri you have to pay for it. Lazima utalipa.
36. Si hata Yesu alifanya hivyo? Alikuwa kutukombo na alilipa in hard wa... way.
37. Na wale ambao wanapenda maovu, they don't pay.
38. Yule ambaye anaiba maybe shilingi kumi au hata mayai that is the person who suffers -lakini wale wanaiba mabilioni katika nchi yetu, oh they go, they are doing very well.

39. They are doing very well, lakini yule ambaye ni maskini, hajui hata namna gani, he is the one who suffers.
40. He is the shinn... shining star, ambaye sio mtu mwingine, umpe shida zako, ...
41. Mama... mamajusi of course tunajua there were so many stars, sio hiyo peke yake, lakini walichagua that particular nyota That particular nyota inaitwa Yesu Kristu tuichukue.
- 42 ... ambao wakati huu wana shida ya school fees hata uniform...they should not give up! waendeleo kukazana na kuomba...
- 44.... Alikuwa na akili kuliko wasichana wote sekondari moja huko kwetu inaitwa Mwanza Girls.
45. Wangapi wanaona wasichana kule town wanazidi hata wake zao waliacha nyumbani?
46. Oh, Emacullata aliona vile, akamwambia afisa mimi, “hapendi mtu isipokuwa wallet!”
47. Anamwambia mama, nilipata mimba nikiwa Form two, sasa mjukuu wako huyo- lea mama.
- 48.... alipokua yule kijana akasoma na akamaliza form four akachaguliwa kujiunga na chuo kimoja cha Business college Dar es salam.
49. Siku moja kijana akamaliza course.
50. Secondary moja inaitwa Mwanza Girls.
51. Wakati analia boyfriend wake akaingia.
- 52....au ni kufanya kazi siku ya sabatu, au una maboyfriend hata ishirini.
- 53.... unajua ndugu rafiki nilikupenda mno. Nimepata case na ukitoa utetezi wako hakuna shida.
54. Akasema ah... ah... akasema yule pale; come! njoo, njoo.

55. Huyu anakuja direct ah... ikawa kama ni direct-amefika pale sasa ikaja case sasa.
56. Ndio mwimbaji anaamua kuja kumwambia Bwana wakati ana boyfriend. Kwa nini? Yaani unamwambia Baba wa mbinguni wakati una boyfriend!
57. Na kwa sababu hiyo, nakwambia ndani ya kanisa leo kuna watu wawili, wengine wataandikwa P.O Box Uzima wa milele na wengine wataandikwa P.O Box Mauti ya Milele.
58. Bwana akasema katika kitabu cha mwanzo, ishirini na mbili na kumi na nane, "I will choose you [...] all nations on earth will be blessed because you are obeyed to me."
59. Huyu no nani? Huyu ni Abrahamu, we are living and we are saved because of Abraham. Kuokoka kwetu na kuishi kwetu ni kwa sababu Abrahamu alikuwa mtu wa kutii.
60. ...kukutia katika hali sawa na Abrahamu. Say Amen.
61. Ndiposa Bwana amemnenea mambo saba-so I will go through this very quickly, vile alimwambia.
62. I will make you into great nation- That's number one, Abraham anaambiwa na Mungu nitakufanya uwe taifa kumbwa sana.
63. I will bless you na Bwana atakubariki.
64. I will make you, your name great-na jina lako litakuwa kumbwa.
65. You will be a blessing-wewe utakuwa baraka Bwana akamwambia.
66. Five, I will bless those who bless you-wale ambao watakubariki na mimi nitawabariki.
67. Number sita, whoever curses you I will curse. Brother you are a serious man. Hakuna mtu akuchezea atapita, if you are living like Abraham.

68. Ya mwisho, all people on earth will be blessed through you-watu wote watabarikiwa kupitia kwako.

69. Unasema Yesu ni mwokozi wa maisha yangu (kimya) God bless you.

70....maana kuna watu wanasema, toka-come, go out –come in, go out –come in and such prayers will almost make you to be in one place.

71. Maanake sasa unamwambia toka –anatoka, come-anacome.

72. Biblia inasema, you will be a blessing. Ibrahimu alikuwa mtu wa kupeana na kwa sababu alikuwa mtu wa kubless watu...

73. Na ndipo tukasoma ikatwambia you will be blessed as you come out, as you come in.

74. Wakristo watoto wetu ndio wangukuwa number one in the classes. They should be top tens.

75. They should be in the top tens. If they are not there, brother its high time you go to your knees, maana Bwana ameahidi kuwa watakuwa top tens in Kenya.

76. Lakini kitu kimoja tuliongea mwakani tulisema, you must be committed to the house of God. And second you must be faithful to the house of God.

77. Ni wangapi wanasema I must get my blessings this year?

78. Unataka kuniambia utakuwa mwaminifu, utakuwa mtiifu katika nyumba ya Bwana – that’s what you are saying?

79. tuna tabia ya kuombaomba, na ile ni tabia ya umaskini Once you become a beggar. you are a beggar throughout you’re your life.

80. Sijaona maskini anaomba pale river road na “kungurukunguru” amenunua nyumba. If you know one, tell me. A beggar is always a beggar throughout.

81...saa zote kulia, wacha nikwambie, God has lost your plans so that you are cursing yourself.

82.Kuanzia leo pronounce wealth in your life.

83.Brother ametwambia asubuhi the lord has gone before you, so why should you, cry?

84.Ambia Yesu, I love you because I am ill. Nimepona.

85.Unajua, Marekani, brother you will just bear with me, they just don't like Africans. Americans, I will come there –but I am sure they just don't us.

86.Hiyo tabia ya kuomba now and then, hiyo ndiyo imekusumbua katika njia zako.

87.Lakini lazima uwe faithful na mwaminifu. You must be committed to the house of God and you must be faithful and then God will release the blessings to you!

88.Tulikutana na brother mzungu town,...

89.Tukaenda tena mahali pengine nikamwambia tukule chips, akauliza, "we have eaten are we going to eat again?" Nikasema, "We are going to eat again," tukakula, nikalipa.

90.Toa hiyo yako na usikubali mtu akulipie chakula mzungu au mwingine kama una pesa lipa kwanza. And that is the way we are a blessing to our people. And when you become a blessing to other people God will command a blessing .

91.Kuwa mwaminifu katika nyumba ya Bwana and be committed and you shall see God.

92.Na kabla sijaomba, there is someone here, and God cannot command a blessing upon you even if you are committed, you are faithful, God cannot command a blessing upon your life. Please you are here and you know within yourself, you have not led to confession upon Jesus Christ as your personal saviour, nakwambia yale nimeongea hayako njiani mwako.

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY